Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

### Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 30 Julai, 2008

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tubaki tumesimama kwa kumbukumbu ya ndugu yetu tuliyemuaga jana.

Waheshimiwa Wabunge, napenda nitangulie leo, baada ya tukio la majonzi la juzi na jana kutoa maneno ya shukrani kwa niaba yenu, kwanza kwa Mheshimiwa Rais wetu ambaye alishiriki kikamilifu jana. Rais wetu amekuwa ni mwepesi kushiriki katika furaha na majonzi ya watu wake, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ushirikiano mkubwa uliotuwezesha kumsindikiza mwenzetu kwa heshima. *(Makofi)*

Naishukuru Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge ambayo kwa pamoja ndiyo ilikuwa kama Kamati ya mazishi na wamefanya kazi kubwa na nzuri kama ambavyo nadhani Taifa limeshuhudia. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Kipekee nawashukuru Kamati yetu ndogo ya matukio ikiongozwa na Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Jenista Mhagama ambayo ndiyo ilisimamia eneo zima la sehemu ya shughuli ya jana. Wamefanya kazi nzuri kwa muda mfupi sana. Namshukuru sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Kamati yake. *(Makofi)*

Mwisho, nawashukuru sana Wabunge, kila mmoja wenu, mmeshiriki vizuri sana tangu juzi, wengine kwa kwenda kule Kisasa kwa nyumbani kwa marehemu, kufariji wafiwa na jana tukaweza kuwa pamoja katika kumsindikiza mwenzetu. Kwa yote haya nasema ahsante sana. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu Chacha Wangwe, mahali pema peponi na azidi kuwarehemu wafiwa waweze kuwa na uvumilivu katika wakati huu mgumu. *Amin.*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:-**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH - (K.n.y. MHE. WILSON M. MASILINGI – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):-**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa Fedha uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2008/2009.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. IBRAHIM MOHAMED SANYA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):-**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2008/2009.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 302

### Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Wilayani

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA (K.n.y. MHE. NURU A. BAFADHILI)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya 2001 – 2003 Halmashauri zilikuwa zikitoa ruzuku kwa vyama vya siasa kulingana na vigezo vilivyoainishwa na Halmashauri hizo:-

Je, ni sababu zipi zilizosababisha kufutwa kwa ruzuku hizo kwa vyama vya siasa Wilayani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ruzuku kwa vyama vya siasa hapa nchini vyenye Wabunge na Madiwani inatolewa na Msajili wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 11 ya mwaka 1996. Ruzuku kwa vyama vyenye Wabunge ilianza kutolewa Julai, 1996 na kuongezwa kundi la Madiwani Julai, 2007 ambayo inalipwa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa ruzuku umeainishwa katika sheria hiyo katika Vifungu vya 16(1)(2) na 17 vya sheria inayompa mamlaka Msajili wa Vyama vya Siasa kutekeleza jukumu hilo na sio chombo kingine chochote. Kwa maana hii hakuna taasisi au chombo kingine kinachopaswa kufanya kazi ya kugawa ruzuku kwa vyama vya siasa bila maelekezo ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya siasa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizomo katika Sheria ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, si jukumu la Halmashauri yoyote hapa nchini kutoa ruzuku kwa vyama vya siasa vyenye Wabunge na Madiwani au kwa kuombwa kufanya hivyo. Suala hilo lilishatolewa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa alikwishachukua hatua ya kusimamishwa kutolewa ruzuku na Halmashauri na kuelekeza sheria izingatiwe.

Na. 303

**Kuimarisha Huduma ya Usafiri kwa Wagonjwa Vijijini**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi nchini wanaishi vijijini ambako huduma za afya ziko kwenye mpango wa kuboreshwa kwa kuwashirikisha wananchi hao:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuimarisha huduma ya usafirishaji wa wagonjwa toka vijijini na kwenye vituo vya afya kupelekwa kwenye hospitali za Wilaya na Mkoa?

(b) Kwa kuwa kwenye Halmashauri ya Sumbawanga, vituo vya afya vilipangiwa magari ya kuhudumia wagonjwa lakini magari hayo hayakutosha vituo vyote, je, ni lini vituo vya afya vya Mwimbi na Matai vitapata magari ya uhakika ili kutoa huduma hiyo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia boti maalum ya wagonjwa vijiji vya Tarafa ya Kasanga kandokando ya Ziwa Tanganyika maeneo ya Kipwa, Kapere, Kalewani, Kipanga na Samazi?

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006, Serikali ilinunua magari ya kubebea wagonjwa *(ambulance)* yapatayo thelathini ambayo yaligawanywa kwa Halmashauri thelathini za Tanzania Bara. Mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali pia ilinunua magari thelathini na tatu ambayo yaligawanywa kwa Halmashauri thelathini na tatu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali Na. 238 la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, katika Mkutano huu mnamo tarehe 18 Julai, 2008, changamoto kubwa inayoikabili Serikali ni ufinyu wa Bajeti. Kwa Bajeti hii iliyopitishwa juzi hakuna kiasi chochote kilichotengwa kwa ajili ya kununulia *ambulance*. Sio rahisi kuzifikia Halmashauri zote kwa wakati mmoja, Serikali itaendelea kununua magari kwa awamu kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. Aidha, nahimiza Halmashauri ziendelee kuweka kipaumbele katika suala hili la magari ya wagonjwa katika mipango ya Bajeti zao. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya vituo vya afya saba vinavyomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, vituo vinne vikiwemo Matai na Mwimbi havina magari ya kusafirisha wagonjwa. Kituo cha Matai kipo kilometa 64 kutoka Makao Makuu ya Wilaya wakati kituo cha Mwimbi kipo kilometa themanini na tisa kutoka Makao Makuu ya Wilaya.

Vituo hivi vimekuwa vikipata huduma ya usafiri kwa kutumia magari yaliyopo Makao Makuu ya Wilaya. Naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga itenge fedha za ununuzi wa gari la kubebea wagonjwa kwa ajili ya kuhudumia vituo vya afya vya Matai na Mwimbi katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ina boti moja inayotumika kwa ajili ya shughuli za usimamizi na usambazaji wa dawa na vifaa kwenye zahanati zilizoko mwambao wa Ziwa Tanganyika ambazo ni Kapare, Samazi na Kipanga. Boti hii ni ya muda mrefu ambayo ilikabidhiwa kwa Halmashauri na Shirika la *AMREF* mwaka 1993. Halmashauri katika mpango wa mwaka 2007/2008, ilinunua injini mpya kwa ajili ya boti hiyo. Halmashauri pia ilikwishafanya tathmini ya kujua gharama ya *housing* ya boti hiyo ambayo itagharimu dola za Kimarekani 8700 na inategemea kuingiza gharama hizi katika Bajeti yake ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutafuta njia mbalimbali za kutatua tatizo la usafiri katika vituo vya afya na zahanati ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau wa maendeleo ili kusaidia uboreshaji wa miundombinu ya usafiri kwa wagonjwa. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Halmashauri ya Sumbawanga hatuna hospitali ya Wilaya na wagonjwa wote katika Wilaya ya Sumbawanga, wanaposhindikana kutibiwa katika vituo vya afya wanapelekwa hospitali ya Mkoa lakini ndiyo vituo vya afya hivi ambavyo havina magari ya kuwahudumia wagonjwa, je, si ni wakati muafaka sasa Serikali kusaidia Halmashauri hii ili iweze kuwa na hospitali yake ya Wilaya ambayo itapunguza umbali wa kuwapeleka wagonjwa katika hospitali ya Mkoa Mjini Sumbawanga?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu vituo hivi vya afya vilikuwa vinajaribu kushirikiana katika kutumia magari ya wagonjwa lakini suala hili limeshindikana, Kituo cha Afya cha Mwimbi kilikuwa kinashirikiana na Lahela na Kituo cha Matai kilikuwa kinashirikiana na Nangorotwa lakini imeshindikana na vijiji vile ambavyo viko kandokando ya Ziwa Tanganyika hiyo boti anayoizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri imechakaa na ni ndogo na Ziwa linapochafuka inakuwa vigumu sana kuingiza ile *fibre boat* ambayo ni ndogo sana katika mazingira ya Ziwa Tanganyika, je, ni lini Wizara itasaidia vijiji vya Kapere, Kipwa, Samazi, Kipanga na Kilewane ili wapate boti ya kuaminika ambayo itawasafirisha wageni katika Ziwa hili la Tanganyika?

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hili la kwanza alilozungumzia la kuwa na hospitali ya Wilaya halina ubishi kabisa kwa sababu sasa hivi tunazungumza habari ya kuleta zahanati katika kila kijiji, hawa wenzetu wana tatizo kwa sababu hawana hospitali ya Wilaya na sera zetu ziko *very clear* zinasema kabisa ni muhimu tukawa na hospitali za Wilaya, Mkoa na Rufaa.

Kwa hiyo, jambo hili halina utata wowote wala halina ubishi wowote, sisi tunachosema ni kwamba katika mipango ya Halmashauri ni vizuri wakaiweka pale na sisi kama Serikali Kuu huku juu tunatakiwa tusaidie, tutasaidia katika mpango mzima wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na Serikali ya Wilaya, hakuna *problem* yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, amezungumzia vijiji hapa ambavyo vinaonekana vina matatizo na kwamba boti hii ina matatizo, ni kweli kabisa. Nimesema boti hii ilipelekwa pale mwaka 1993 na ina hali mbaya. Boti yenyewe kwa maana ya injini imepatikana, kinachogomba hapa sasa ni *housing* ambayo ndiyo hiyo nimejibu hapa kwamba, itakuwa ni

vizuri Halmashauri ya Sumbawanga ikahakikisha kwamba inaingiza katika Bajeti yake. *(Mkaofi)*

Kwa hiyo, hivi tunavyozungumza Bajeti imeshapita hapa na hatuna eneo lolote lile lakini kwa sababu ya *sensitivity* ya jambo tunalolizungumza hapa bado tunafikiri kwamba wenzetu hawa wanaweza kuja tukaangalia kwa pamoja kuona ni eneo gani tunaweza kusaidia lakini hali inabaki hivyo kwa sababu Bajeti ilishapita.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa swali lililoulizwa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila ni la muhimu sana hasa ukizingatia kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi za dunia zilizokubaliana katika kutekeleza *Millennium Development Goals* na kwa kuwa *Millennium Development Goals* zinasisitiza umuhimu wa kupunguza vifo vya akinama wajawazito na watoto wadogo ambavyo vingi vinatokana na kukosa usafiri ambao ni wa kuaminika.

Je, Serikali inaweza ikalichukulia hili katika mpango mzima wa Taifa wa kutekeleza haya majukumu ambayo sisi tumeyakubali na kuhakikisha kwamba tunapunguza vifo vya akinamama wajawazito kwa kutoa hasa kipaumbele katika maeneo ya maji ikiwemo na Wilaya ya Ukerewe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kabisa kwamba ni kweli katika maeneo ya vijijini huduma zetu zina matatizo. Nakumbuka hapa tumejibu sehemu mbalimbali ambao wapo katika maeneo ya mwambao ambao hawana boti kwa ajili ya kusaidia watoto na akinamama wanaofariki. Tatizo hili hatuwezi kukaa hapa na kushindana nalo kwa kusema kwamba si tatizo, ni tatizo ambalo linagusa maisha ya binadamu, lakini mwisho wa kila siku ni kwamba tunazungumzia habari ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, mazingira yanayozungumzwa hapa ni mazingira ambayo wana matatizo ya usafiri wa barabara na wakati huo kuna tatizo la usafiri wa majini lakini jibu linabaki pale pale kwamba Bajeti ndiyo kikwazo kikubwa katika mpango huu. Kwa hiyo, tunasema kwamba kama Halmashauri ya Ukerewe inaona kwamba ni vizuri wakaingiza katika Bajeti yao katika kipindi kinachokuja ili tatizo hilo liweze kutatuliwa. *(Makofi)*

Na. 304

**Mradi wa Maji toka Pongwe - Chuo cha Utafiti wa Kilimo Mlingano**

**MHE. HERBERT J. MTANGI** aliuliza**:-**

Kwa kuwa mwaka 2006 iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia ofisi ya Umwagiliaji ilipata shilingi 212,240,827/= kutoka kwenye Mfuko wa *FACF* za kusaidia miradi ya maji toka mfumo wa maji wa Jiji la Tanga, kituo cha Pongwe kwenda Kituo cha Utafiti wa Kilimo, Mlingano Wilaya ya Muheza:-

(a) Je, ni kwa nini hadi sasa mradi huo haujatekelezwa?

(b) Je, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeshirikisha vipi Halmashauri ya Wilaya ya Muheza katika utekelezaji wa mradi huo?

(c) Je, Serikali haioni kwamba kucheleweshwa kwa utekelezaji wa mradi huo kutachangia kuongezeka gharama zaidi ya fedha zilizotengwa mwaka 2006?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mtangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mwaka 2006 Serikali ya Japan kupitia Mfuko wa *Tanzania – Japan Food Aid Counterpart Fund (TJFACF)* iliidhinisha kiasi cha shilingi milioni 220 kati ya shilingi milioni 260 zilizohitajika kutekeleza mradi wa maji kwa kituo cha Mlingano.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Maji aliridhia kituo kipewe maji ya *TUWASA* kutoka Pongwe mnamo mwaka 2006. Awali Mhandisi Mkuu wa *TUWASA* alikuwa ameandaa makadirio ya shilingi milioni 260 kwa ajili ya utekelezaji mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006, Wizara ilitangaza zabuni ya mradi huu, mara ya kwanza walijitokeza wakandarasi wawili tu ambao wote hawakuweza kukidhi vigezo kulingana na Sheria ya Umma ya Ununuzi. Zabuni ilipotangazwa mara ya pili mwaka 2007, vilevile mkandarasi hakupatikana na waombaji kutotimiza masharti.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kushindikana kwa utaratibu huo, Wizara imeamua kutumia utaratibu wa *single source* kwa kutumia Mhandisi wa Maji wa Mkoa ambaye atanunua vifaa na kusimamia ujenzi. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza wameamua kuchangia mradi huu kwa kugharamia ujenzi wa tanki litakalosambaza maji hayo. Gharama hizo zimo kwenye mipango wao wa mwaka 2008/2009. Hivyo, tuna hakika kwamba mradi huu sasa utatekelezwa na kukamilika katika mwaka 2008/2009. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyotoa yenye matumaini. Hata hivyo tarehe 21 Julai, 2008 wiki moja na nusu iliyopita Mheshimiwa Rais alitembelea Chuo hicho cha Utafiti cha Mlingano na aliwaahidi wananchi wa vijiji jirani vya Ngomeni, Bagamoyo na Mkanyageni kwamba mradi huo utatekelezwa. Je, ni lini hasa kazi ya utekelezaji itaanza licha ya programu ya mwaka 2008/2009 kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu utatokana pia na utayari wa Halmashauri ya Muheza. Fedha hizo zipo na utaratibu wetu umeshaandaliwa Serikalini. Kwa hiyo, Wizara hii kwa kuwa Bajeti za Wizara husika zimeshapita, Halmashauri wakishakuwa tayari mradi huu utatekelezwa haraka iwezekanavyo.

Na. 305

**Upatikanaji wa Vitendea Kazi vya Kilimo**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa michango ya wanawake nchini kwenye sekta mbalimbali ndiyo chachu ya maendeleo na kwa kuwa wanawake wa vijijini ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwarahisishia upatikanaji wa vitendea kazi ili kuboresha shughuli zao za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika kwamba, michango ya wanawake nchini kwenye sekta mbalimbali ndiyo chachu ya maendeleo na kuwa wanawake wa vijijini ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ili kurahishisha shughuli za kilimo na kuongeza uzalishaji tija na mapato ya wakulima wetu wakiwemo wanawake, baadhi ya mambo Serikali inayoyafanya ni haya yafuatayo:-

(i) Kuendeleza matumizi ya wanyamakazi na zana zinazokokotwa na wanyamakazi kama vile plau, kipandio, jembe la palizi na mikokoteni.

(ii) Kuendeleza matumizi ya matrekta yakiwemo ya mkono pamoja na zana zake.

(iii) Kuendelea kutoa mafunzo ya kilimo na zana za mafunzo.

(iv) Kufanya maonyesho ya teknolojia mbalimbali za kilimo cha zana bora na usindikaji.

Mheshimiwa Spika, ili kuwarahisishia wakulima upatikanaji wa vitendea kazi na kuendeleza matumizi ya zana bora, Wizara kwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo imeendelea kutoa mikopo kwa wakulima kwa ajili ya kununua matrekta makubwa na ya mkono na zana zake tangu mwaka 2003/2004. Mikopo hii inatozwa riba nafuu ya asilimia nane na kurejeshwa katika kipindi cha miaka hadi mitano. *(Makofi)*

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na upatikanaji wa mikopo lakini huwa kuna mzunguko mkubwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuwapa kipaumbele wanawake ili waweze kufaidika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kwa nini pembejeo zinachelewa kuwafikia wakulima kwa muda unaotakiwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama anavyokubali yeye mwenyewe kwamba wanawake wengi wanajishughulisha na kilimo na hivyo hivyo hata kwenye mikopo wanaokopa wengi ni wanawake, kwa hiyo, tayari *automatically* wameshapata upendeleo maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tutakuwa tunajitahidi mwaka hadi mwaka kuwahisha pembejeo na kama mnavyofahamu sasa hivi tunabadili mfumo wa kupeleka pembejeo kwa maana ya kutumia vocha na taratibu pia za kuwahisha pembejeo hizo zinaambatana na utaratibu huo. *(Makofi)*

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wanawake hao ndiyo hao wanaojishughulisha zaidi na kilimo, je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuwalimia kwa matrekta na wao kulipa baada ya mavuno ya mazao yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kama Serikali haikodishi matrekta lakini inakopesha matrekta kwa watu binafsi, wafanyabiasha pamoja na vikundi ama Vyama vya Ushirika na wanapokopeshwa wanapewa muda ambao unaitwa *grace period* ya miezi sita ambako kuna uwezekano kabisa wa kuanza kulima na kuvuna na kuuza ili waweze kurudisha mkopo lakini mkopo ule unalipwa kwa miaka mitano. Serikali haiwezi kutoa mkopo mtu alime miaka mitano ndipo arudishe lakini inaweza kutoa *grace period* ya miezi sita kusudi mkulima aweze kujiandaa kulipa baada ya ile miezi sita.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa majibu mazuri ningependa kutoa majibu ya ziada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Nuru Bafadhil, anazungumzia juu ya mikopo na wanawake kulimiwa kitu ambacho ningependa kushauri ni kwamba kwa sababu sasa hivi hatuna chombo cha kutoa mikopo ya namna hiyo, akinamama katika vikundi vyao wanaweza wakaanzisha *SACCOS* na kupitia kwenye zile *SACCOS* kwa mikopo ya matrekta yanayopelekwa vijijini wanaweza kulimiwa, wakakopa kwenye *SACCOS,* halafu wanapovuna wanazilipa *SACCOS*. Huo ndiyo ushauri wetu. *(Makofi)*

Na. 306

**Tatizo Sugu la Maji Nchini**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa maji ni uhai na maeneo mengi nchini yanakabiliwa na tatizo la maji na katika kukabiliana na tatizo hilo Serikali imetangaza mikakati mbalimbali ukiwemo wa kuvipatia maji vijiji kumi kwa kila Wilaya kila mwaka:-

(a) Je, utekelezaji wa mpango huo umefikia wapi kwa nchi nzima hususan kwa Wilaya ya Mbozi?

(b) Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mpango huo haukwami kutokana na kutegemea fedha za wafadhili peke yake?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Maji na Umwagiliaji, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, napenda kuweka sawa na kufanya masahihisho kidogo katika swali na ni baada ya kujadiliana naye kwamba Serikali haikusema imeweka mkakati wa kuvipatia maji vijiji kumi kwa kila mwaka kila Wilaya. Tunachosema ni kuweka mkakati wa kuvipatia maji vijiji kumi kwa kila Wilaya. Maneno yale ya kila mwaka yanaweza yasilete maana ambayo Serikali imeahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la maji nchini, mwaka 2007/2008 programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijijini imekuwa ikitekeleza kupitia aina tatu za miradi kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini;
(ii) Miradi mikubwa ya maji Vijijini (vijiji 10) katika kila Halmashauri; na
(iii) Miradi inayoleta matokeo ya haraka maarufu *quick wins*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu ilitumia shilingi bilioni 16.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya *quick wins* katika Mamlaka ya Miji ya Mikoa minane, Miji ya Wilaya na Miji midogo 36 na kwenye skimu sita kubwa za maji za Maswa, Chalinze, Mugango/Kyabakari, *HTM*, Wanging'ombe na Makonde. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukarabati mfumo wa usambazaji maji, ununuzi wa dira na ufungaji wa mitambo ya kusukuma maji. Mamlaka zote zilitekeleza miradi kufuatia vipaumbele walivyojiwekea wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapa Bungeni tarehe 9 Julai, 2008 katika Kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini, taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia zilichelewesha utekelezaji wa miradi ya vijiji 10 katika Halmashauri. Katika kutatua tatizo hili, Serikali iliiomba Benki ya Dunia kulegeza masharti yake na tarehe 8 Julai, 2008 Benki ya Dunia ilikubali kulegeza masharti yake kwa Halmashauri 82. Hatua inayofuata sasa ni kwa Halmashauri hizo kuzielekeza Kampuni za wataalam washauri ziandae mapendekezo ya usanifu wa miradi ya maji. Halmashauri 33 ambazo hazikutimiza masharti zitarudia zoezi la kutafuta washauri waelekezi na tayari matangazo ya zoezi hili yamekwishatoka katika magazeti. Tunachoomba ni Halmashauri zinazohusika kufuatilia matangazo haya na kuzingatia. Aidha, Halmashauri 17 ikiwemo ya Mbozi zinarudia kufanya upya tathmini ya Kampuni zilizoomba kufanya kazi za ushauri. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inajidhatiti kutumia fedha za ndani pale inapowezekana kulingana na uwezo wake kifedha. Kwa kuwa programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inakadiriwa kutumia dola za Kimarekani 951, ifikapo mwaka 2010, ni dhahiri kwamba tutaendelea kushirikiana na washirika wetu wa maendeleo kwa lengo la kupata fedha zao mapema iwezekanavyo bila kuathiri utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa hali ya maji ya Mji wa Mlowo pamoja na Tunduma kule Mbozi ni mbaya sana na kwa kuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa anapita kujinadi ugombeaji wa Urais mwaka 2005 aliahidi kwamba atahakikisha kwamba miji hiyo miwili inatatuliwa tatizo lake kubwa la maji, je, Waziri sasa anaweza akawahakikishia wananchi wa Miji hiyo miwili kwa maana ya Mlowo na Tunduma kwamba tatizo hilo la maji sasa litapatiwa ufumbuzi?

(b) Kwa kuwa kuna Halmashauri ambazo hazikukidhi vigezo vya Benki ya Dunia kwa maana ya yale masharti Mbozi ikiwa mojawapo, je, nini muda sasa maalum kwamba Halmashauri hizo ambazo zilikosa sifa hizo zitakamilisha zoezi hilo ili wananchi wapate maji

wafaidike sawa sawa na wale wana Halmashauri nyingine 82 ambazo zimepata sifa? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli zipo ahadi za Serikali zilizotolewa na Mheshimiwa Rais kuhusu maji Tunduma na maji Mlowo. Kuhusu maji Tunduma nafurahi kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba Tunduma maji ya kutosha chini ya ardhi yalipatikana katika kipindi cha miezi miwili iliyopita baada ya uchimbaji wa visima.  Tatizo la Tunduma linatokana na umeme. Lakini tutashughulika na wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini kulitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mlowo vile vile kuna ahadi ya kuwapatia maji ya uhakiki Mlowo na Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba katika hotuba yangu nilieleza Bunge lako Tukufu kwamba kuna mradi wa Lukulilo na mradi *Iyula Group*, mradi wa Lukulilo ni mradi ambao hatma yake ni kupeleka maji ya uhakika Mji wa Mlowo. Nafurahi kumweleza Mheshimiwa Mbunge, wiki hii natuma wahandisi waandamizi kutoka Wizarani kwenda kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kuanza kutekeleza ahadi niliyotoa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu hili naliunganisha na lile alilosema Mheshimiwa Herbert Mntangi kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais Muheza baada ya ziara ya Mheshimiwa Rais nimezungumza na Mheshimiwa Herbert Mntangi na namhakikishia kwamba zitatekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni Bajeti ya tatu tangu tumeanza awamu hii ya nne na mimi katika Wilaya yangu ya Same Bajeti ya kwanza tulipewa ahadi ya miradi kumi kwa Wilaya ya Same na mwaka wa pili tulipewa ahadi ya miradi kumi kwa Wilaya ya Same ambayo ndiyo hii ya *quick wins*. Lakini miradi hii tulipewa kimaandishi mimi nina maandishi na haikutekelezwa kama ambavyo tulipewa na Wizara ya maji. Chanzo nilipotafuta nikagundua ni kwamba Serikali inategemea sana fedha za nje katika *quick wins*.

Je, Serikali sasa haioni kwamba kwa sababu miradi hii ambayo ingesaidia sana kutatua tatizo la maji vijijini ni muhimu itumie zaidi fedha za ndani na pia inapotuandikia sisi Waheshimiwa Wabunge ile miradi ihakikishe kwamba miradi ile inatekelezwa kwa sababu na sisi tunarudi kwenda kuwaambia wananchi kwamba kipindi hiki mtapata hiki na kile. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema ikatekeleza yale ambayo inatuandikia sisi Waheshimiwa Wabunge? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu chanzo cha fedha za Serikali kwa ajili ya miradi ya maji, Serikali ina njia mbalimbali za kupata fedha zake mojawapo ni kukopa na hizi ambazo tumekopa Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika ni za uhakika kabisa, kinachochelewesha ni taratibu. Tukikopa si fedha za benki tena ni fedha zetu kwa sababu tutazilipa. Kwa hiyo, ningependa kumhakikishia kwamba tuna matatizo sisi vile vile kwa sababu huwa tunachelewesha mambo fulani fulani lakini wenzetu wa benki wanachelewa vile vile. Tutaendelea kutatua haya matatizo jinsi tunavyoendelea. Lakini kwa sasa kama nilivyotangaza katika Bunge lako Tukufu hii miradi imeanza. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tutajaribu kutoa ahadi pale ambapo miradi inaanza siyo kabla kuanzia sasa ili tatizo kutoa ahadi ambazo hazitekelezeki lisitokee tena. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Job Ndugai kwa swali la nyongeza, lakini nilimuona Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ambaye siku nyingi sana hajauliza swali la nyongeza. Kwa hiyo, yeye ndiyo atakuwa wa mwisho.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu alisema lengo la Serikali la kutoa huduma kwa vijiji kumi kwa kila Wilaya lakini bila kuweka *time frame* na ziko Wilaya zina vijiji 100 Wilaya kama ya Kongwa ina vijiji 70 kwa utaratibu huo wa vijiji kwa muda usioeleweka kuja kufikia vijiji 70 au vijiji 100 sijui itachukua miaka mingapi, je, kwa mwendo huu kweli tutafika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani hili swali ni la Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu kwenye Bunge lako Tukufu nilieleza kwamba vijiji kumi ni wastani katika Wilaya nyingine vinaweza kuwa vijiji 14, katika Wilaya nyingine vinaweza kuwa vijiji 8 inatokana na jiografia na vyanzo vya maji, hilo la kwanza. Lakini la pili vijiji kumi vikiisha basi vijiji kumi vingine vitaanza kwa hiyo, ni changamoto kwa Halmashauri kutekeleza katika kile kipindi ambacho sisi tunatoa fedha. Kwa hiyo, wengine watakwenda haraka zaidi ya wengine. Kwa hiyo, haina maana kwamba hivi vijiji kumi ni mpaka mwisho wa dunia, hapana. Naomba nimhakikishie kwamba iwapo Wilaya ya Kongwa itakamilisha vijiji kumi katika kipindi cha mwaka 2009/2010, mwaka 2010/2011 tutaongeza vijiji kumi vingine kwa hiyo, tutaendelea hivyo hivyo. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali fupi kabisa kutoka Mchinga.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shilingi bilioni 16 na ushehe zilizotajwa na Mheshimiwa Naibu Waziri zilihusisha pia na vijiji vya Milola na Kiwawa kule Jimbo na Mchinga, na kwa kuwa Wizara hiyo iliniandikia barua ambayo kivuli chake nimemkabidhi Mheshimiwa Waziri, je, mwaka huu wa fedha vijiji hivyo vya Milola na Kiwawa ambavyo viliahidiwa mwaka uliopita wa fedha shilingi milioni 148 kwa Milola na milioni 115 kwa Kiwawa vitapatiwa fedha robo ya kwanza, ya pili au ya tatu? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli alinikabidhi hapa barua ambayo aliandikiwa na Wizara yangu miaka takriban miwili iliyopita na nakiri vile vile nakala ya barua hiyo, kuhusu ahadi iliyotolewa na Wizara kwa Jimbo lake. Ni bahati mbaya wakati nadhani hotuba yangu hapa sikumuona, lakini ningemhakikishia kwamba katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Wizara imetenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya vijiji alivyovitaja. *(Makofi)*

Na. 307

**Ucheleweshaji wa Mishahara ya Askari**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali huwaajiri baadhi ya askari polisi wastaafu kwa mikataba mara baada ya kustaafu; na kwa kuwa wanapoajiriwa huwa hawajalipwa kiinua mgongo chao; na kwa kuwa askari hao hutumikia ajira hizo kwa muda mrefu bila kupata mishahara:-

Je, ni lini Serikali itashughulikia tatizo hilo la ucheleweshaji wa mishahara ili kuwapunguzia askari hao ukali wa maisha?

**SPIKA:** Hapo leo mmeshirikiana vizuri sana kwa maswali haya.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali iliwapa mkataba wa kazi wa miaka miwili askari wastaafu wapatao 215. Taratibu zilifanywa ili kuwaweka askari hao wote katika daftari la malipo ya mishahara *(payroll)* mara baada ya kujaza mikataba husika. Hata hivyo, askari 25 mikataba yao ilikuwa na matatizo ya kiutumishi ikiwemo kutokamilika kwa nyaraka za mikataba ambapo askari wengine waliandika taarifa tofuati na zile zilizomo katika kumbukumbu zao za awali kabla ya kustaafu. Kutokana na hilo Serikali ilichukua hatua za kuhakikisha askari hao wanajaza upya mikataba hiyo na wanairejesha kwa hatua zinazofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo hilo la ucheleweshaji wa malipo ya mishahara kwa askari hao 25, Serikali iliamua kuwalipa kiasi cha fedha ili waweze kujikimu wakati taratibu za kuingizwa katika daftari la malipo ya mishahara *(payroll)* zilikiwa zikikamilishwa baada ya dosari zilizokuwemo katika mikataba yao kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia tatizo hili la ucheleweshaji wa malipo ya mishahara, Serikali pia imetoa *payroll print* kwa Jeshi la Polisi ambapo kuanzia Aprili, 2008, askari na watumishi wengine wa Serikali ambao nyaraka zao ni timilifu na zimepata kibali cha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma wataweza kuingizwa kwenye daftari la malipo ya mishahara *(Payroll)* moja kwa moja sambamba na malimbikizo yao ya mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole askari wetu wote ambao wamekumbwa na tatizo hili. Aidha, ni vyema wakaelewa kwamba ucheleweshaji huo umetokana na taratibu za kiutumishi na mkakati mzima wa udhibiti wa matumizi ya fedha na watumishi hewa Serikalini. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hili lilikwishagunduliwa mapema na limechukua muda mrefu kupatiwa ufumbuzi. Mheshimiwa Waziri kwanza ningemuomba atumie nafasi yake kuwaandikia askari hawa ambao wamekumbwa na tatizo hili awepelekee taarifa hii kwa maandishi ili wajue kinachoendelea nia dhamira Serikalini kwa upande wao lakini pia askari hawa ambao tunawapa silaha kwenda kulinda walinzi wetu kwa sababu ya tatizo walilonalo la kimaisha wasije wakazitumia silaha zao vibaya ili kuweza kujikimu katika maisha?

La pili, kwa kuwa tatizo hili limegunduliwa mapema sana, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusiana na watu hao mikataba yao ingesitishwa ili wasiingizwe katika matatizo haya ya kupata matatizo ya kimaisha pamoja na familia zao kwa sababu muda umekuwa ni mrefu sana miaka mitatu siyo mchezo kumgawia mtu fedha kidogo za kuweza kujikimu Mheshimiwa Waziri anasemaje na tatizo hili likajitokeza tena pia? Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli na ndiyo maana nimesema wakati nahitimisha jibu la msingi kwamba tumewataka radhi kwa ucheleweshaji wa shughuli hizi. Lakini ningependa niwe muwazi kwa Mheshimiwa

Mbunge kwamba yalijitokeza mambo mawili haya na yalijitokeza kwa mpigo, kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

La kwanza wakati hawa askari wanaingia katika mkataba 215 polisi ilikuwa inakwenda katika utaratibu wa ku-*computerise system* yote ya malipo na hiyo ilikuwa ni *exercise* nzuri ya kuweza kudhibiti tatizo la kuwalipa watumishi hewa wasiokuwa katika kazi za Serikali. Lakini pili ikaja ikatokana na hiyo kujazwa kwa fomu ambazo hawakuja vizuri.

Lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo tatizo limekwisha na tumefikia hatua za mwisho na nadhani kiasi mwezi mmoja/miezi miwili kuanzia sasa malipo yao yatakuwa ni sawa, pia ikiwemo malimbikizo yao. Kuhusu mikataba hiyo ambayo unaitaja Mheshimiwa Mbunge ambayo itakuja baadaye nafikiri kwa kuwa hili tatizo tumelimaliza na tumeweka utaratibu mzuri wa kujaza zile fomu na sasa kila kitu kinaeleweka nadhani hili tatizo halitatokea tena. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 308

**Shirika la Bima la Taifa**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Bima la Taifa kwenye miaka ya hivi karibuni lilijitangaza kwenda hadi vijijini ambapo lilifanikiwa kuwashawishi na kuwaingiza kwenye Bima za Maisha na Elimu watumishi mbalimbali wakiwemo walimu, wauguzi na madaktari; na kwa kuwa bima zao zinapokuwa zimeiva wanacheleweshewa malipo na hata wanapoomba kusitisha bima hizo hukataliwa au kuzungushwa.

Je, Serikali inafahamu kuwepo kwa tatizo hilo na inatoa tamko gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la kucheleweshwa kulipwa bima zinapoiva na Shirika la Bima la Taifa na inakiri kuwepo kwa madai mengi. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2007, madai ya bima za miasha kwenye Shirika la Bima la Taifa yalikuwa shilingi bilioni 12.04 na zisizo za maisha yalikuwa shilingi bilioni 4.28. Madai haya mengi yalisababishwa na tatizo la uhaba wa fedha unaolikabili Shirika la Bima la Taifa. Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za muda mfupi na wa kati zinazolenga kuondoa tatizo lililopo. Hatua hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kuliruhusu Shirika la Bima kutumia gawio linalotokana na hisa zake kwenye makampuni mbalimbali ili kulipia bima zilizoiva;

(ii) Kutoa kibali kwa Shirika la Bima kuuza hisa zake za mradi wa jengo la *Ubungo Plaza* kule Dar es Salaam; na

(iii) Kutoa kibali kwa Shirika la Bima kuuza baadhi ya mali ambazo hazifungamani na biashara ya Bima.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi hizo, hadi kufikia Juni, 2008 Shirika la Bima limefanikiwa kulipa shilingi bilioni 3.84 kwa madai ya Bima ya Maisha na shilingi bilioni 2.16 kwa Bima zisizo za maisha. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 1.90 zimekwishatumwa Wilayani kwa lengo la kulipia madai mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hatua za muda mrefu ambazo zinalenga kutatua matatizo yanayolikabili Shirika la Bima la Taifa ni pamoja na kulifanyia marekebisho ili lifanye kazi zake za huduma ya bima kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika**,** kwanza kabisa napenda Serikali ifahamu kwamba wapo watu ambao watoto wao wameshindwa kwenda shule kwa sababu ya bima hizo. Kwa sababu wakati wakifanya matangazo na kuwapitia kuwashawishi hawakuwapa elimu ya kutosha. Sasa inapofika mahali ambapo Shirika linashindwa kumlipa mtu wakati bima yake imeiva na akiwa ameiweka ile bima kwa malengo fulani, mimi nadhani hii ni hatari. Lakini pia si vizuri kwa sababu Serikali itambue kwamba suala la bima ni suala la kimaendeleo, na kwa hiyo, Serikali inasema nini katika hali ya sasa ambapo wanaodai wanazidi kuathirika na ni mpaka lini bima zisizokuwa za maisha wataweza kulipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ambalo ningependa Serikali inijibu ni kwamba je, katika bima hizi nyingine zote kwa tofauti ya kiasi hicho wanacholipa na ukiangalia uwezo halisi wa Shirika la Bima la Taifa. Serikali inalisaidiaje Shirika hili la Bima maana yake sasa limebeba fedha za watu na haliwalipi na Serikali inataka kusema nini juu ya hatma sasa ya Shirika lenyewe na uwezo wake katika kuwahudumia wateja wake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** (**MHE. JEREMIAH S. SUMARI**): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, lini zitamalizika kulipwa bima ambazo zimeiva.

Mheshimiwa Spika, matarajio yetu ni kwamba kufikia mwisho wa mwaka huu mwezi Desemba, 2008 nyingi ya bima hizo zitakuwa zimekwishalipwa. Lakini nitahadharishe hapa pale Serikali inafanya hivyo, na hata baada ya kufanya hivyo mara nyingine huwa yanajitokeza mambo mengine ambayo yanahusishwa na malipo ambayo yalifanywa na Serikali hapo awali. Lakini kwa *time frame* tunategemea kwamba kufikia mwisho wa mwaka huu tatizo hili kwenye Shirika la Bima litakuwa limekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba siyo kusudi la Serikali kutatiza mwananchi yeyote ambaye anakata bima yake ama ya maisha au ya vyombo ambavyo vinahitajika kukatiwa bima. Lakini mara nyingine mimi ninafikiri na kwa kweli ni vizuri tukaanza vile vile kulinda heshima ya Serikali kwamba vyombo hivi ingawa vinaitwa ni vya Serikali, lakini vina Bodi zake zina menejimenti yake, na kwa vyombo vingi hivi Serikali inaacha macho pale, lakini inaondoa mikono yake kwenye uendeshaji na hivyo ni kutokana na utawala bora wa kuendesha Mashirika hayo. Ni pale panapotokea matatizo ndipo Serikali inapoingilia na kuanza kutafuta jinsi ya kuwanusuru wale wananchi ambao watakuwa wameumia katika ile huduma ambayo inatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika hili Serikali itashirikiana na Shirika la Bima na tayari imekwishaagiza Shirika la Bima kwamba waombe uuzaji wa mali ambazo hazihusiani na bima ili zipatikane fedha kwa ajili ya kulimaliza tatizo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali fupi la mwisho Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha za Shirika la Bima la Taifa ni fedha zilizotolewa na walioweka bima zao; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali inaondoa mikono lakini inaweka macho yake; na kwa kuwa hasara hii au hali hii imejulikana kwa muda mrefu na watu hao wamekosa fedha zao kwa muda mrefu. Serikali ambayo ina macho yake lakini haikuwa imeweka mikono katika kusimamia, je, Serikali inachukua hatua gani kwa wale ambao kwa uzembe wao wamefanya wananchi wapoteze fedha zao na kuingia katika hasara kubwa kwa kiasi cha kushindwa kusomesha watoto wao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** (**MHE. JEREMIAH S. SUMARI**): Mheshimiwa Spika, hatua zitakazochukuliwa zinategemeana sana na kile kitachobainika kwamba kimetendwa ama kimefanyika na yule mhusika. Lakini katika Shirika la Bima la Taifa sasa hivi tupo katika mchakato wa kulirekebisha na katika kulirekebisha kule ni pamoja na kutazama mizania yake, ni pamoja na kutazama Taarifa ya Mapato na Matumizi, ni pamoja na kutazama wanaodai lile Shirika la Bima, lakini pamoja na vile vile kutazama picha kubwa ya Sekta ya Fedha na Sekta ya Bima. Katika kufanya hivyo, tunaamini kwamba tutakapokuwa katika mchakato huo wa kulirekebisha basi huko kama tutabaini kwamba kuna watu ambao kweli wametufikisha mahali pabaya basi hatua ambazo wanastahili kuchukuliwa, watachukuliwa. *(Makofi)*

Na. 309

**Kupanda kwa Bei ya Mafuta**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya mafuta ya dizeli na petroli imepanda ghafla kati ya tarehe 15 na tarehe 30 Aprili, 2008 na bado inaendelea kupanda:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha hali hiyo?

(b) Je, ni nini athari zinazotokana na hali hiyo?

(c ) Je, ni athari gani zinazotokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hizo zinazomgusa mwananchi wa kawaida hususan wale wa vijijini na Serikali inachukua hatua gani kubadili hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** (**MHE. JEREMIAH S. SUMARI**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Jimbo la Nyangh’wale, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ongezeko la bei ya mafuta hapa nchini limesababishwa na ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia. Hali hii imetokana na kuongezeka mahitaji ya mafuta duniani ukilinganisha na uzalishaji wake, lakini pia na soko lenyewe la mafuta.

(b) Mheshimiwa Spika, kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kunaziathiri sana nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Athari hizo ni pamoja na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma kunakosababishwa na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji, kuongezeka kwa nakisi ya biashara *(trade deficit)*, pamoja na kupungua kwa nafasi za ajira. Kuendelea kwa hali hii kunakwamisha pia juhudi za Serikali na wananchi katika kujiletea maendeleo ya haraka ambayo yanalenga katika kuboresha hali zao za maisha.

(c) Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa mfumuko wa bei nchini kunasababisha pia kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi walio wengi hususan walio vijijini kwani hali hii inaathiri Bajeti ya kaya kwa kupunguza uwezo wa kaya katika kujipatia mahitaji yake muhimu kama vile chakula. Kutokana na hali hiyo, familia zilizo maskini ambazo ndiyo nyingi zinashindwa kununua chakula cha kutosha na hivyo kuathiri afya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na hali hiyo ni kama zifuatazo:-

(i) Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria mpya ya Petroli mwezi Aprili, 2008. Sheria ambayo inaruhusu uagizaji wa mafuta kwa jumla *(bulk procurement)*, ambao unatarajiwa kupunguza gharama za mafuta yanayoingizwa kutoka nje ya nchi.

(ii) Serikali ikishirikiana na makampuni mbalimbali inaendelea na juhudi za kutafuta vyanzo vya mafuta hapa nchini.

(iii) Serikali inaendelea kuboresha miundombinu kama vile barabara na bandari ili kurahisisha usambazaji wa bidhaa yakiwemo mafuta, kwa lengo la kupunguza gharama za usafirishaji ambazo zinachangia kuwepo kwa mfumuko wa bei.

(iv) Kuandaa utaratibu wa kutumia gesi viwandani, majumbani pamoja na vyombo vya usafiri kama nishati mbadala.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu marefu na mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kupanda kwa bei ya petroli kumekwenda sambamba na kupanda bei ya chakula duniani; na kwa kuwa kwa sasa hivi chakula nacho ni petroli nyingine ya dunia, lakini pia kwa kuwa Tanzania ina ardhi nzuri na hali ya hewa inayofaa kwa kilimo, je, Serikali katika mwaka ujao wa fedha itakuwa tayari kuwawezesha kwa kuwapa mikopo wakulima moja kwa moja kwa mazao kwa mazao ya chakula na biashara kama vile ya mahindi, mpunga, pamba, korosho ili wazalishe zaidi ili waweze kuuza kwa wingi hii petroli mpya duniani?

Lakini suala la pili, kwa kuwa bei ya mafuta inapanda zaidi kadri unavyokwenda mbali na Dar es Salaam hususan katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, je, Serikali itatoa taarifa gani leo kuhusu ule mradi wa kupeleka bomba la mafuta ya petroli kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu mikopo kwa wakulima, hili limeshazungumziwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mawaziri na Serikali imeshatoa matamko mengi na kuna Mfuko wa Pembejeo kwa hiyo kutokana na hayo ambayo yameshasemwa kwa kweli kuongezea zaidi ni kurudia ambayo tayari tunayafahamu na mambo ambayo tayari Serikali imeshayafafanua.

Swali la pili, kuhusu bomba la mafuta, nikiri hapa sina taarifa kuhusu hili limefikia wapi tunajua lilikuwa na mzozo na jambo hili lilifikishwa Mahakamani kwa hiyo nikiri siwezi kulisemea hapa leo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea kuzingatia muda. Muda wa maswali sasa umekwisha, lakini maswali haya mawili nadhani tuyamaliza kwa sababu nilichukua muda kutoa matangazo mengine. Zamu ya Wizara ya Miundombinu swali linaulizwa na Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama.

Na. 310

**Kupandisha Hadhi Barabara – Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara za Kahama – Ulowa kupitia Kata za Nyandekwa, Ukune, Kisuke, Uyogo na Ushetu kilometa 100 na Kahama – Bulungwa kupitia Nyandekwa na Mpunze kilometa 50 kwenye Jimbo la Kahama ni muhimu kiuchumi siyo tu kwa Wilaya ya Kahama bali kwa Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Mikoa jirani kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara kama vile, pamba, tumbaku, mahindi, mihogo, mpunga na mazao ya misitu kama vile mbao, nta na asali lakini licha ya umuhimu wake barabara hizo ziko kwenye hali mbaya sana:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazoifanya Serikali kupata kigugumizi cha kuzipandisha hadhi barabara hizo kuwa za Mkoa hata baada ya vikao vya juu vya Mkoa kuridhia kupandishwa hadhi barabara hizo?

(b) Je, ni lini tatizo la madaraja ya Mto Kalole kwenye barabara ya Kahama – Bulungwa – Kwimba kwenye barabara ya Kahama – Ulowa yatatengenezwa kwa kiwango kinachostahili ili kuondoa kero ya kuharibika kutokana na mafuriko kila msimu wa mvua unapowadia?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vigezo vya kupandisha au kushusha daraja barabara mbalimbali vitaainishwa katika Kanuni za Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007. Hivi sasa Wizara inaandaa Kanuni za Sheria hiyo *(regulations)* ili taratibu za kupandishwa na kuteremshwa daraja barabara yoyote ziweze kuwa wazi zaidi. Kazi hii inaendelea kufanyika kwa umakini nchi nzima kufuatana na sheria inavyoagiza ambapo inatarajiwa kukamilishwa ifikapo mwezi Septemba, 2008. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, barabara za Kahama – Ulowa na Kahama – Bulungwa bado zinabakia kuwa ni za Halmashauri ya Wilaya ya Kahama hadi hapo tutakapokamilisha Kanuni za Sheria na kubainishwa zitakuwa kwenye ngazi gani. Kwa msingi huo ninamshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama kuona jinsi ya kupata fedha za kutosha ili kujenga madaraja katika Mto Kalole. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa zoezi la kuandaa kanuni hizi limechukua muda mrefu na haliendi sambamba na uzalishaji unavyoendelea katika maeneo mbalimbali ya nchi na sasa tunaambiwa litakamilika mwezi Septemba mwaka huu. Je, Waziri anaweza kulieleza Bunge hili na umma wa Watanzania baada ya Septemba, 2008 lini zoezi la kujadili kanuni hizo litakamilika na litachukua muda gani?

Pili, kwa kuwa barabara hizi mbili nilizozitaja za Kahama - Ulowa, Kahama – Bulungwa ni uti wa mgongo kwa uchumi sio tu wa Wilaya ya Kahama bali wa nchi nzima; na kwa kuwa Serikali inatambua hivyo, je, Waziri ana kauli gani ya kuwaambia wananchi wa maeneo haya kauli ya kuwapa moyo wa kuendelea kuzalisha zaidi wakati wananchi wakisubiri kukamilika kwa taratibu alizozitaja? Ahsante.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu ukamilishaji wa zoezi wa uandaaji wa kanuni. Hili tumelitilia mkazo sana tumelishikia bango Serikalini na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kazi hii kwa kila namna tutajihidi ikamilike mwezi Septemba, 2008. Tayari sasa hivi Kampuni ya *KMMN Advocates* ya Dar es Salaam iko kazini kushughulikia upitiaji wa sheria hii na uandaaji wa kanuni kwa maana hiyo ni kwamba tutasimamia hiyo kazi kikamilifu ili tuhakikishe kwamba imekamilika kwa muda ule ambao tumeutaja na pia kujadili kanuni hizi. *(Makofi)*

Swali la pili, niwahakikishie wananchi wa Wilaya ya Kahama katika maeneo haya yenye umuhimu mkubwa wa kiilimo kwamba Serikali inafahamu umuhimu wa miundombinu ya barabara na itafanya kila linalowezekana kuona kwamba hawakatishwi moyo kuendelea na kazi hizi muhimu za kujenga uchumi. *(Makofi)*

Na. 311

**Vyumba vya Ibada Katika Uwanja wa Ndege**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye viwanja vingi vya Ndege vya Kimataifa duniani kuna vyumba maalum vya ibada kwa wasafiri waendao masafa marefu:-

(a) Je, viwanja vyetu vya Ndege vya Kimataifa vina vyumba kama hivyo?

(b) Kama havipo, kuna mipango gani ya kuanzisha sehemu kama hizo kwenye viwanja vyetu?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baadhi ya Viwanja vya Ndege vya Kimataifa Duniani vina vyumba maalum vya ibada kwa wasafiri waendao masafa marefu. Hata hivyo katika Viwanja vyetu vya Kimataifa vya Julius Nyerere, Kilimanjaro na Zanzibar, hakuna vyumba maalum kwa ajili ya ibada. Kukosekana kwa vyumba kama hivyo kunatokana na ukweli kwamba viwanja vyetu vya ndege vya Kimataifa si viunganishi *(international hub)* vya kuweza kuwa na abiria wengi wanaosubiri ndege za kuunganisha *(transit passengers)* kwa muda mrefu. Kwa sababu hiyo wazo la kuweka vyumba vya ibada ndani ya majengo ya abiria halikufikiriwa huko nyuma. Kinachofanyika kwa sasa ni kwamba pale ambapo abiria anataka kufanya ibada, mamlaka zinazoendesha viwanja hivyo humwelekeza mhusika kwenye sehemu za wazi ndani ya jengo la abiria na hivyo kupata fursa ya kufanya ibada. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, hitaji la vyumba vya ibada litazingatiwa. Hitaji hilo limezingatiwa kwa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe kinachojengwa hivi sasa Mkoani Mbeya na pia tutazingatia wakati wa kusanifu jengo la tatu la abiria *(Terminal Building III)* katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNIA). (Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimefarijika kusikia kwamba katika usanifu wa *Terminal Building* namba III ya Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Julius Nyerere kutafikiriwa kuwekwa sehemu kama hizo za ibada. Lakini hivi sasa ingawa viwanja vya ndege vyetu sio *international hubs* lakini kuna wasafiri ambao wanakaa muda mrefu kungoja safari za Kimataifa na wanahitaji kuwa na sehemu hizo za ibada. Kwa nini basi katika Kiwanja chetu cha Ndege cha Mwalimu Julius Nyerere *building* namba II na kile cha Zanzibar na Kilimanjaro hivi sasa kisiweke vyumba kama hivyo kwa ajili ya ibada, hilo suala la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili, katika kila sehemu za Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa kote pale ulimwenguni panakuwa na mabango au *labels* kuwaonesha wasafiri kwamba sehemu hizo zinatumika kwa ajili gani? Je, kwa nini pawe na umuhimu wa msafiri ambaye anataka kufanya ibada aende akatafute wakala au mamlaka inayoendesha Kiwanja cha Ndege kujua sehemu za ibada pasiwe na *labels* kuonyesha kwamba sehemu fulani unakwenda kufanya ibada yako? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu kuweka vyumba vya dharura vya Kiwanja chetu cha Ndege cha Mwalimu Julius Nyerere na kule Zanzibar, hakika Kiwanja cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kilijengwa mwaka 1984 na mpaka hivi sasa hali pale ni ngumu sana kuna upungufu wa vyumba vingi kwa ajili ya taratibu au kazi mbalimbali. Msongamano umekuwa mkubwa na hiyo ndio sababu imeletea kwamba tuunganishe nguvu na sekta binafsi ili moja, kupanua jengo hilo namba mbili kujenga *terminal building III.* Kwa sasa haitokuwa rahisi sana kufanya hivyo, lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaangalia kila linalowezekana kwa njia za dharura kufanya kile kitakachowezekana, itakaposhindikana niliombe Bunge lako Tukufu tuvute subira mpaka pale ambapo tutakuwa tumekamilisha kazi hii. *(Makofi)*

Kuhusu kuonyesha sehemu zilizohusika kwa vile hatunayo hivi sasa imekuwa tatizo kuonyesha sehemu inayohusika kwa sababu vyumba havipo. Lakini kama alivyosema katika swali lake la kwanza tutaangalia kila kinachowezekana katika kipindi hiki kifupi kabla maboresho ambayo tunategemea kuyafanya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Matangazo na nitaanza na wageni.

Wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Kego Masha ni kama ifuatavyo, wa kwanza ni bibi Stella Lawrence Kego Masha ambaye ni mkewe Mheshimiwa Waziri. Yule pale juu *speaker's gallery,* ahsante sana karibu sana mama, karibu sana. Pia, kuna Lawrence mdogo, Lawrence Kego Masha *Junior* mwanawe. Aah, karibu sana, sijui na wewe utafuata nyayo hizo hizo. Halafu yupo ndugu Yacoub Elhilo, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Wakimbizi *(UNHCR). You are warmly welcome to the House please.*

Sasa Wizara hii kubwa sana sijui wageni wataalam na Watendaji Wakuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo, Bwana Mohamed Said Muya ni Katibu Mkuu wa Wizara, yule pale. Ahsante sana. Tunaye *IGP* Ndugu Saidi Mwema, ahsante sana. Bwana Robert Manumba Mkurugenzi wa Upelelezi, Bwana Clodwig Mtweve, Kamishna wa Utawala na Fedha katika Jeshi la Polisi, ahsante sana na Bwana Paul Aman Chagonja, Kamishna wa Mafunzo na Operesheni. Tena hawa nimeandikiwa ovyo ovyo wana mavyeo yao huwezi kusema Bwana, lakini basi bahati mbaya. *(Makofi)*

Wengine ni Bwana Khamis M. Simba, Kamishna wa Polisi Zanzibar, ahsante sana, halafu Bibi Victoria Fovo, Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Bibi Angela Nyoni, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Bwana G. R. Mbunda, Mkurugenzi hoo, huyu naye wa Sera na Mipango nadhani wako wawili sijui, Bwana Oneil Malisa, Mratibu wa Huduma kwa Jamii, Bibi Judith Mtawali, Mkurugenzi Idara ya Wakimbizi yule pale, Bwana Augustine D. Shio, Mkurugenzi Idara ya Kushughulikia malalamiko. Duh!!! Hii Wizara ina mambo mazuri kweli, kuna Mkurugenzi wa Kushughulikia Malalamiko. *(Makofi)*

Bwana Dickson Maimu, Mtendaji Mkuu wa Vitambulisho vya Taifa, aaha hayupo, Bwana Florian W. P. Mushy, Mwanasheria Mkuu wa Wizara, yule pale, Bwana Simon Mjelu Mwenyekiti wa *TUGHE* Wizarani, yule pale pamoja na Msaidizi wake Makamu Mwenyekiti ambaye anaitwa Bwana Arcado Nchinga, yule pale. Halafu Bwana Yona S. Mwakilembe, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Kushughulikia Malalamiko ahsante sana, Bwana Johnson P. Brahim, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Wakimbizi, yule pale, Bwana Peter P. Mosha, Naibu Kamishna wa Polisi na Mkuu wa Kitengo cha Mipango na Utafiti Makao Makuu ya Polisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine ni Bwana Peter Kivuyo, Naibu Kamishna wa Polisi kutoka Idara ya Upelelezi, naona hawa wapelelezi wamejificha mahali hawa, Bwana Omar Mganga, Naibu Kamishna wa Polisi na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Ahsante sana Kamanda Mganga, ahsante sana umekuwa ni msaada mkubwa sana katika siku tatu hizi tulizokuwa na matatizo hapa Bungeni. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Yupo Bi Zuhura Munisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Kitengo cha Maendeleo na *Logistics,* Bwana Augustino N. Nanyaro, Kamishna Mkuu wa Magereza, yule pale karibu sana Kamishna, Bwana Elias M. Nkuku, Kamishna wa Utawala na Fedha upande huo huo wa Magereza, Bwana M. Manyara Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma, Bibi Anna Katule, Mhasibu Mkuu Jeshi la Magereza, Bwana Nimrod Mahozi, Mkaguzi Mkuu wa Ndani katika Jeshi la Magereza, yule pale na Bwana Matwani Mohamed Kapamba, Kaimu Kamishna wa Jeshi la Zimamoto, yule pale, loo, karatasi hii imekuwa ndefu. *(Makofi)*

Bwana Michael Shija, Kaimu Kamishna wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Utawala na Fedha, yule pale, Bwana Rogatius Kipali, Naibu Kamishna wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Usimamizi na Uratibu wa Vikosi, yule pale, Bwana Ali Liangwike, Naibu Kamishna wa Jeshi la Zimamoto la Uokoaji Sera na Utafiti, yule pale, Bwana Kinemo W. D. Kihomano, Mkurugenzi wa Uhamiaji, yule pale, Bwana Minchoum H. Salum, Mkurugenzi Msaidizi wa Uhamiaji Zanzibar, yule pale karibu sana, Bwana Peniel Mgonja, Mkurugenzi Msaidizi wa Uhamiaji, Utawala na Fedha, Bibi Mary Mwankanye, Afisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma, ahsante sana, Bwana Damian Mbwilo, Mhasibu Mkuu Idara ya Uhamiaji na mwisho kabisa Bwana Tukumbwike Mwakatundu, eeh huyu wa Kyela sijui, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Idara ya Magereza upande wa kulia pale, ahsante sana. Samahani wageni walikuwa wengi lakini ndio upana wa Wizara hii. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam ni viongozi wa chama kinachoshughulikia maslahi ya Maalbino Bwana Oscar Daman Haule, Mwenyekiti, yule pale na Bwana Aman Elisha Mkumbo, Katibu. Ahsanteni sana kwa kujitoa ili tuweze kuhudumia ndugu zetu hawa ambao wana matatizo hayo maalum. Mgeni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji, Bwana Stanley Matende ambaye ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Mitundu, Mgandu. *(Makofi)*

Wapo sasa sijui wapo humu humu ndani au wako kule *basement* wanafunzi na walimu 70 kutoka Shule ya Sekondari inaitwa *Lake, Lake Secondary School*, nadhani labda wako kwenye ukumbi mwingine ule. Wapo pia wanafunzi na walimu 40 kutoka Shule ya Msingi Kikuyu “B” Dodoma. Naomba wasimame kama wapo, wale pale. Karibuni sana walimu na vijana wetu tunawatakia mema katika masomo. Ahsante sana. Wapo walimu na wanafunzi 30 kutoka *Mkonze Secondary School* hapa Dodoma. Ahsante sana karibu sana nanyi pia tunawatakia mafanikio katika masomo. *(Makofi)*

Matangazo ya vikao, Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali ameniomba nitangaze kwamba leo kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo saa 7.00 mchana katika ukumbi namba 231. *PAC*, Kamati ya Hesabu za Serikali saa 7.00 mchana ukumbi namba 231.

Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu anaomba Wabunge wote wa Kamati hiyo wakutane katika ukumbi Na. 432 saa 7.00 mchana, kwa hiyo, Kamati ya Miundombinu saa 7.00 mchana ukumbi namba 431.

Mheshimiwa John Cheyo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati Ndogo inayoshughulikia Miswada ya Bunge ameomba kwamba Wajumbe wote wa Kamati Ndogo ya Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge wanaoshughulikia masuala ya Miswada ile muhimu wakutane saa 5.30 asubuhi katika ukumbi wa Spika, saa 5.30 asubuhi Kamati Ndogo inayoshughulikia Miswada. Huo ndio mwisho wa matangazo. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Kanuni ipi?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR**: Ukurasa wa 11, kifungu 15 (2).

**SPIKA**: Endelea.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu kifungu hicho kinasema kwamba; "Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni atateua Wabunge wa Chama chake au Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambao watakuwa Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara zilizopo Serikalini."

Mheshimiwa Spika, naomba nipate mwongozo wako wakati ulipokuwa ukimwita Mheshimiwa Shoka, ulimwita Mheshimiwa Shoka kama Waziri Kivuli na hili limekuwa likifanyika. Naomba Mwongozo wako hivi kifungu gani humu ndani kinatamka kwamba tutakuwa na Waziri Kivuli katika Bunge, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir si mambo yote yamo tu katika kanuni. Ni utaratibu wa Mabunge yote ya *Commonwealth* kwamba wale wanaokaa Kambi ya Upinzani wanatambuliwa kama vile nayo ni Serikali tarajiwa. Ukiwa mkereketwa sana litakuudhi lakini ndio ukweli huo kwamba kuna pande mbili kwa hiyo, katika nchi zote ukienda Uingereza, Australia na Canada wale Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani wanajulikana kwa jina la Kiingereza *Shadow Ministers,* Kiswahili tunawaita Mawaziri Kivuli, kwa hiyo, Bunge la Jamhuri ya Muungano limetumia utaratibu. Tunaongozwa na Katiba, Sheria, Kanuni na taratibu na tamaduni za Kimabunge katika nchi ambazo tunafanana nazo Kidemokrasia. Kwa hiyo, tumetumia utamaduni huo, ahsante sana. *(Makofi)*

## MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

### Maelezo Binafsi ya Mbunge Kuhusu Ujenzi wa Chuo Kikuu Dodoma

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maelezo binafsi. Lakini kabla ya kufanya hivyo naomba kwanza kabisa niungane nawe na Waheshimiwa Wabunge wote kutoa salaam zangu nyingi za rambirambi kwanza mimi binafsi na familia yangu, wananchi wote wa Jimbo la Bahi na wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwa ujumla kwa familia, ndugu na marafiki wa Marehemu Chacha Zakayo Wangwe, kwa msiba huu mkubwa uliowafika. Tuko pamoja nao katika msiba huu mzito na tunamwomba Mwenyezi Mungu awafariji na vile vile amuweke Marehemu Chacha Zakayo Wangwe, mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya rambirambi hizo basi naomba kwa kutumia kifungu cha 50(1) za Kanuni za Bunge nitoe maelezo binafsi yanayohusu shukrani kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania na Serikali ya awamu ya nne kwa uamuzi wa kujenga Chuo Kikuu hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma, sisi Wabunge wa Mkoa Dodoma tunatoa shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wetu na Serikali yake ya awamu ya nne kwa uamuzi wa busara na hekima wa kujenga Chuo Kikuu kikubwa kuliko vingine vyote hapa nchini katika mkoa wetu wa Dodoma. Chuo hiki kinachoitwa *The University of Dodoma* ambacho kinatarajiwa kuwa na wanachuo 40,000 ni uwekezaji mkubwa sana ambao Serikali imeamua kuufanya katika mkoa wetu. Hii ni fahari kwetu sisi wa Mkoa wa Dodoma na kwa kweli kwa Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chuo hiki kinatarajiwa kuwa na vyuo ndani yake kama ifuatavyo, *College of Social Science and Humanities, College of Information and Ventral Education, College of Education, College of Health Sciences and College of Natural Sciences and Mathematics.*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wa Mkoa wa Dodoma tunafahamu kuwa kiini cha wazo hili ni tamko la yeye mwenyewe Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliyetoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa mwaka 2005. Aidha, sera madhubuti za Chama cha Mapinduzi na Serikali yake pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 juu ya kusudio la kuongeza udahili wa wanafunzi katika Vyuo Vikuu hapa nchini. Tunaamini kwamba Chuo Kikuu hiki cha Dodoma ndiyo jibu sahihi la tatizo la upungufu wa wataalamu hapa nchini na hasa upungufu wa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chuo hiki kimeshaanza toka mwaka 2007 kwa kudahili wanafunzi 1200 na kwa taarifa tulizonazo kwa mwaka 2008/2009 kinatarajia kudahili wanafunzi wasiopungua 5,000 katika fani mbalimbali. Ama kwa hakika kazi hii ya utekelezaji ni kubwa sana na ya ajabu na kwa kweli ni kinyume kabisa ya matarajio ya wengi kuwa isingewezekana chuo hiki kuanza kwa ufanisi kama huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kasi hii ya uanzishwaji na maendeleo ya ujenzi unaofanyika, tutakuwa wachoyo sana wa fadhila endapo hatutawapongeza na kuwashukuru Mkuu wa Chuo Msaidizi Profesa Idriss Kikula na wasaidizi wake Profesa Ludovick Kinabo na Profesa Shaban Mlacha kwa kazi nzuri na ngumu wanayoifanya usiku na mchana katika kuhakikisha kuwa chuo kinaendelea na hakuna jambo linaloshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania hawa wanafanya kazi nzuri sana na kwa kweli historia haitausahau mchango wao kwa Taifa letu. Kwa hiyo tunapendekeza kuwa Serikali ifikirie kuwatunuku Maprofesa hawa Nishani ya Utumishi uliotukuka kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaendelea kuifanya hadi sasa. Aidha, tunawapongeza watumishi wote wa chuo hiki kwa maana wamekubali kufanya kazi katika mazingira magumu ya mpito na hivyo uvumilivu wao ni muhimu sana katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yanayoanza kuonekana katika ujenzi wa chuo hiki yasingewezekana kama mifuko yetu ya hifadhi ya jamii isingekubali kujitosa na kuwezesha kuanza kwa shughuli za ujenzi wa chuo unaoonekana hivi sasa. Kwa hiyo, kipekee kabisa tunaipongeza mifuko hii kwa kukubali kutoa mkopo kwa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa chuo hiki. Mifuko hiyo ni kama ifuatavyo; *National Social Security Fund (NSSF), Public Service Pension Fund, Local Authority Provident Fund na Parastatal Pension Fund*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiuchumi chuo hiki kimeshaanza kuleta mabadiliko makubwa hasa katika mzunguko wa fedha hapa mkoani kwetu kwani soko la vyakula sasa limechangamka na biashara kwa ujumla imeongezeka kiasi kwamba maendeleo ya Dodoma yameanza kushika kasi mpya ambayo haikutarajiwa katika hatua hii ya awali na bado chuo hiki hakijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pindi ujenzi huu mkubwa na wa kasi ya ajabu unaoendelea kule Chimwaga utakapokamilika na idadi ya wanachuo kufikia idadi hiyo ya 40,000 na jumuiya nzima ya chuo hiki kufikia zaidi ya laki moja wote wakawepo Dodoma basi mji huu utakuwa tofauti na unavyoonekana hivi leo. Tunatoa pongezi nyingi sana kwa Serikali yetu. Aidha, tunapenda kutumia fursa hii kuwaomba wananchi wote wa ndani na nje ya nchi waje wawekeze rasilimali zao hapa Dodoma kwani hivi sasa Dodoma kumekucha. Karibuni sana nyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu na faida za ujenzi wa chuo hiki hapa Mkoani kwetu sisi Wabunge wa Mkoa wa Dodoma tunatoa wito maalum kwa wananchi wa vijiji vinavyokizunguka chuo hiki vya Ng’ong’ona, Mhande, Chitogolo na vinginevyo wito

huo ni kwamba kwa kuwa Serikali imekwishawalipa fidia kwa kutwaliwa ardhi yao kwa mujibu wa Sheria basi wale baadhi yao wanaoleta vikwazo na pingamizi visivyo na maana waache vitendo hivyo mara moja kwani chuo hiki kina manufaa makubwa kimaendeleo kwao wenyewe na kwa watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila jambo zuri lolote halikosi changamoto. Kutokana na kuwepo kwa chuo hiki hapa Dodoma kitakachoongeza idadi ya watu hapa Dodoma kuna haja ya Serikali kuyaangalia mambo yafuatayo:-

(i) Kujenga uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Msalato mapema iwezekanavyo.

(ii) Kuendeleza vyanzo vingine vipya vya maji zaidi ya kilichopo cha Mzakwe kwa kuwezesha ujenzi wa bwawa kubwa la maji katika mto Bubu.

(iii) Kuipatia fedha ya kutosha katika Bajeti Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu yaani *CDA* ili iweze kutimiza majukumu yake hasa la kupima viwanja kwa ajili ya ujenzi wa makazi na huduma za jamii na barabara katika eneo lote lililoainishwa kwenye mpango kabambe wa *CDA.*

(iv) Kuanza ujenzi wa barabara ya Iringa, Dodoma hadi Babati kwa kiwango cha lami haraka iwezekanavyo ili kurahisisha usafiri.

(v) Bajeti ya Chuo Kikuu cha Dodoma ya mwaka huu ina mapungufu ya shilingi bilioni 23.6 tunaiomba sana Serikali iangalie kipekee suala hili muhimu ili ifikapo Septemba, 2008 Chuo kiweze kudahili wanafunzi 5000 kama ilivyopanga.

Mheshimiwa Spika, tunaomba turudie tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais yeye mwenyewe binafsi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sio tu kwa uamuzi huu wa kujenga na kuendeleza Chuo Kikuu cha Dodoma lakini pia kwa kutekeleza kwa kasi ya ajabu ujenzi wa Chuo hiki. Historia ya Mkoa huu na Taifa letu haitamsahau Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana kwa kutupatia nafasi hii na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma. Huu pia ni mfano mzuri sana na mambo mazuri tunapoyapata katika maeneo yetu tuige mfano wa wenzetu wa Dodoma ambao wanatoa maelezo kuishukuru Serikali. Isiwe muda wote ni kulaumu, kuhoji, basi iwepo hali kama hii mimi nimeifurahia sana. *(Makofi)*

Washimiwa Wabunge, ninao udhuru kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Spika, aje aendelee na shughuli zinazofuata.

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mapema leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama ya Bunge, likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutoa rambirambi zangu kwa familia, wapigakura, Kambi ya Upinzani na wananchi wote wa Tarime na Mkoa wa Mara kwa ujumla kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Tarime Marehemu Chacha Zakayo Wangwe, kilichotokea juzi tarehe 28 Julai, 2008 kwa ajali ya gari. Mimi binafsi nitamkumbuka sana Mheshimiwa Chacha Wangwe, kwa kuwa alikuwa rafiki yangu wa karibu sana. Kwa unyenyekevu mkubwa naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuungana na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa familia na wananchi wa Kiteto kwa kumpoteza aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Benedict Kiroya Losurutia. Aidha, natoa rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa wa Marehemu Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum kutokea Mkoa wa Kilimanjaro na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wenzetu hao walitutoka katika mwaka wa fedha uliopita wa 2007/2008. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Taifa lilikumbwa na msiba mkubwa ambapo wachimba madini wadogo wadogo maarufu kwa jina la Wana Apolo katika machimbo ya Mererani wapatao 72 walipoteza maisha kutokana na mafuriko katika migodi hiyo yaliyosababishwa na mvua za masika. Nachukua fursa hii kuwapa pole ndugu wa marehemu na waathirika wote wa tukio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maafa mengi yametokea zikiwemo ajali za barabarani na za ndege ambazo zimesababisha athari kwa wananchi na mali zao. Kwa waathirika wote wa matukio hayo nawapa pole. Aidha, nawapa pole wananchi wa Kyela ambao kufuatia mafuriko yaliyosababishwa na mvua za masika walipoteza mali zao pamoja na mashamba kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na halafu kuthibitishwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu. Tunatambua na kuheshimu dhamana kubwa aliyokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba zao walizozitoa mapema katika Mkutano huu wa 12 wa Bajeti ambazo pamoja na mambo mengine, zimetoa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na hali ya uchumi kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali katika Baraza jipya la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wetu ndani ya Bunge na wale wa Kamati za Kudumu za Bunge hili Tukufu pamoja na wasaidizi wako chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayowafanyia Watanzania. Nawapongeza pia Wabunge wenzangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mara baada ya kuundwa kwa Baraza jipya la Mawaziri. Naahidi kwa mara nyingine tena kufanya kazi hii kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama ya Bunge chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha pamoja na ushauri wao katika masuala mbalimbali ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda pia kumshukuru mke wangu Stella ambaye jana kwa mapenzi ya Mungu tumetimiza miaka 13 ya ndoa pamoja na watoto wangu Chela, Aman na Lau *Junior*, kwa uvumilivu wao na ushirikiano wao kwa kipindi chote ambacho nimekuwa mbali nao nikiwa nalitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hali ya amani na utulivu imeendelea kuwa ya kuridhisha licha ya baadhi ya matukio ambayo yalionekana kutishia usalama wa nchi yetu. Takwimu zilizopo zinaonyesha kulikuwa na jumla ya matukio ya jinai 509,462 yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi nchini kwa mwaka 2007 ikilinganishwa na matukio 428,629 yaliyoripotiwa mwaka 2006. Takwimu hizi zinaonyesha ongezeko la matukio 80,833 ambalo ni sawa na asilimia 18.9.

Kwa upande wa makosa ya usalama barabarani, mwaka 2007 yaliripotiwa jumla ya matukio 230,751 ikilinganishwa na matukio 109,868 yaliyoripotiwa mwaka 2006. Kuna ongezeko la matukio 120,883 ambalo ni sawa na asilimia 110 (Tazama Kiambatisho Na.1). Kuongezeka kwa matukio haya ya uhalifu kunatokana na sababu nyingi zikiwepo juhudi za polisi za kuendesha misako nchi nzima ambapo wahalifu wengi zaidi wamenaswa na vile vile kuongezeka imani ya wananchi kwa Jeshi la Polisi na hivyo wananchi wengi kuwa tayari zaidi kuripoti matukio ambayo hapo awali yalikuwa hayaripotiwi kutokana na huduma ambazo hazikuwa za kuridhisha katika Vituo vya Polisi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za matukio hayo ya uhalifu zinaonyesha kuna ongezeko zaidi katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tabora, Iringa, Kilimanjaro, Ruvuma, Kagera, Shinyanga, Arusha na Pwani. Ongezeko hili kwa kiwango kikubwa linatokana na kiwango kikubwa cha uhamiaji mijini ambalo haliendi sambamba na ongezeko la askari na hivyo kusababisha uwiano wa askari kwa raia kuwa mkubwa zaidi. Kwa sasa hivi uwiano huo ni 1:1339 badala ya 1:400 uliokubalika Kimataifa. Upungufu huu wa askari unasababisha kuwepo mtawanyiko mdogo wa askari kwenye maeneo wanayoishi wananchi na hivyo kuacha baadhi ya maeneo kubaki bila huduma ya polisi kama inavyotarajiwa. Kuwepo kwa maeneo yasiyo na huduma ya polisi kunatoa mwanya kwa wahalifu kutenda matukio ya uhalifu na hivyo kusababisha ongezeko la matukio ya uhalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, kukua kwa uchumi wa nchi yetu kumesababisha kuwepo shughuli nyingi zaidi za wananchi kujitafutia kipato. Hali hii imesababisha kuwepo urahisi wa watu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine nchini

na hata kutoka nchini mwetu kwenda nchi nyingine. Kama ambavyo imekuwa rahisi kwa raia wema kufanya shughuli zao za kujipatia kipato, vile vile wahalifu nao wameweza kutumia mwanya huo kufanya shughuli zao za kihalifu na hivyo kusababisha ongezeko la uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2007/2008. Sasa naomba kutoa tathmini ya utekelezaji wa malengo katika mwaka wa fedha uliopita wa 2007/2008 tukiongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Serikali ya jumla ya shilingi bilioni 20.5. Hadi mwisho wa mwezi Aprili, 2008 tulikuwa tumekusanya shilingi bilioni 20.8 sawa na asilimia 102 na hivyo kuvuka lengo kwa wastani wa asilimia 2. Mahesabu ya mwaka yatakapokamilishwa ni dhahiri lengo litavukwa zaidi ya hapo. Tumelenga kukusanya shilingi bilioni 30 katika mwaka ujao wa fedha wa 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka uliopita Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu matumizi ya kawaida ya jumla ya shilingi bilioni 199.1 na mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2008 zilikuwa zimetumika shilingi bilioni 181.2 sawa na asilimia 91. Kati ya hizo mishahara ilikuwa shilingi bilioni 79 na Matumizi Mengineyo *(OC)* shilingi bilioni 102.1. Aidha, shilingi bilioni 13.5 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Mpaka mwisho wa mwezi Aprili, 2008 tulitumia shilingi bilioni 10.3 sawa na asilimia 76.3 ya tengo la mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa Wizara una Idara tisa na vitengo sita. Kati ya idara hizo, sita ni idara kuu za kiutendaji ambazo ni Idara ya Polisi, Idara ya Magereza, Idara ya Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Uhamiaji, Idara ya Wakimbizi na Idara ya Huduma kwa Jamii. Idara tatu za huduma za kijumla ni Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Sera na Mipango na Idara ya Kushughulikia Malalamiko *(Complaints).* Idara hizi tatu hutoa huduma kwa Idara nyingine zote za Wizara kwa jumla. Vitengo sita vilivyopo ni Fedha na Uhasibu, Ukaguzi wa Ndani wa Mahesabu, Habari, Elimu na Mawasiliano, Ugavi, Kitengo cha Mfumo wa Habari *(Management Information System)* na kitengo cha Usajili wa Vyama *(Civil Societies). B*aada ya maelezo ya kijumla ya utekelezaji wa Bajeti niliyoyatoa awali, ifuatayo sasa ni taarifa kwa kila Idara kuu ya Kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za polisi. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Jeshi la Polisi liliboresha zaidi mikakati yake ya kupambana na uhalifu. Moja ya maboresho hayo ni kuwashirikisha wananchi katika suala zima la kulinda usalama wao na mali zao. Maana ya dhana ya ushirikishwaji wa wananchi ni Jeshi la Polisi kujenga mazingira ya uelewano kati yake na wananchi ili kwa pamoja waweze kutambua matatizo ya uhalifu yaliyoko katika jamii na kisha kwa kutumia taarifa sahihi za uhalifu na rasilimali walizonazo wanajamii kwa pamoja kukabiliana na changamoto za uhalifu. Hivyo basi, Polisi Jamii imejikita katika mihimili miwili ambayo ni ushirikiano baina ya Polisi na Jamii *(Police-Community Partnership)* na utatuzi wa matatizo kwa pamoja *(Joint problem solving).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limekuwa na mipango mbalimbali ya kuwahamasisha wananchi ili waweze kutoa ushirikiano wao kwa Polisi ili kazi ya kupambana na uhalifu iweze kufanyika kwa mafanikio. Mipango hiyo ni pamoja na Jeshi la Polisi kushiriki kwenye maonyesho ya Saba Saba ili kuwaelimisha wananchi shughuli mbalimbali zinazofanywa na Jeshi hilo, kutoa elimu kwenye shule za Msingi na Sekondari, Mtandao wa Ulinzi Jirani, vipeperushi, vipindi vya radio na televisheni na mikutano ya hadhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali katika suala zima la kupambana na uhalifu hasa ujambazi wa kutumia silaha, dawa za kulevya, umiliki haramu wa silaha ndogo ndogo na nyepesi, biashara haramu ya kusafirisha binadamu, usambazaji wa bidhaa bandia na ongezeko la ajali za barabarani. Ushirikiano huu umefanyika katika nyanja za ubadilishanaji wa taarifa za uhalifu na wahalifu, mafunzo na operesheni mbalimbali. Wadau ambao Jeshi la Polisi limekuwa likishirikiana nao ni pamoja na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Idara ya Usalama wa Taifa, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Magereza, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji Majini na Nchi Kavu *(SUMATRA)*, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua ukweli kwamba uhalifu hauna mipaka, Jeshi la Polisi limeendelea kuimarisha ushirikiano na Majeshi mengine ya Polisi ulimwenguni. Ushirikiano huo ni ule wa Kimataifa na wa Kikanda ambapo Jeshi la Polisi Tanzania ni mwanachama. Jeshi letu la Polisi limekuwa likishirikiana na Shirikisho la Polisi la Kimataifa *(INTERPOL)*, Shirikisho la Polisi la nchi za Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika *(EAPCCO)*, na Shirikisho la Polisi la nchi za Kusini mwa Afrika *(SARPCCO)*. Ushirikiano huo unahusisha ubadilishanaji wa taarifa za kihalifu na wahalifu, operesheni za pamoja za kukabiliana na uhalifu wa Kimataifa, mikutano na semina mbalimbali, na mafunzo yanayolenga kukabiliana na changamoto za uhalifu wa kimataifa *(International Organized Crime)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Bunge lilitunga sheria ya kuhamisha jukumu la uendeshaji mashtaka kutoka Polisi kwenda kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka *(Civilianization of Prosecution)* kwa lengo la kutenganisha majukumu ili kuimarisha uwajibikaji. Kwa upande wake Jeshi la Polisi limeendesha mafunzo mbalimbali kwa wapelelezi kwa lengo la kuwajengea uwezo zaidi ili waweze kupeleleza kesi kwa haraka na kwa ufanisi unaotakiwa. Vile vile Jeshi la Polisi linaendelea kupitia mifumo mbalimbali inayotumika katika upelelezi wa makosa ya jinai kwa lengo la kuiboresha ili iweze kuendana na mazingira ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Jeshi la Polisi liliwapa mafunzo mbalimbali askari na maafisa 10,085 ndani ya nchi na 33 nje ya nchi. Aidha, idadi kubwa ya askari walipatiwa mafunzo wakiwa kazini. Mafunzo haya yamesaidia sana kuwajengea uwezo wa kiutendaji askari hao kiasi cha kuwezesha kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi katika utoaji huduma zake kwa wananchi. Kuboreshwa kwa huduma za polisi kumesaidia kuwashawishi wananchi wengi zaidi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi na kufanya kazi ya polisi ya kupambana na wahalifu kuwa na mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeboresha mbinu zake za kupambana na uhalifu pamoja na mazingira ya kufanyia kazi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008 Jeshi la Polisi liliendelea na ujenzi pia ukarabati wa nyumba za kuishi askari na majengo mengineyo kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba za makazi. Mradi wa ujenzi wa nyumba 60 za ghorofa tatu kila moja za kuishi familia 240 za askari. Mgawanyo wa nyumba hizo ni kama ifuatavyo:-

Kambi za Polisi *Kilwa Road*, Dar es Salaam 54, Ziwani – Unguja tatu na Limbani - Kaskazini Pemba tatu. Mradi huu umeanza kwa mkopo wa fedha kutoka *NSSF* na unaendelea vizuri, ujenzi wa nyumba mbili za ghorofa moja kila moja unaendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Kituo cha Polisi

Namtumbo Mkoa wa Ruvuma umekamilika, ujenzi wa nyumba tatu za familia nne kila moja za askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia wa Kambi ya Finya - Pemba umekamilika, ujenzi wa nyumba ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja umekamilika, ujenzi wa nyumba ya kuishi familia mbili za askari Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma umekamilika na ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Kituo cha Polisi Bahi Wilaya ya Bahi, umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa nyumba za makazi. Ukarabati wa nyumba za askari zilizoko kwenye Kambi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia *(FFU)* Machui na Tunguu Kusini Unguja unaendelea, ukarabati wa nyumba mbili za Maafisa Msasani, ghorofa moja Kambi ya Buguruni na Bwalo la Maafisa wa Polisi Oysterbay nao unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara imejenga na kukarabati majengo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ofisi, maktaba na chuo. Ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mwanza na Kikosi cha *FFU* Dodoma umekamilika, ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Tabora, na Kilimanjaro unaendelea, ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Polisi wa Wilaya za Morogoro, Mpanda, Ludewa, Newala na Chato unaendelea, ujenzi wa kituo cha Polisi Makambako unaendelea, ujenzi wa Ofisi ya Polisi Usalama Barabarani Mkoani Arusha unaendelea, ujenzi wa maktaba na vyumba viwili vya madarasa Chuo cha Polisi Zanzibar unaendelea, wakati ujenzi wa jiko, hodhi la maji na vyoo katika chuo hicho umekamilika na hatua za awali za maandalizi ya michoro na uchambuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Upelelezi Dodoma zimekamilika. Usanifu wa michoro unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa ofisi na vyuo. Ukarabati wa Ofisi za Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kituo cha Polisi *Mbamba Bay* umekamilika. Aidha, ukarabati wa ofisi ya Mkuu wa Polisi wilaya ya Mbinga unaendelea, ukarabati wa mabweni na mifumo ya maji safi umekamilika katika Chuo cha Polisi Moshi na ukarabati wa majengo ya Chuo cha Polisi Kidatu - Morogoro unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Jeshi la Polisi limenunua magari 95 na pikipiki tisa kwa lengo la kuimarisha shughuli za usafiri na usafirishaji. Aidha, Jeshi la Polisi limenunua nyumba 22 zilizoko Kigamboni Jijini Dar es Salaam zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya *TIPPER.* Nyumba hizo zimekwishafanyiwa ukarabati na askari wamekwishahamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi na usalama ni nguzo muhimu kwa maendeleo na uwekezaji. Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao ndilo jukumu la msingi la Jeshi la Polisi. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Jeshi la Polisi limefanya yafuatayo:-

Kwanza ni operesheni na doria za Polisi zilifanyika katika Mikoa yote nchini, pili, operesheni ya kudhibiti makosa ya uhalifu wa Kimataifa iliendelea kwa kushirikisha baadhi ya nchi za *SADC* za Malawi, Zambia na Mauritius, tatu, Jeshi la Polisi limeandaa programu ya miaka saba (2007/2008 -2013/2014) ya Maboresho ya Jeshi *(Police Force Reform Programme)* yenye malengo makuu yafuatayo:-

(a) Kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa, linalozingatia taaluma na linaloshirikiana na Jamii *(Mordenization, professionalism & Community Policing).*

(b) Warsha za uhamasishaji kuhusu Polisi Jamii/Ulinzi Shirikishi kama mkakati wa kukabiliana na uhalifu zimeendelea kutolewa kwa wananchi.

(c ) Wizara imekamilisha rasimu ya Sera ya Usalama wa Raia ambapo Polisi Jamii ni moja wapo ya mikakati ya kutekeleza Sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Magereza. Jukumu la Jeshi la Magereza ni kuhifadhi wafungwa na mahabusu wa aina zote pamoja na kurekebisha tabia za wale waliohukumiwa vifungo. Kazi zote hizi zimeendeshwa kwa mujibu wa sheria. Urekebishaji wa tabia za wafungwa ili wamalizapo vifungo vyao wawe raia wema katika jamii hufanywa kupitia programu za mafunzo kwa njia ya vitendo katika miradi ya ujenzi, kilimo na viwanda vidogo vidogo, mafunzo ya nadharia katika Chuo cha Magereza Ruanda - Mbeya, Gereza la Vijana Wami na utoaji ushauri nasaha kwa kutumia walimu wa dini na Maafisa Ustawi wa Jamii. Hata hivyo jukumu hilo limeendelea kutekelezwa katika mazingira magumu kutokana na ufinyu wa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani. Uwezo wa sasa wa magereza kisheria ni kuhifadhi wafungwa na mahabusu 27,653 ukilinganisha na uwezo uliokuwepo awali wa kuhifadhi wafungwa 22,669 tu. Ongezeko hili ni kutokana na jitihada za Serikali za kukarabati, kukamilisha, kupanua na kujenga mabweni ya wafungwa katika vituo mbalimbali. Tarehe 1 Juni, 2008 kulikuwepo wafungwa na mahabusu 39,951. Kiwango hiki ni kikubwa zaidi kwa kuwa na idadi ya mahabusu na wafungwa 12,298 ambao ni sawa na asilimia 44 ukilinganisha na uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu magerezani uliopo nchini kote. (Kiambatisho Na. 4 kinatoa mchanganuo wa idadi ya wafungwa na mahabusu wa aina zote Tanzania Bara pamoja na uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu magerezani kisheria nchini kote).

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za Kukabiliana na tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Jeshi la Magereza limechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *Parole*. *Parole* ni utaratibu unaotumika kuwaachilia wafungwa wa vifungo virefu wenye tabia njema magerezani ili watumikie sehemu ya vifungo vyao iliyobaki nje ya magereza chini ya masharti maalum kwa kutumia Sheria ya Bodi za *Parole* Na. 25/1994. *(Makofi)*

Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 wafungwa 233 waliachiliwa kwa utaratibu wa *Parole*. Kama inavyoonekana idadi hii ni ndogo. Tatizo la utaratibu huu ni wigo finyu wa sheria ya Bodi za *Parole* inayosababisha wafungwa walio wengi kutofaidika na mpango huu kutokana na makosa yao kuwa yenye hisia kali kwa jamii. Hata hivyo Wizara imeshakamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Bodi za *Parole* ya mwaka 1994 ili kupanua wigo wa wafungwa wanaoweza kunufaika na utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha wa Rais. Jumla ya wafungwa 7,696 walifaidika na msamaha wa Rais. Wafungwa 4,049 walifaidika na msamaha uliotolewa tarehe 9 Desemba, 2007 siku ya sherehe za miaka 46 ya Uhuru na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wafungwa 279 waliachiliwa kwa msamaha maalum. Wafungwa wengine 3,368 waliachiliwa kwa msamaha wa kawaida uliotolewa tarehe 26 Aprili, 2008 katika kilele cha sherehe za miaka 44 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungo cha nje. Kwa mujibu wa Sheria Kuu ya Magereza Namba 34 ya mwaka 1967 *(Prisons Act, No.34 of 1967),* wafungwa wanaostahili kutolewa na kutumikia kifungo cha nje ni wale wanaotumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2007 hadi 1 Mei, 2008 wafungwa 736 walikuwa wanatumikia kifungo cha nje kwa kutumia kanuni za kifungo cha nje za mwaka 1968. Hata hivyo utaratibu huu unashindikana kutumika kikamilifu sehemu nyingi kwa kuwa Halmashauri za miji hazina fedha za kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa Magereza. Jitihada zinafanywa na Jeshi la Magereza kujenga Magereza katika wilaya mpya na ukarabati wa mabweni ya zamani yaliyochakaa utafanyika ili kuongeza nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, urekebishaji wa Sheria. Jeshi la Magereza litaendelea kutoa ushauri juu ya sheria ya utoaji wa adhabu za vifungo virefu, upelelezi wa kesi mbalimbali za mahabusu na utoaji dhamana kwa wale ambao hawajafikishwa gerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu za urekebishaji wafungwa zimeendelea kutekelezwa kwa njia ya vitendo kupitia ujenzi, viwanda vidogo vidogo, kilimo, mifugo na utunzaji wa mazingira. Jukumu la urekebishaji wa wafungwa hufanyika kwa kuwafundisha stadi mbalimbali za kazi kama vile uashi, ufundi rangi, bomba, umeme, kilimo bora cha mazao mbalimbali na bustani, umwagiliaji, upandaji miti na ufugaji. Stadi za kazi nyingine ni ufundi seremala, ushonaji na ufumaji nguo wa aina mbalimbali zikiwemo sare za wafungwa na askari, utengenezaji wa sabuni, chokaa, chumvi, vifaa vya henzerani, majiko na masanduku ya bati.

Aidha, mafunzo kwa askari na wafungwa yanaendelea katika Chuo cha Ufundi cha Mbeya na masomo wanayofundishwa ni uashi, useremala, ufundi bomba, umeme na rangi. Mafunzo haya yanakusudia kuongeza ufanisi kwenye miradi yetu ya maendeleo na shughuli mbalimbali magerezani hivyo kutekeleza kwa nadharia na vitendo sera ya urekebishaji wa wafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya askari. Jumla ya askari na maofisa 1,321 wa vyeo mbalimbali wamehudhuria na kuhitimu mafunzo ya ngazi mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa magereza kupitia vyuo vya ndani ya Jeshi. Mafunzo hayo ni Utawala wa Magereza, Cheti cha Sheria, stadi mbalimbali za ufundi na udereva. Mchakato wa kuajiri askari wapya 816 ambao watapatiwa mafunzo ya awali ya uaskari Chuo cha Magereza Kiwira umekamilika. Aidha, wapo watumishi 508 wanaosomea taaluma mbalimbali nje ya vyuo vya Jeshi la Magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya Jeshi la Magereza katika mwaka wa fedha 2007/2008 umekuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba za kuishi na ofisi, upanuzi na ujenzi wa mabweni ya wafungwa uliendelea katika Magereza ya Mahabusu Tabora, Kambi - Mvuti, Mkuza, Kibiti, Kigongoni na Nkasi, ujenzi na uboreshaji sehemu za kupumzikia wafungwa unaendelea katika Magereza ya mahabusu ya Singida na Mbozi, ujenzi wa majengo ya Utawala katika Magereza ya Magu, Kayanga, Rombo, Mang'ola, Isupilo na Kyela umekamilika na ujenzi wa nyumba za askari katika Magereza ya Ukonga, Muleba, Babati, Mbinga, Igunga, Mahabusu Iringa, Utete na Mbarali umeendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ujenzi wa mifumo ya majitaka katika Magereza ya Loliondo, Newala, Kasulu, Nzega, Bagamoyo, Musoma, Meatu na Bangwe umeendelezwa, ujenzi wa mfumo wa majisafi katika Gereza la Isupilo unaendelea. Utafiti wa kuchimba kisima kirefu katika Gereza la Liwale umeanza na ujenzi wa bwawa la kumwagilia mpunga katika Gereza la Mang'ola - Karatu kwa ufadhili wa *Tanzania/Japan Food Aid Counterpart Fund* unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa nyumba za kuishi na ofisi, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Magereza ambalo kwa sasa limeanza kutumika rasmi tangu tarehe 31 Desemba, 2007 umekamilika, ukarabati na uboreshaji wa majengo na miundombinu ya magereza yenye ulinzi mkali umefanyika na unaendelea katika Magereza ya Keko, Lilungu, Ukonga na Gereza Maalum Isanga. Pia ukarabati na ukamilishaji wa mabweni ya wafungwa uliendelea katika Magereza ya mahabusu ya Morogoro, Geita, mahabusu Mugumu, Kyela, Mbinga, Meatu, Mkuza, Kwamngumi, Kanegele na Isupilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia na upimaji wa maeneo. Fidia ya mazao na majengo katika eneo la upanuzi wa Gereza la Mahabusu Segerea imelipwa na upimaji wa maeneo umekamilika katika Magereza ya Ubena, Wami Kuu, Wami Vijana na Rwamrumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Magereza *(Prisons Corporation Sole)*. Ndani ya Jeshi la Magereza, lipo Shirika la Magereza *(Prison's Corporation Sole)* lililoanzishwa chini ya Sheria Na. 23/1974 *(The Corporations Sole Establishment Act, 1974)* kwa madhumuni ya kuendesha programu za urekebishaji wa wafungwa kwa njia ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na viwanda vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Magereza linayo miradi ya kilimo na mifugo 15 na miradi ya viwanda vidogo vidogo nane, hivyo kufanya jumla ya miradi yote kuwa 23 ambayo aidha, lengo lake ni kuwafundisha wafungwa stadi za kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Shirika limeendelea kuimarisha viwanda kwa kufunga mashine mpya katika Kiwanda cha Viatu Karanga, Moshi na Uhunzi katika Gereza Ukonga. Jitihada za kuboresha mashamba ya mazao zilifanyika kwa Shirika kununua pembejeo za kutosha na Serikali kutoa ruzuku ya zana za kilimo kwenye mashamba ya magereza ya Mollo, Sumbawanga na Songwe, Mbeya ambapo jumla ya ekari 1,000 za mahindi zimelimwa. Aidha, ekari 500 za mpunga zimelimwa katika shamba la Gereza Idete lililoko Ifakara, Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Usindikizaji wa Mahabusu Mahakamani. Katika mwaka 2007/08, Jeshi la Magereza limepokea magari 14 kwa ajili ya utekelezaji wa jukumu la kusafirisha mahabusu kwenda mahakamani na kurudi gerezani kama ifuatavyo: Mabasi makubwa 3, Mabasi madogo 4, Gari dogo 1 na *pick-ups* 6.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hilo lilianza rasmi tarehe 19/05/2008 kwa mahabusu waliopo Mkoa wa Dar es Salaam na wale wa Wilaya za Kisarawe, Mkuranga na Kibaha Mkoa wa Pwani. Utekelezaji wa jukumu hili umeonyesha mafanikio makubwa kwa sababu ya kutokuwepo kwa malalamiko ya baadhi ya mahabusu kutofikishwa mahakamani kwa tarehe walizopangiwa. Kesi za mahabusu zimekuwa zikisikilizwa kwa tarehe zilizopangwa na kumalizika katika muda muafaka hatua itakayosaidia kupunguza msongamano Magerezani

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Jeshi la Magereza liliendelea na juhudi za kuboresha mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yake kote nchini. Siku ya upandaji miti kitaifa tarehe 1 Januari, 2008 jumla ya miti 67,279 ilipandwa katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa yamepata mvua kufikia tarehe hiyo. Aidha, hadi sasa idadi ya miti yote iliyopandwa ni 3,701,594. Kati ya hiyo, miti 356,334 imepandwa katika magereza ya Idete, Msalato na Isupilo kwa ufadhili wa *NORAD* ikishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii. Miti inayopandwa ni kwa ajili ya matumizi ya kuni, mbao, matunda, kivuli, mapambo na malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanya misitu kuwa endelevu, tumeanzisha ufugaji wa nyuki katika vituo vya Bariadi, Malya, Kasungamile, Mgagao, Ngwala, Songwe na Wami Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza limekuwa mdau mkubwa katika zoezi la kupanda miti si kwa ajili ya kuboresha mazingira tu, bali kwa sababu ni mtumiaji mkubwa wa miti kwa ajili ya kuni za kupikia chakula cha wafungwa. Hadi sasa, hatua zilizochukuliwa na Jeshi la Magereza kuhusiana na matumizi ya Nishati mbadala ni pamoja na kutumia makaa ya mawe kwa vituo vya mkoa wa Mbeya, kutumia *Liquid Petroleum Gas (LPG)* Chuo cha Maafisa wa Magereza Ukonga na kutumia gesi asilia katika gereza la Keko Dar es Salaam. Aidha, Jeshi la Magereza limesaini mkataba na Kampuni ya *Tanzania Biogas and Solar Ltd* ambayo itajenga mitambo ya Biogas katika gereza Ukonga Dar es Salaam. Mkandarasi ameshaanza maandalizi kwa kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu kwa umma, Jeshi la Magereza lina kipindi kijulikanacho kwa jina la IJUE MAGEREZA kinachorushwa na Shirika la Utangazaji Tanzania kila wiki. Aidha, gazeti la Sauti ya Magereza pamoja na vipeperushi vya Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa lugha ya Kiswahili limeendelea kuchapishwa na kusambazwa katika magereza yote pamoja na kuweka mabango kwenye milango ya magereza ili kuendelea kuielimisha jamii kuhusu majukumu muhimu ya Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma kwa Jamii (*Community Service).* Sheria ya huduma kwa Jamii Na.6 *(Community Service Act. No.6)* ya mwaka 2002 ilianza kutumika katika mikoa 6 kuanzia mwaka 2005 na sasa imefikia mikoa 12. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Mwanza, Dodoma na Shinyanga. Mingine ni Iringa, Mbeya, Kagera, Mara na Mtwara. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei mwaka huu jumla ya wafungwa 732 wamefaidika na Programu ya Huduma kwa Jamii. Wafungwa hawa wamekuwa wakifanya kazi mbalimbali katika Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Wakimbizi. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008 nchi yetu imeendelea kuhifadhi maelfu ya wakimbizi ambapo mpaka tarehe 31/05/2008 tulikuwa na wakimbizi 404,782. Kati yao 303,808 ni kutoka Burundi, na 98,990 ni kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), 1,789 ni Wasomali na 195 wanatoka mataifa mengine yakiwemo Rwanda, Sudan, Uganda, Ethiopia, Kenya na Zimbabwe. (Rejea Kiambatisho Na.6 kinachoonyesha mchanganuo wa wakimbizi hao kwa kila kambi).

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuwarejesha kwao wakimbizi linaendelea. Utekelezaji wa zoezi hili unatokana na maamuzi ya Tume mbili za Pande Tatu *(Tripartite Commissions)* moja inayohusisha nchi za Burundi, Tanzania na *UNHCR* na nyingine Tanzania, DRC na *UNHCR.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu zoezi la urejeshaji wakimbizi lilipoanza rasmi mwaka 2002, jumla ya Wakimbizi 464,966 wamerejea kwao (Tazama Kiambatisho Na.7) na jumla ya kambi nane (8) ambazo ni Kitali, Karago, Mtendeli, Kanembwa, Lugufu II, Muyovosi, Mkugwa na Lukole B zimefungwa kati ya Kambi 13 zilizokuwepo kwa kipindi cha kati ya mwaka 2002-2008. kwa mwaka 2007/08 pekee hadi tarehe 31 Mei 2008 wakimbizi 71,021 wamerejea kwao. Kati yao 51,906 ni kutoka Burundi, na 19,115 kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, katika kipindi hicho Kambi mbili (2) za Lugufu II na Kanembwa zimefungwa. Mpaka hivi sasa jumla ya Kambi nne (4) zimebaki ambazo ni Nduta (Kibondo), Mtabila na Nyarugusu (Kasulu) na Lugufu I (Kigoma Vijijini).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa nchi yetu imeanza awamu nyingine ya utekelezaji wa zoezi la kuwarejesha wakimbizi wa Burundi ambao sasa walengwa ni wakimbizi waliokimbilia nchini mwaka 1972, ambao wanaishi kwenye Makazi ya Wakimbizi ya Mishamo na Katumba Wilaya ya Mpanda-Rukwa na Ulyankulu Wilaya ya Urambo-Tabora. Hii inatokana na tathmini iliyofanyika mwezi Septemba 2007 na kuonyesha kwamba asilimia 19 ya wakimbizi 216,350 wanaoishi katika makazi hayo wangependa kurejea kwao. Zoezi la kuwarejesha kwao lilizinduliwa rasmi na Kamishna Mkuu wa Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) Bw. Antonio Guterres tarehe 9/03/2008 wilayani Mpanda ambapo Wakimbizi wa mwanzo 255 kutoka Makazi ya Katumba na Mishamo waliondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 31 Mei 2008 tayari Wakimbizi 1,745 walikuwa wamerejea Burundi toka kwenye makazi haya. Hata hivyo, zoezi hili haliendi kwa kasi iliyotarajiwa kutokana na matatizo ya barabara na usafiri kwa jumla hasa wakati wa masika katika maeneo hayo. Usafiri pekee ambao wakimbizi hao walikuwa wanategemea ni kutumia Kampuni ya Reli Tanzania ambayo kwa kipindi fulani ilikumbwa na migogoro ya kikazi ya mara kwa mara, hivyo kusababisha kuahirishwa kwa misafara ya kuwarejesha wakimbizi. Kwa kuwa kipindi cha masika kimemalizika tunatarajia kasi itaongezeka majira ya kiangazi kuanzia mwezi Juni na kuendelea hadi Oktoba/Novemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma yetu kuwa, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2008 wakimbizi wote wawe wamerejea kwao kwa hiari na kambi zilizopo katika mikoa ya Kigoma na Kagera ziwe zimefungwa. (Rejea Kiambatisho Na.8 kinachoonyesha takwimu za urejeaji wa wakimbizi).

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia mwezi Mei 2008, jumla ya wakimbizi 5,051 wamehamishiwa nchini Marekani kutokana na mpango wa Serikali ya Marekani wa kuwapa makazi *(resettlement)* wakimbizi kati ya 13,000 – 15,000 wa Burundi katika kipindi cha 2005-2008. Wakimbizi hawa ni wale walioingia nchini mwaka 1972 wakawa wanaishi Mikoa ya Kigoma na Kagera. Mpango huu unatekelezwa kwa pamoja kati ya Shirika la Kimataifa la Uhamiaji *(International Organisation for Migration)*, Serikali za Marekani na Tanzania na Shirika la *UNHCR.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, katika tathmini iliyofanywa kwa wakimbizi wa Burundi wanaoishi kwenye Makazi, asilimia 81 ya wakimbizi hao wameomba kubaki nchini. Hivyo Serikali inaendelea na mchakato wa kuwapa fomu za maombi ya uraia kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za Uhamiaji nchini. Hata hivyo hakuna atakayeruhusiwa kuendelea kuishi ndani ya makazi hayo baada ya kupata uraia, bali watatakiwa kuishi kwenye maeneo mengine ya Tanzania nje ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2007 hadi Desemba 2007 Serikali tayari imewapa uraia wakimbizi 550 kutoka Somalia wenye asili ya Kizigua wanaoishi katika makazi ya Chogo, Wilaya ya Handeni, Mkoani Tanga. Hivyo hadi hivi sasa wakimbizi wa Somalia waliopewa uraia ni 732, na bado Wizara yangu inashughulikia maombi mengine ya wakimbizi 1,792 waliobaki. Kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Wizara yangu ya mwaka jana Bungeni, uamuzi wa kuwapa uraia wakimbizi wa Somalia, ambao ni wa pekee, unatokana na ukweli kuwa wakimbizi hao asili yao ni Tanzania na wameonesha nia ya dhati ya kuendelea kuishi hapa nchini hata kama hali ya amani na utulivu itarejea nchini Somalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Zimamoto na Uokoaji. Majukumu ya msingi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa mujibu wa sheria mpya, *The Fire and Rescue Force Act Na. 14* ya mwaka 2007" ni kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye maeneo mbalimbali, kuzima moto, kuokoa maisha na mali kwenye majanga ya moto na majanga mengineyo, pia kuelimisha Umma juu ya tahadhari ya moto na kinga ya moto na majanga mengineyo ambayo yanaweza kulikumba Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imeanza kutumika tarehe 1 Juni, 2008. Kanuni zake za Kiutumishi na Kiutendaji zimeanza kutumika tarehe 21 Julai, 2008. Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inalenga kuwa na Komandi moja. Pamoja na Sheria hiyo, pia Muundo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji unaainisha mfumo wenye mtiririko kuanzia Kamishna Jenerali hadi Makamanda wa Zimamoto wa Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Halmashauri za Miji, Manispaa pamoja na Jiji katika ununuzi wa magari ya kuzima moto na uokoaji. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Halmashauri zilizonufaika ni Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza, Bagamoyo, Mpanda na Njombe. Aidha ajira ya askari wa Zimamoto na Uokoaji 170 imefanyika. Kati yao 72 wamepatiwa mafunzo katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji. Waliobaki watapatiwa mafunzo katika mwaka wa fedha 2008/2009. Mafunzo yaliyotolewa kwa Askari wa Zimamoto na Uokoaji 72 yataleta ufanisi katika shughuli za kuzima moto na uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto lilifanyika katika taasisi mbalimbali. Jumla ya maeneo 3,496 yalikaguliwa. (Kiambatisho Na.9 ni mchanganuo wa maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi).

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Uhamiaji. Jukumu la msingi la Idara ya Uhamiaji ni kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaaji wa wageni na pia kuwawezesha raia wa Tanzania kupata hati za kusafiria. Aidha, Idara hii ndio inayoratibu mchakato wa maombi ya uraia kwa wageni wanaoomba uraia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2007 hadi Mei, 2008, jumla ya wageni 732,328 waliingia nchini, ikilinganishwa na wageni 531,834 walioingia nchini katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Aidha, wageni 681,750 walitoka ikilinganishwa na wageni 504,742 waliotoka nchini katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Kwa jumla idadi ya wageni walioingia na kutoka nchini imeongezeka. Ongezeko hili linatokana na hali ya amani, utulivu na usalama iliyopo nchini na mazingira bora ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2007 hadi Juni, 2008 wageni 12,415 walipewa vibali vya kuishi nchini ikilinganishwa na wageni 6,943 waliopewa vibali mwaka 2006/2007. Aidha, kuanzia Julai, 2007 hadi Juni 2008, vibali 1,838 viliongezewa

muda ikilinganishwa na vibali 1,619 vilivyoongezewa muda katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Ongezeko hili kama nilivyokwisha kutanabahisha hapo awali linatokana na hali ya amani, utulivu na usalama iliyopo nchini, mazingira bora ya uwekezaji na kuongezeka kwa matangazo na vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ongezeko la utoaji vibali kwa wageni wanaoingia na kuishi nchini kihalali, pia kumejitokeza tatizo la wimbi la wageni kuingia na kuishi nchini kinyume cha sheria. Katika kipindi cha Julai 2007 hadi Juni, 2008 doria na misako yenye lengo la kudhibiti wageni haramu nchini, lilifanyika sehemu mbalimbali kama vile mahotelini, migodini, Vijijini, Mijini na sehemu nyingine zenye mikusanyiko mikubwa na zile za maficho. Kutokana na zoezi hilo, jumla ya wageni 3,445 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikilinganishwa na wageni 1,876 waliokamatwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007. Aidha jumla ya wahamiaji haramu 1,635 kutoka nchi za Pembe ya Afrika hususan Somalia (514) na Ethiopia (1,121) walikamatwa na wapo katika magereza mbalimbali hapa nchini wakati Serikali inatafuta fedha za kuwarudisha kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuratibu maombi ya wageni wanaoomba uraia wa Tanzania. Katika kuratibu mchakato wa maombi ya wageni wanaotaka uraia wa Tanzania, katika kipindi cha 2007/2008 Wizara yangu imeweza kuwapa uraia wageni 177 waliotimiza masharti, na wageni 9 walikataliwa maombi yao ya uraia kutokana na kutokuwa na sifa zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008, Watanzania 63 waliukana uraia wa Tanzania na kupata uraia wa nchi nyingine. Watanzania wengi wanaoukana uraia wetu ni wanawake. Kati ya idadi hiyo wanawake ni 50, ambao ni sawa na asilimia 79.4 kutokana na wengi wao kuolewa na wageni wa mataifa mengine. Wengine ni wanaume 13, ambao ni sawa na asilimia 20.6 ambao hulazimika kuukana uraia wetu kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kupata ajira ughaibuni na kupata mafao mengine yatolewayo kwa raia husika wa nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pasipoti na Hati za Kusafiri; katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Idara ya Uhamiaji imetoa jumla ya pasipoti 73,568. Kati ya hizo 70,198 ni za kawaida, 2,857 ni za Afrika Mashariki, 408 za kibalozi na 105 za kiutumishi, ikilinganishwa na jumla ya pasipoti 52,345 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka jana. Katika kipindi hicho zilitolewa pasipoti 88 za kitumishi, 273 za kibalozi, 1,675 za Afrika Mashariki na 50,309 za kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu pia imekuwa ikikabiliwa na tatizo sugu la vijana wetu wa Kitanzania kwenda nje ya nchi kinyume cha sheria, kwa visingizio vya kutafuta maisha bora zaidi. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, vijana 382 walirudishwa nchini toka nchi mbalimbali baada ya kubainika kwamba wapo kwenye nchi hizo kinyume cha Sheria za nchi husika, ikilinganishwa na vijana 193 waliorudishwa nchini mwaka jana. (Tazama Kiambatisho Na.10 kinachoonyesha mlinganisho wa huduma zilizotolewa na Idara ya Uhamiaji kwa miaka ya 2006/2007 na 2007/2008 hadi Juni kwa miaka hiyo).

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango mingine iliyotekelezwa na idara ya Uhamiaji kwa mwaka uliopita wa 2007/08 ni pamoja na:-

- Ujenzi wa nyumba za kuishi na Ofisi: Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam na upanuzi wa Ofisi Kuu Zanzibar unaendelea;

· Ukarabati wa nyumba za kuishi na Ofisi: Ukarabati wa majengo na ufungaji wa kompyuta katika Chuo cha Mafunzo ya Uhamiaji Mjini Moshi umekamilika. Dhamira ni kukifanya chuo hicho kuwa cha kanda *(Regional Academy)* ya Afrika Mashariki *(EAC);*

· Mitambo ya kutunza kumbukumbu: Katika jitihada za kutunza kumbukumbu muhimu, Idara imeanza mradi wa kutunza kumbukumbu za wateja kwa njia ya kisasa *(Archiving and Scanning)* Mtoni Kijichi-Dar es Salaam. Mradi huu utaendelezwa kadri bajeti itakavyoruhusu hadi kumbukumbu zote za idara ziwekwe kwenye mfumo wa kisasa;

· Ununuzi Katika kuongezea idara uwezo wa kiutendaji, ununuzi wa Magari 8 na pikipiki 12 umefanyika;

· Misako: Misako na doria imefanyika kwa ushirikiano na Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA);*

· Mitambo ya *Visa Stickers* kwa ajili ya kutoa visa kwa kompyuta imefungwa katika vituo 19 vya kuingilia nchini ambavyo ni Viwanja vya Ndege vya Mwalimu Julius Nyerere, Kilimanjaro, Zanzibar na Mwanza. Vingine ni Namanga, Holili, Horohoro, Sirari, Mtukula, Rusumo, Kabanga, Manyovu, Tunduma, Kasumulu, Kasesya, Kilambo na Tarakea pamoja na bandari ya Zanzibar na Kigoma;

· Askari wa Uhamiaji wapya 175 wameajiriwa;

· Watumishi 179 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi na nje na ndani ya nchi kwa lengo la kujenga uwezo na kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji pia imeendelea na zoezi la uboreshaji wa mfumo wa *Personal Identification, Secure, Comparison and Evaluation System (PISCES)* ili kudhibiti uingiaji wa wageni nchini. Mitambo hiyo imefungwa kwenye viwanja vya Ndege vya kimataifa vya Mwalimu Julius Nyerere, Kilimanjaro na Zanzibar na bandari ya Zanzibar na mji wa Namanga. Hatimaye mitambo hiyo itaunganishwa na Makao Makuu ili kuimarisha ufuatiliaji wa karibu wa taarifa za wageni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uandikishaji Wageni wakaazi *(Foreign Residents)* katika daftari la Wahamiaji. Wizara yangu ina dhamana ya kutambua nani ni raia na nani si raia. Katika kutekeleza jukumu hilo Idara ya Uhamiaji imekwishaanza mchakato wa kuorodhesha idadi ya wageni wanaoishi sehemu mbalimbali hapa nchini katika daftari ambalo litasaidia kuendesha zoezi muhimu la utambuzi na uandikishaji wa watu wakati wa zoezi la utoaji wa vitambulisho vya Taifa kwa raia na wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vitambulisho vya Taifa. Katika Bunge lako la bajeti la mwaka 2007/2008 nilitoa maelezo kuhusu maendeleo ya mradi wa vitambulisho. Napenda kuchukua nafasi hii kulijulisha Bunge hili kuwa Wizara yangu imekwisha karabati jengo la Ofisi anzilishi ya mradi na kumteua Mratibu wa mradi atakayesimamia shughuli zote za mradi. Aidha Wizara yangu ikishirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na asasi nyingine zipo katika hatua za mwisho za kuunda chombo kitakachosimamia na kuendesha zoezi la utoaji wa vitambulisho vya Taifa. Katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi Wizara yangu imekwisha tangaza zabuni ili kumpata mzabuni atakayejenga mfumo mzima wa utunzaji kumbukumbu *(data base)* kwa nchi nzima. Hatua

hii ni muhimu sana katika utekelezaji wa mradi, kwa kuwa kumbukumbu hizo ndizo zitatumika kutengeneza vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usajili wa Vyama vya Kijamii *(Civil Societies)*. Usajili wa Vyama vya Kijamii unasimamiwa na kuratibiwa na Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama hivyo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008 jumla ya Vyama 290 viliandikishwa, ikilinganishwa na Vyama 399 vilivyoandikishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha uliopita. Idadi hii inafanya jumla ya Vyama vilivyoandikishwa hadi sasa kwa mujibu wa sheria kuwa 5,426.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za kushughulikia Malalamiko. Kutokana na kuongezeka kwa malalamiko ya wananchi dhidi ya utendaji kazi wa vyombo vilivyopo chini ya Wizara yangu, katika mwaka wa fedha uliopita wa 2007/08 Serikali iliamua kuunda Idara chini ya Wizara yangu na kupewa jukumu la kushughulikia malalamiko ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/08, Idara ya kushughulikia malalamiko ilipokea jumla ya malalamiko 1,166. Kati ya hayo, malalamiko 1,164 yalihusu Jeshi la Polisi, lalamiko 1 Jeshi la Magereza na lalamiko 1 Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko dhidi ya Jeshi la Polisi yalihusu ubambikizaji wa kesi, ucheleweshaji wa upelelezi, Polisi kupora mali na fedha za watuhumiwa wakati wa upekuzi, watuhumiwa kudhalilishwa wakati wa kukamatwa na mahojiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko kuhusu Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji yalishughulikiwa na kukamilishwa hatimaye wahusika kujulishwa. Kati ya malalamiko yaliyohusu Polisi, malalamiko 56 yamekwishapatiwa ufumbuzi na walalamikaji kuridhika na hatua zilizofikiwa. Malalamiko mengine 233 bado yanafanyiwa kazi. Malalamiko 875 hayakushughulikiwa kwa vile yanahusu kesi zilizopo Mahakamani au majalada yake kufikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa maamuzi ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Utawala. Maendeleo ya Watumishi na Mafunzo katika kipindi cha mwaka 2007/2008. Wizara ilikuwa na watumishi 58,234, kati ya hao watumishi 2,452 waliajiriwa kama ajira mpya na mbadala. Nafasi za ajira mbadala zilitokana na kustaafu, kufariki na kuacha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Watumishi 1,349 walipandishwa vyeo kwa utaratibu wa ushindani na watumishi 853 walithibitishwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 watumishi 582 wamestaafu, 272 wamefariki na watumishi 35 wameacha kazi kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ustawi wa Watumishi. Katika kuboresha ustawi wa watumishi wake uongozi wa Wizara umewawezesha watumishi kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa *(SACCOS)*. Hadi kufikia Mei, 2008 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilikuwa na matawi manne ya SACCOS yenye jumla ya Wananchama 16,473 ambapo Askari ni 16,201 na Watumishi raia 272. Wanachama hao wamekopeshwa jumla ya sh. 5,060,566,500 kwa lengo la kukidhi mahitaji ya kijamii na vilevile kutekeleza mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikopo ya Mabenki. Aidha Wizara imeingia mikataba na Benki mbalimbali inayowezesha watumishi kukopa fedha. Benki hizo ni NMB, Azania, Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam, Benki ya Posta, Benki ya Taifa ya Biashara na Benki ya *Barclays*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rushwa. Wizara yangu imedhamiria kuimarisha Utawala Bora pamoja na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa. Wizara imeshiriki kikamilifu katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kupambana na Rushwa (NACSAP). Aidha elimu kwa Umma imetolewa pamoja na semina na mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa Idara zilizo chini ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI. UKIMWI umekuwa janga na tishio kubwa kwa taifa letu kwani husababisha upotevu wa nguvu kazi kubwa. Katika jitihada za kupambana na janga hili, Wizara yangu katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 imeendelea kutekeleza mpango mkakati wa kudhibiti UKIMWI. Lengo la mkakati huo ni kuhakikisha kuwa Wizara inachukua hatua za kudhibiti kuenea kwa UKIMWI miongoni mwa wafanyakazi wake na wadau wengine. Aidha Wizara katika kupambana na janga hili imeendelea kutoa mafunzo kwa waelimishaji rika, washauri nasaha, kamati ya ushauri ya UKIMWI na watumishi wa ngazi zote. Vilevile Wizara imeendelea kutoa elimu na mafunzo kwa familia za watumishi (wake/waume) na wafungwa kuhusu janga hili. Hatua hii inalengo la kuhakikisha kuwa janga hili linapungua au hata kutokomezwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shabaha na Malengo kwa Mwaka 2008/2009. Baada ya kuelezea utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka uliopita, sasa naomba kuelezea shabaha na malengo kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua tatizo la ufinyu wa bajeti ya Serikali na hivyo kuifanya Wizara kutoweza kupata asilimia 100 ya mahitaji yake ya fedha, kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2008/09 Wizara imejipanga kutumia fursa na rasilimali zilizopo ndani yake kwa lengo la kutekeleza baadhi ya kazi wenyewe badala ya kutumia Wakandarasi nje ya Wizara. Tayari Wizara imeunda kikosi chake cha kazi kinachotayarisha utaratibu wa kutekeleza zoezi hilo kwa kuanzia na ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Jinsia, nalo tutalitilia mkazo katika maeneo yetu mbalimbali ya kazi. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa idadi ya Watumishi wanawake katika Utumishi wa Wizara inaongezeka kila wakati kulingana na majukumu na kazi zilizopo. Aidha uwiano huu wa Jinsia utazingatiwa pia katika masuala ya utoaji mafunzo, na upandishwaji vyeo. Kwa mfano katika mwaka wa fedha uliopita jumla ya askari na maafisa wa Polisi 5,372 wa ngazi mbali mbali wamepandishwa vyeo ambapo kati yao wanawake ni 1,085 hii ikiwa ni sawa na asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Polisi. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/09, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha mikakati ya kupambana na uhalifu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi. Katika kutekeleza jukumu hili Jeshi la Polisi lina malengo yafuatayo:-

(a) Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi na Sera ya Usalama wa Raia. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/09, Jeshi la Polisi litaendelea na mchakato wa maboresho katika utendaji kwa lengo la kuongeza ufanisi ili hatimaye malengo ya MKUKUTA kuhusu Utawala Bora yaweze kufikiwa. Programu hii imelenga kuboresha mbinu za kupambana na uhalifu, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi askari na vile vile kuboresha vitendea kazi na miundombinu ya kipolisi. Lengo la Jeshi la Polisi ni kuwa lenye kushirikisha wananchi, kufanya kazi kisasa na kuzingatia uweledi *(Professionalism)*. Kwa sasa hivi taratibu za kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri zinafanyika ili kuiarifu rasmi

Serikali juu ya programu hii ambayo ni mojawapo ya programu za maboresho katika sekta ya umma. Aidha, Wizara itaendeleza mchakato wa kukamilisha Sera ya Usalama wa Raia.

(b) Ujenzi wa Nyumba za Makazi

§ Kukamilisha ujenzi wa miradi ya nyumba za kuishi askari, Finya, Tunguu na Unguja Ukuu – Zanzibar. Tanzania Bara ni ujenzi wa makazi ya askari utakaokamilishwa Wilaya za Mwanga–Kilimanjaro na Bahi-Dodoma;

§ Kukamilisha Ujenzi wa nyumba ya kuishi Kondoa; na

§ Kuendeleza ujenzi wa nyumba kwenye Kambi ya Polisi Kilwa Road - Dar es Salaam, Ziwani - Unguja na Limbani-Kaskazini Pemba.

(c) Ujenzi wa Ofisi

§ Kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Dodoma na Mbeya;

§ Kukamilisha jengo la Ofisi ya FFU Dodoma na ujenzi wa Kituo cha Polisi Namtumbo;

§ Kukamilisha vituo vya Polisi vya Morogoro, Mpanda, Makambako, Ludewa, Newala, Bukombe, Meatu na Chato Tanzania Bara.

(d) Ujenzi na upanuzi wa vyuo

§ Kuanza ujenzi wa Chuo cha Upelelezi Dodoma; na

§ Kupanua Vyuo vya Polisi Moshi, Kidatu na Dar es Salaam.

(e) Ukarabati

§ Ukarabati wa nyumba za askari utafanyika katika kambi za Tunguu, Ziwani na Madunga –Zanzibar, Buguruni, Msasani na Tabata - Dar es salaam;

§ Kukarabati Bwalo la Maofisa wa Polisi Oysterbay, Maabara ya uchunguzi yaliyopo Makao Makuu ya Polisi na Ofisi za Makao Makuu ya FFU Ukonga - Dar es Salaam; na

§ Kukarabati ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kambi za Polisi – Mara na Mabatini – Mwanza.

(f) Ununuzi

§ Kununua sare za askari, vifaa vya ofisini kama tarakilishi *(computers)*, magari na vipuri vyake, mafuta na vilainishi vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha wa 2008/2009 tutaendelea kujenga tija kwa askari wa vyeo mbalimbali kwa kutoa mafunzo ili kuwapa uwezo na maarifa

katika utoaji huduma.  Baada ya mafunzo tunaamini kuwa askari watakuwa wakifanya kazi kwa matakwa ya mabadiliko ya kidunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kupanuka kwa sekta binafsi na shughuli za kiuchumi, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha Vikosi vyake Maalumu vya ulinzi wa migodi *(Mining Protection Unit)* na ulinzi wa Watalii *(Tourist Protection Unit)* kwa lengo la kuimarisha usalama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Magereza. Katika mwaka wa fedha 2008/09 Jeshi la Magereza litaendelea na mikakati ya kukabiliana na tatizo la msongamano magerezani, uharibifu wa mazingira, upatikanaji wa nyumba za kuishi askari pamoja na uimarishaji wa programu ya urekebishaji wa wafungwa kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Ajira

- Kuajiri askari wapya 1,215 watakaopatiwa mafunzo ya awali na pia watumishi 80 watapata mafunzo ya taaluma mbalimbali nje ya Jeshi la Magereza.

(b) Mradi

- Jeshi la Magereza litaendelea na mradi wa Offenders *Management Information System (OMIS)*.

(b) Ukarabati

- Kuendelea na ukarabati, ukamilishaji na ujenzi wa mabweni ya wafungwa, ofisi za magereza, nyumba za askari, mifumo ya maji taka na maji safi katika magereza 25 yaliyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tabora, Lindi, Arusha, Kagera, Mbeya, Manyara, Ruvuma na Rukwa.

- Kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu ya magereza yenye ulinzi mkali ya Isanga maalum - Dodoma, Gereza Isanga – Dodoma, Ukonga-Dar es Salaam, Lilungu- Mtwara na Karanga-Kilimanjaro.

(d) Upimaji na Fidia

- Kuendelea na upimaji wa maeneo ya magereza na ulipaji wa fidia katika magereza 5 yaliyopo katika mikoa ya Rukwa, Pwani na Kilimanjaro.

(b) Mazingira

- Kuendeleza utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti katika magereza ya Idete, Isupilo na Msalato kwa fedha za msaada zilizotolewa na NORAD kwa ushirikiano na Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na kupanda miti katika magereza 11 yaliyopo katika mikoa ya Mwanza, Singida, Kigoma, Iringa, Ruvuma, Shinyanga, Rukwa, Kilimanjaro na Mbeya.

(f) Ununuzi

- Kununua majiko yanayotumia makaa ya mawe ili yatumike katika magereza yaliyopo katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ili kuepukana na matumizi makubwa ya kuni.

- Kununua magari 64 ya aina mbalimbali kwa ajili ya kupunguza tatizo la usafiri magerezani. Kama sehemu ya upanuzi wa mradi wa kusafirisha mahabusu, Jeshi la Magereza litanunua magari 9 kwa ajili ya kusafirisha mahabusu kwenda na kurudi mahakamani katika mikoa ya Pwani na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza litaendeleza mikakati ya kuimarisha na kuboresha utendaji kazi katika Shirika la Magereza. Kazi hizo ni pamoja na kununua vitendea kazi na zana za kilimo kwa ajili ya kuimarisha kazi za uzalishaji ndani ya Shirika la Magereza. Pamoja na mikakati hiyo, hatua zitachukuliwa za kuingiza kikosi Ujenzi cha Magereza kwenye miradi ya Shirika. Kuingizwa kwa mradi wa kikosi cha Ujenzi katika Shirika la Magereza kutawezesha Shirika la Magereza kufanya kazi za Ukandarasi wa miradi yote ya ujenzi ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hatua hii itasaidia kupunguza gharama za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu kwa Umma itaendelea kutolewa kupitia kipindi cha “Ijue Magereza” kinachorushwa na Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kila wiki. Aidha, gazeti la Sauti ya Magereza, vipeperushi vya Mkataba wa Huduma kwa Mteja vitaendelea kuchapishwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kusambazwa kwenye vituo vyote vya Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Wakimbizi. Kutokana na kuendelea kuimarika kwa amani nchini Burundi na kwenye maeneo mengi ya jimbo la Kivu Kusini katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), pia kuwepo kwa Makubaliano ya pande tatu *(Tripartite Agreement)* yanayohusisha Tanzania, DRC na UNHCR tunatarajia kuwa kasi ya urejeaji kwao Wakimbizi kwa hiari itaongezeka. Tunatarajia kuwa ifikapo mwezi Desemba, 2008 kambi zote za wakimbizi katika Mikoa ya Kigoma na Kagera zitakuwa zimefungwa. Aidha, kutokana na kuendelea vema kwa zoezi la kuwarejesha kwao wakimbizi kutoka Makazi ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu, na mchakato wa kuwapa uraia wakimbizi wengine walioomba uraia wa Tanzania toka makazi hayo; ni imani yetu kuwa makazi haya nayo yanaweza kufungwa ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa awamu ya kwanza ya Mradi wa Kukabiliana na Athari za Wakimbizi 2003-2006 katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Ngara, Mkoani Kagera unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark umekamilika. Awamu ya pili ya mradi 2006-2009 inaendelea. Katika awamu hii ya mradi, Serikali ya Denmark imekubali kuufadhili kwa gharama ya Danish Kronor Milioni 60 sawa na shilingi za Tanzania Bilioni 14.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea kuishawishi Jumuiya ya Kimataifa kusaidia katika maeneo yaliyoathiriwa na ujio wa wakimbizi hususan katika nyanja za hifadhi ya mazingira, ukarabati wa miundombinu, ujenzi na ukarabati wa zahanati, maji, shule na sekta nyingine za kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma kwa Jamii. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Wizara yangu inatarajia kuongeza mikoa mingine mitatu ya Morogoro, Pwani na

Lindi katika utekelezaji wa Programu ya Huduma kwa Jamii.  Hivyo kufanya mikoa inayotekeleza sheria ya Huduma kwa Jamii Na.6/2002 kufikia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika,  Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tumeanza kulishughulikia tatizo la uhaba wa watendaji kwa kuboresha muundo wa Idara hii, ambapo sasa tunatarajia kuwa na watumishi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ambao watawajibika moja kwa moja kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.  Aidha, Idara hii zaidi ya kusimamia wafungwa wa Huduma kwa Jamii, itashughulikia pia wafungwa walioachiwa chini ya Sheria ya Bodi za Parole, adhabu za kifungo cha nje pamoja na Sheria ya Huduma ya *"Probation" (Probation of Offenders Act, Cap. 247, R.E 2002).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Zimamoto na Uokoaji. Ili kuboresha na kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokoaji nchini, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litafanya yafuatayo:-

(a) Sheria ya Zimamoto na Uokoaji

- Kuanza utekelezaji wa sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na.14 ya mwaka 2007 na Kanuni zake chini ya utaratibu wa Komandi moja.

(b) Mafunzo kwa Askari wa Zimamoto na Uokoaji kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

- Ni azma ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kujizatiti katika kutoa mafunzo ya kisasa ya kuzima moto na uokoaji na pia mafunzo ya uaskari ili kujenga Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lenye Nidhamu na Ufanisi katika majukumu ya kuokoa maisha na mali.  Askari 300 watapewa mafunzo hayo.

(b) Mafunzo kwa Umma

- Kazi ya kuelimisha umma juu ya Tahadhari na Kinga za Moto na athari zake, itatolewa kwa watumishi wa Serikali kwenye Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Makampuni, shule n.k.  Elimu hiyo itatolewa kupitia sehemu za kazi na katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Dar es Salaam.  Vilevile kwa njia ya majarida na vipeperushi.

(b) Ununuzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu

- Katika mwaka huu wa fedha 2008/09 Wizara imepanga kununua jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

(c) Vitendea Kazi

- Ununuzi wa vitendea kazi ili kuimarisha utendaji wa kazi kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji utafanywa kwa kununua magari, sare za askari wa Zimamoto na Uokoaji na vitendea kazi vingine yakiwemo madawa ya kuzimamoto na vifaa vya kinga kwa mzimamoto

(d) Ukaguzi wa Tahadhari za Moto

- Kuendelea kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye maeneo mbalimbali.

(e) Ajira

- Kuajiri askari wapya 6. Kwa ngazi ya *Assistant Inspector*. Askari hao ni Wahitimu wa shahada ya Chuo Kikuu. Lengo baada ya kupatiwa mafunzo ya uaskari wa Zimamoto na Uokoaji wataongeza nguvu katika masuala ya kiutendaji na kiutumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Uhamiaji. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Idara ya Uhamiaji itafanya yafuatayo kwa lengo la kuimarisha uwezo wa idara kiutendaji ikiwa ni pamoja na kutoa huduma bora kwa raia na wageni na kudhibiti mipaka.

a) Misako

- Kufanya misako na doria ili kupambana na wahamiaji haramu.

b) Kuajiri na Mafunzo

- Kuajiri Askari wa Uhamiaji wapya 134 na kuwapeleka watumishi 140 kwenye kozi mbalimbali za kujiendeleza za muda mrefu na mfupi ili kujenga uwezo na kutoa huduma bora.

c) Kuchapisha

- Kuchapisha nyaraka mbalimbali zinazowezesha kutoa huduma za uhamiaji mwaka mzima.

d) Elimu

- Kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma za Uhamiaji kwa lengo la kutoa huduma bora kwa umma wa Tanzania.; Kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara yanayotokana na wananchi kuwahifadhi au kuwalinda wahamiaji haramu ili kuweza kupunguza tatizo la ongezeko la wahamiaji haramu nchini.

e) Ujenzi wa nyumba za kuishi na Ofisi

- Ili kupata ofisi zenye hadhi na nyumba bora za makazi, idara ya Uhamiaji itaedelea na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam, upanuzi wa Ofisi Kuu Zanzibar na nyumba za Askari wa Uhamiaji Mikoa ya Arusha na Manyara.

- Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza jukumu la kudhibiti mipaka, idara itajenga kituo cha Uhamiaji Muhukuru – Songea Vijijini katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

f) Kukarabati nyumba za kuishi na Ofisi

- Kukarabati Ofisi za Uhamiaji na nyumba za makazi ya watumishi katika vituo vya kuingilia nchini kwa lengo la kuboresha ofisi na makazi ya watumishi

g) Ununuzi

- Kununua magari nane (8) ili kuwa na uwezo zaidi wa kufanya misako na doria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vitambulisho vya Kitaifa. Mradi wa Vitambulisho vya Kitaifa katika mwaka wa fedha wa 2008/09 Wizara yangu inatarajia kumpata mkandarasi atakayesimika mtandao wa ukusanyaji wa takwimu (data) za watu kutoka sehemu mbalimbali nchini. Zoezi hili litaenda sambamba na kuelimisha umma juu ya umuhimu wa vitambulisho, kuanzisha Ofisi za Usajili za Wilaya na kutoa mafunzo kwa watendaji watakao husika na zoezi zima la usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Kusajili Vyama vya Kijamii. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Kijamii itafanya yafuatayo:-

- Kuelimisha vyama vilivyoandikishwa kuhusu wajibu wao kwa mujibu wa Sheria;

- Kushughulikia migogoro ya Vyama vilivyoandikishwa;

- Kuhakiki utendaji na uhai wa Vyama; na

- Kuimarisha na kuboresha utendaji wa Ofisi ya Usajili kwa kununua samani za ofisi na vitendea kazi vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za kushughulikia Malalamiko; ili kuimarisha utendaji katika Idara ya kushughulikia malalamiko katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/09, Idara imejiwekea malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kushughulikia malalamiko kwa ufanisi; na

- Kuelimisha umma juu ya haki na wajibu wao, mgawanyo wa kazi na utendaji wa vyombo vilivyoko chini ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Utawala. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Idara ya Utawala itafanya yafuatayo:-

- Kuendeleza vita dhidi ya Rushwa;

- Kuendeleza vita dhidi ya UKIMWI; na

- Kutekeleza mpango wa mafunzo ambao umelenga kuboresha utendaji kazi wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Balozi Khamis Suedi Kagasheki Mbunge wa Bukoba Mjini, Katibu Mkuu Bwana Mohamed Said Muya, Wakuu wa Idara, Makamanda wote, askari pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao kwa ushirikiano wao wamewezesha hotuba hii kuandaliwa na kukamilika katika wakati unaotakiwa. Aidha, napenda kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu

wa Serikali Bwana Cassian Chibogoyo na Wasaidizi wake kwa kufanikisha uchapishaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani za pekee kwa nchi wahisani za China, Canada, Sweden, Denmark, Belgium na Uholanzi. Aidha shukrani zangu iziendelee taasisi za kimataifa za *UNDP, World Bank, NORAD, UNAFRI, WFP, IOM, UNHCR* na *INTERPOL* ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2008/2009. Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liwezeshe Wizara yangu kutekeleza hayo yote niliyoyaeleza kwa kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya jumla ya Shilingi 273,976,585,500 kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 kama ifuatavyo:-

**Fungu 14: Zimamoto na Uokoaji**

| | | |
|---|---|---|
| Mishahara | 645,445,000 | |
| Matumizi Mengineyo | 3,000,000,000 | |
| Matumizi ya Maendeleo | 3,000,000,000 | |
| **JUMLA** | | **6,645,445,000** |

**Fungu 28: POLISI**

| | | |
|---|---|---|
| Mishahara | 65,538,848,000 | |
| Matumizi Mengineyo | 75,013,260,000 | |
| Matumizi ya Maendeleo | 9,963,955,000 | |
| **JUMLA** | | **150,516,063,000** |

**Fungu 29: Magereza**

| | | |
|---|---|---|
| Mishahara | 30,430,513,000 | |
| Matumizi Mengineyo | 40,303,529,000 | |
| Matumizi ya Maendeleo | 5,881,000,000 | |
| **JUMLA** | | **76,615,042,000** |

**Fungu 51: Utawala**

| | | |
|---|---|---|
| Mishahara | 1,274,961,000 | |
| Matumizi Mengineyo | 3,637,182,000 | |
| Matumizi ya Maendeleo | 6,555,853,500 | |
| **JUMLA** | | **11,467,996,500** |

**Fungu 93: Uhamiaji**

| | |
|---|---|
| Mishahara | 8,175,514,000 |
| Matumizi Mengineyo | 9,403,212,000 |

| | |
|---|---|
| Matumizi ya Maendeleo | 11,153,313,000 |
| **JUMLA** | **28,732,039,000** |

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyoshughulia Wizara hii.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zambi, Mwongozo!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu 68(7), Kifungu cha 151, kinahusu salamu za pongezi na pole. Najua wote tunapopata matatizo, tunaguswa sana na mambo haya na kila mtu angependa anaposimama atoe pongezi zake au rambirambi zake lakini Kanuni hiyo niliyoitaja, inatuzuia kufanya hivyo. Kwa sababu Kanuni tumeitunga sisi wenyewe na tunaendelea kuivunja sisi wenyewe, naomba utoe mwongozo wako, kama tunaona pengine ni kipingamizi tuifute ili isiwepo, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Anachosema Mheshimiwa Zambi ni kweli. Kwa mujibu wa kifungu hiki, salamu za rambirambi na pole kwa familia ya mwenzetu aliyeondoka, zimeshatolewa na Mheshimiwa Spika na pia Serikalini anatoa Waziri Mkuu, kwa hiyo, hatutumii muda mwingi kusema haya tunayoyasema kwa sababu ni dhahiri wote tulishiriki pamoja kutoa salamu za rambirambi kwa familia na ndugu na marafiki wa marehemu. Kwa hiyo, kifungu hicho kinasema hivyo. Si mategemeo yetu kuanza kusikiliza mtu anasema naanza kutoa salamu za rambirambi halafu Spika anamsimamisha, haitakuwa vizuri. Afadhali msiseme ili kusudi tusiingie katika majaribu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. WILSON M. MASILINGI – MWENYEKITI, KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii, kabla sijaanza kuisoma taarifa hii ya Kamati, nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na leo nimesimama mbele yako kuweza kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Iramba Magharibi, kwa kuwa nami kwa muda wote na kunipa ushirikiano wa masuala muhimu ya kimaendeleo katika kuliendeleza Jimbo letu la Iramba Magharibi. Nathamini sana kiwango cha ushirikiano wanachonipa wananchi wa Jimbo langu katika kutekeleza wajibu wangu wa Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nichukue nafasi hii, nimshukuru sana mke wangu Hajra, pamoja na wanangu Sitti, Latifa, Faisal na Fahd, kwa kunipa ushirikiano na kunitia

moyo muda wote hasa ninapokuwa nafanya shughuli hizi za kuwawakilisha wananchi wa Jimbo langu la Iramba Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, nitoe taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika mwaka wa fedha 2007/2008 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni Na. 99 (7), Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili maoni ya Kamati na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya majukumu ya Kamati hii, ni kuchambua Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, tarehe 2 Juni, 2008 na tarehe 3 Juni 2008, Kamati ilifanya Kikao na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Jijini Dar es Salaam. Katika Kikao hicho, Kamati ilipata maelezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Mapendekezo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. Aidha, tarehe 24/6/2008, Kamati ilifanya tena kikao na Wizara kwa mara ya pili ili kupata maelezo zaidi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi na kazi zilizopangwa kufanywa kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2006/2007 na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa 2007/2008, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, wakati huo ilitoa Ushauri na mapendekezo kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Ushauri huo ulihusu Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Utawala kwa ujumla. Taarifa ya Wizara ilionyesha kuwa, sehemu kubwa ya ushauri bado ipo kwenye mchakato wa kutekelezwa. Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, inaendelea kushauri kuwa ushauri uliotolewa mwaka 2007/2008 ambao bado upo kwenye mchakato, uzingatiwe na kutekelezwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuelezwa juu ya utekelezaji wa maoni ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa mwaka wa fedha uliopita, vile vile tulielezwa kuwa makusanyo ya maduhuli hadi Aprili, 2008, yalivuka lengo kwa asilimia mbili. Sambamba na maelezo hayo, Kamati pia iliarifiwa kuwa hapakuwepo na tatizo la mtiririko wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Hata hivyo, tatizo lililokuwepo ni ufinyu wa bajeti hususan kwa matumizi mengineyo na yale ya maendeleo (*development expenditure*). Hali hii, ilikuwa ni changamoto kubwa kwa Wizara hii katika kipindi cha mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa Wizara kwa mwaka 2008/2009, Kamati ilielezwa juu ya mpango wa Serikali kuwapatia Askari makazi (*barracks*). Aidha, tatizo la usafiri kutoka makazi ya Askari hadi kazini kwao linaendelea kushughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika Vilevile, Kamati ilielezwa kuwa, azma ya Serikali katika eneo la wakimbizi bado ni tete kwa kuwa pamoja na kuongeza juhudi za kuwarejesha

wakimbizi makwao, nchi wanapotoka wakimbizi hao huzusha tena mapigano kati yao jambo ambalo huwafanya wakimbizi wasite kufuata ratiba yao ya kurejeshwa makwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Kamati ilielezwa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kama ifuatavyo:-

1. Kuimarisha Jeshi la Polisi kwa ajili ya ulinzi wa raia na mali zao;

2. Upatikaji wa vitendea kazi vya kisasa;

3. Mafunzo ya Kisasa na yenye taaluma maalum;

4. Kuimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

5. Kuboresha huduma ya Uhamiaji;

6. Kuendeleza Mpango wa Serikali kuwapatia Askari makazi *(barraks)*;

7. Kupanua na kuimarisha miundombinu ya Magereza;

8. Usafirishaji wa wafungwa na mahabusu kwenda na kurudi kutoka Mahakamani;

9. Urekebishaji wafungwa kupitia uzoefu wa kazi viwandani na kwenye Kilimo; na

10. Kuimarisha utendaji katika Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imeomba jumla ya Sh.273,976,585,500/= (Bilioni mia mbili sabini na tatu, mia tisa sabini na sita milioni, laki tano na elfu themanini na tano na mia tano). Kati ya hizo Sh.36,554,121,500/= (Bilioni thelathini na sita, mia tano na hamsini na nne milioni, laki moja na elfu ishirini na moja na mia tano), ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Shilingi 237,422,464,000/= (Bilioni Mia mbili na Thelathini na Saba, milioni mianne Ishirini na mbili, laki nne na sitini na nne elfu), zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kamati ilijadili kwa undani Taarifa ya Utekelezaji na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na kuunga mkono Maombi ya Wizara hii. Hata hivyo, Kamati ilitoa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa kuzingatia Dira ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na majukumu ya Wizara hiyo, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kwa mafungu matano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi, Kutokana na taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi nchini, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatia matukio ya mara kwa mara ya ujambazi na utekaji magari na mauaji ya Albino Kanda ya Ziwa, uandaliwe mpango maalumu wa ulinzi kukomesha hali hiyo;

(b) Serikali iendelee kuliwezesha kibajeti Jeshi la Polisi nchini ili liwe na mafunzo bora zaidi sambamba na kuendelea kulipatia vitendea kazi na zana za kisasa;

(c) Serikali iliwezeshe Jeshi la Polisi, Kikosi cha Wanamaji (*Police Marine*) ili kiongeze ufanisi katika Ulinzi kwenye maziwa na bahari;

(d) Serikali iwe na mpango wa kujenga Hospitali ya Rufaa kwa Jeshi la Polisi nchini ili kusaidia huduma bora ya afya kwa Askari;

(e) Serikali iendelee na juhudi zake za kuboresha makazi ya Askari Polisi kwa kuandaa mpango maalum wa kushughulikia suala hili ili kulinda hadhi ya Jeshi la Polisi nchini;

(f) Serikali ifuatilie malalamiko ya wananchi dhidi ya Makamanda na Askari Polisi wachache wala rushwa na kuchukua hatua haraka ili kuimarisha imani ya Raia wema kwa Jeshi la Polisi; na

(g) Kamati iliridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi kuboresha ulinzi na kushauri kuwa elimu kuhusu maboresho ya Jeshi la Polisi hususan katika Ulinzi Shirikishi (Polisi Jamii), itolewe kwa viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla ili kufanikisha malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza, kutokana na taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Magereza, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Serekali iongeze kasi katika kutatua tatizo la makazi ya Askari Magereza;

(b) Jeshi la Magereza liendelee kuboreshwa kibajeti ili liweze kumudu vema majukumu yake ya msingi na kuwa na ufanisi kiutendaji;

(c) Kikosi cha Ujenzi cha Magereza kiruhusiwe kutekeleza miradi ya ujenzi bila masharti ya kibali kupitia zabuni ili kupunguza gharama za ujenzi; na

(d) Jeshi la Magereza liwezeshwe kifedha kupitia Mpango wa Kitaifa wa Kuendeleza Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme – ASDP)* ili kutumia vyema nguvukazi na utaalamu wa Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhamiaji**,** kuhusu Idara ya Uhamiaji Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Serikali iimarishe vituo vya Uhamiaji vilivyopo na kuanzisha vingine katika mipaka yetu hasa katika maeneo yaliyokithiri kwa njia zisizo rasmi (Njia za panya);

(b) Serikali iiwezeshe Idara ya Uhamiaji kibajeti ili iweze kudhibiti wahamiaji haramu ambao wanaongezeka sana; na

(c) Idara ya Uhamiaji iimarishe taratibu zake za kuandaa hati za kusafiria ili mafanikio yaliyopatikana dhidi ya rushwa yawe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimatomo na Uokoaji, kuhusu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, imeanza kutekelezwa tarehe 1 Juni, 2008, utaratibu wa kuhamisha vyombo vya Zima moto na uokoaji kutoka Serikali za Mitaa kwenda Jeshi hilo utekelezwe haraka;

(b) Mafunzo ya Zimamoto na Uokoaji yapewe uzito unaostaili ili kuwa na watendaji wenye uwezo wa kutekeleza vema majukumu yao;

(c) Ili kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lijengewe ofisi ya Makao Makuu badala ya kupanga; na

(d) Serikali iongeze juhudi ya kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendea kazi bora na vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa jumla. Pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati katika maeneo niliyoyataja, vile vile Kamati inashauri kuwa Hazina ichukue madeni yote ya Wizara hii na kuyalipa haraka. Aidha, Serikali iandae utaratibu utakaoyawezesha Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini kuwa na Tume ya Utumishi inayojitegemea kwa kila Jeshi. Tume ya Utumishi inayojitegemea, itawezesha Majeshi yetu kuajiri, kupandisha vyeo na mambo mengine ya kiutumishi pasipo kuathiriwa na urasimu wa kiraia. Aidha, maslahi ya Askari wetu yaendelee kuboreshwa ili kuimarisha morali ya Askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzipatia motisha Idara zinazokusanya maduhuli, Hazina isipunguze bajeti za Idara hizo kadri ya Sehemu ya Maduhuli inayobakishwa (*Retention*) Wizarani. Maduhuli yanayobakishwa (*Retention*) iwe ni nyongeza kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho**.** Nachukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, nawashukuru sana Mheshimiwa Laurence K. Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Balozi Khamisi S. Kagasheki, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa uchapaji kazi unaoridhisha na ushirikiano kwa Kamati yangu. Kadhalika, nawashukuru Bwana Mohammed Said Muya, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Inspekta Jenerali Saidi Mwema, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, Kamishna Augostino Nanyaro, Mkuu wa Jeshi la Magereza Nchini, Ndugu Kinemo Kihomano, Mkurugenzi Mkuu wa Uhamiaji, Kamishna Msaidizi Mohammed Kapamba, Kaimu Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na watendaji wengine wa Wizara hii kwa kazi nzuri na ufafanuzi walioutoa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao na kwa kufanya uchambuzi wa kina ulioiwezesha hoja hii kufikia hatua iliyopo sasa. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mwenyekiti, Mheshimiwa Musa A. Zungu, M/Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohammedi Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A.Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N.Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dkt.John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col.Mst. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mheshimiwa Dkt.Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brg.Jen. Mst.Hassan A. Ngwilizi,

Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, lakini si kwa umuhimu, napenda pia kuwashukuru Dkt. Thomas D. Kashililillah, Kaimu Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa. Bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Neema Kiula kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA - MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweka kumbukumbu sawa, kwanza napenda niseme kwamba hii hotuba ni ya Kambi ya Upinzani na msemaji wake ni Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, yeye mwenyewe yupo safarini na wala mimi siyo Naibu wake, naisoma kwa niaba ya Kambi ya Upinzani.

**NAIBU SPIKA:** Nadhani ndivyo tulivyosema sisi, kwamba Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Sawasawa.

**NAIBU SPIKA:** Sawa endelea.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA - MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Awali ya yote, tunapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa tukiwa wazima wa afya na kujadili mambo muhimu yanayogusa maslahi ya umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama changu cha Wananchi (CUF) na wapiga kura wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe Zanzibar kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia katika kuhakikisha kuwa ninatekeleza majukumu yangu kama Mbunge ipasavyo na kwa umahiri mkubwa ili kutimiza malengo na sera za Chama chetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naushukuru pia uongozi wa Kambi ya Upinzani chini ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Slaa, kwa mchango wao mkubwa katika maandalizi ya hotuba hii. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni wajumbe wa Kamati ya Mambo ya nje, Ulinzi na

Usalama, kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa katika kutimiza wajibu wangu kama Waziri Kivuli wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Masha pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki, kwa ushirikiano wao. Sambamba na hilo, nawapongeza Viongozi wakuu wa Jeshi la Polisi kwa jitihada zao katika kukabiliana na uhalifu licha ya hali ngumu kiutendaji wanayokabiliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunawashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wote wa uhamiaji pamoja na Jeshi la Magereza katika kutekeleza kazi zao vyema bila ya kujali muda na hali ngumu ya maisha inayowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kutoa na kuomba ufafanuzi kwa masuala mbalimbali ili kuinua utendaji kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama nchini, inaonekana Tanzania si shwari tena, kwani ni hivi karibuni tu kumejitokeza hali inayoashiria baadhi ya watu kujilimbikizia mali isivyo halali. Hali hii, italipelekea Taifa letu kutoaminiwa na hata wawekezaji pamoja na raia wavuja jasho kutoiamini tena Serikali yao kutokana na mali zao kuvushwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalitaka Jeshi la Polisi kufanya kazi zake kisayansi kwa hali ya juu kabisa ili wale watakaobainika na dhambi hizi wafikishwe katika vyombo vya sheria nchini. Hii ndiyo njia ya kurejesha imani kwa raia na kuona kwamba Serikali yao iko makini katika kulinda haki zao pamoja na rasilimali za nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na mauaji yanayofanywa kwa makundi maalumu ya watu huku Serikali ikionekana kushindwa kabisa kutokomeza mauaji hayo. Tunaitaka Serikali kutoa takwimu sahihi hadi sasa ni vifo vingapi vimekwisha tokea, tangu wimbi la mauaji ya Maalbino yaanze kujitokeza katika Mikoa mbalimbali hapa nchini na ni mkakati gani mahsusi ya kulilinda kundi hili la Watanzania walio na haki ya kuishi kwa furaha na matarajio kama walivyo Watanzania na binadamu wote wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaelewa kuwa taratibu mahali pengi duniani ambapo heshima na haki za binadamu zinathaminiwa, Askari wanakuwa na mipaka katika kutekeleza majukumu yao. Mfano, Askari hawatakiwi kumpekuwa raia zaidi ya saa kumi na mbili jioni. Kwa msingi huo, napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili, ni mamlaka yapi yaliyotumika kuwavamia wakazi saba wa Pemba zaidi ya saa saba za usiku, waliojiita Askari, walifanya fujo, wakatishia hata kuvunja milango ya nyumba za hao waliowaita watuhumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inauliza je, huu si uvunjaji wa haki za raia na kwenda kinyume na matakwa ya Umoja wa Mataifa wa kuheshimu haki za binadamu na za raia?

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazolikabili Jeshi La Polisi, ni jambo la kusikitisha kwamba chombo muhimu kama Jeshi la Polisi linakabiliwa na matatizo makubwa yanayolizuia kufanya kazi kwa ufanisi na huku Serikali ikiyafumbia macho mambo haya. Kambi ya Upinzani, inasema hayo kwa kufanya marejeo ya taarifa ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini inayosomeka kama '*Challenges Of Enhancing Performance and Responsiveness in the*

*Police Force'* kama alivyoitoa tarehe 18 Juni, 2008. Taarifa hiyo iliainisha yafuatayo ambayo tunaitaka Serikali iyashughulikie kwa kuyapa kipaumbele na kuyatatua:-

(1) Ukosefu wa rasilimali watu za kutosha;

(2) Muundo wa kitaasisi usio wa kiufanisi katika Jeshi la Polisi;

(3) Mfumo duni wa habari na mawasiliano; na

(4)Vyanzo vya mapato na fedha visivyotosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inasikitisha iwapo kweli tunakusudia kuwa na Jeshi la Polisi, ambalo tunalitaka litulinde katika uhalisia wake. Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kwamba ni lazima zichukuliwe juhudi za makusudi ili kuboresha hali mbaya ya Jeshi hilo kwa kuangalia undani wa matatizo hayo, chimbuko lake ni moja tu, nalo ni kuwa kasma ni ndogo. Kambi ya Upinzani, inasema ni kwa nini Jeshi la Polisi nalo lisitengewa kasma kama ambavyo wanatengewa usalama wa Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaona hiki kinaweza kuwa ni chanzo kikuu cha malalamiko toka kwa wananchi kuwa utendaji wa Jeshi la Polisi huko chini na usiofuata maadili yao ya kazi. Askari ni binadamu kama wengine, hivyo kutowawezesha vizuri kwa kadri ya kukidhi mahitaji ya msingi ya familia zao kunasababisha Askari hao kuingia kwenye vishawishi vya kukiuka maadili ya viapo vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli wa mambo ni kwamba Askari wote wa Jeshi la Polisi, ni wenye nidhamu ya hali ya juu kabisa katika utendaji wao, ila tu kilichokosekana ni haki zao za msingi kutopatikana kutokana na uzito wa kazi zao. Naomba ieleweke kwamba njaa ndiyo iliyokosa nidhamu kwani ikianza kutokota basi kinachofuatia ni Askari hawa kuanza kufanya mahesabu ya wapi apenye ili kutuliza tumbo lake. Huo ndio mwanzo wa rushwa. Hivyo ni jambo la busara mishahara na posho zao zipandishwe ili ziendane na hali ya maisha ilivyo na zitolewe katika muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaeleweka vyema kwamba kazi hii haihitaji muda wa mapumziko, kwani zile siku ambazo raia au hata wafanyakazi wanapopata mapumziko au kusherehekea sikukuu mbalimbali nchini Askari yeye huwa ndiyo wakati wake mgumu wa kuhakikisha kwamba kila kitu kinakwenda vizuri na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari kukosa sare angalau mbili kila mmoja, ni kasoro kubwa katika Jeshi hili, hivi Askari atakapoamua kufua sare yake na bahati nzuri ikanyesha mvua na tena bahati mbaya akahitajika ghafla kituoni atakwenda akiwa kavaa nini? Serikali iliangalie sana suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza hata hao ambao huwa wanatoa sare na vifaa vyingine kwa njia halali za zabuni, wanadai mabilioni ya shilingi na bado hawajafikiriwa kulipwa. Hivi ni uhakiki gani au uchunguzi gani wa madeni hayo usiokwisha? Mdaiwa anapokuwa hodari wa kulipa basi hutoa nafasi nzuri ya kukopeshwa tena. Tusiogope kukopa kwani bado ni maskini lakini vile vile tuwe mahodari wa kulipa kwani hao wakopeshaji hutumia mikopo ya benki na wanapocheleweshwa malipo yao mwishowe hujikuta badala ya faida wamepata hasara na hii inatokana na kiwango cha riba kuzidi kupanda kutoka katika mabenki waliyokopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Ulinzi Jamii/Shirikishi, mpango huu si mpya hapa Tanzania. Pamoja na kuwa haukuwepo kisheria na wala haukuwekewa utaratibu mzuri, utaratibu wa Sungusungu umekuwepo katika nchi yetu kwa muda mrefu. Wananchi katika maeneo yao waliwekeana utaratibu wa kujilinda wao na mali zao.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza Watanzania ni sababu gani za msingi zilizosababisha mpango huo wa Sungusungu kutowekewa utaratibu mzuri na wa kisheria kuliko unavyoendelea hivi sasa katika maeneo mengi lakini hauratibiwi rasmi na Sheria. Jamii ingetakiwa kupewa mafunzo ya awali, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya matumizi ya Silaha. Uwepo wa Sungusungu ungewekwa kisheria tofauti na ilivyokuwa ikifanya kazi. Matumizi haya si mageni sana duniani kwani hata nchi zilizoendelea kama Uswisi, Marekani ambapo ulinzi jamii wanaita "*citizen on patrol- cop*" wanatoa mafunzo ya kiulinzi na usalama kwa kila raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Polisi Jamii na au Sungusungu uliigwa kutoka katika nchi mbalimbali duniani kama vile Uingereza na Marekani. Hata hivyo, mpango huu katika nchi hizo umeshindikana kutekelezwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya ongezeko kubwa la idadi ya watu, maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia. Hizi ni sababu ambazo kwa Tanzania hazihitaji kutafutwa ziko wazi na ni wazi kuwa mpango huu unatakiwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na kujua sababu za kufanikiwa na kufa kwa mpango huu wa SUNGUSUNGU.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jeshi la Polisi liliamua kuanzisha Kanda Maalum ili kuwezesha utendaji wenye ufanisi. Pamoja na lengo hili, Serikali haionekani kulitia maanani jambo hili kwani inashangaza kuona kwamba katika mwaka huu wa fedha kanda hii haikutengewa fedha zikiwemo za mafuta ya magari, je, kanda hii itafanyaje kazi? Hii ni sawa na kuweka sufuria katika jifya lisilo na moto, chakula kitaivaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaona hali hii ndio chanzo kinachopelekea baadhi ya Polisi kuwadai wananchi fedha kwa ajili ya kufuatilia matukio ya uhalifu wakati wanapopewa taarifa za kutokea kwa matukio hayo. Hivyo basi, tunajiuliza kama hali ndio hiyo, uhalifu kweli utakwisha katika Mkoa wa Dar es Salaam?

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kujiendeleza kimasomo kwa Askari Polisi, ni wazi kuwa hii ni karne ya sayansi na teknolojia na ili mtu apate ufanisi katika utendaji wa kazi yoyote anayoifanya, kuna haja ya kuwa na elimu inayoendana na wakati. Pamoja na ukweli huu, Jeshi la Polisi linaonekana halithamini mpango huu, kwa sababu suala la kutoa ruhusa kwa watendaji wake hasa wa ngazi za chini kujiendeleza kimasomo linaonekana kuwa ni gumu sana. Katika hili, nitafanya marejeo kwenye barua ya wazi iliyoandikwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika Gazeti la Nipashe toleo la Jumamosi, tarehe 5 july 2008, naomba ninukuu sehemu ya barua hiyo ambayo inasema:-

*"Sisi kama Askari Polisi, hatuwezi kamwe kuendana na hali hii ya dunia kuwa kama kijiji bila ya kuwa na elimu ya kutosha ili kuweza kuwiana na majeshi mengine duniani. Hili tunalieleza wazi kwako ili ufahamu ukiritimba tunaofanyiwa sisi wanao (Askari Polisi) kwani kulingana na mkataba wa kufanya kazi na kulingana na Police General Order(PGO), kuwa unapoanza kazi, utafanya kazi kwa muda wa miaka mitatu ndipo uruhusiwe kwenda kujiendeleza kimasomo kwa yule anayehitaji.*

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko haya yamesikika pia kila kona ya nchi kutoka kwa Askari wa ngazi za chini. Kama hali hii ipo kweli, basi ni jambo la kusikitisha kwani Jeshi letu la Polisi kwa kawaida linaajiri vijana wengi waliomaliza Kidato cha Nne na kama hawapewi nafasi ya kujiendeleza tutakua na Jeshi la Polisi lililo bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hali hii ipo na kwa kuwa Jeshi letu la Polisi mara nyingi huajiri vijana wengi waliohitimu elimu ya Kidato cha Nne, je, tutaweza kuwa na Askari wenye vigezo na umahiri wa kushiriki katika harakati za Kijeshi kama *Interpol* na nyinginezo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kwenda sambamba na maendeleo ya kitaaluma kwa sasa, kambi ya Upinzani, inashauri kuwa utaratibu mahsusi uandaliwe utakaowawezesha Askari Polisi kujiendeleza katika taaluma za kawaida, kwa wale wachache au hata wengi watakaotaka kujiendeleza kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kupandisha vyeo, kulingana na taratibu za kazi za Jeshi la Polisi, *PGO* na *Police Force Service Regulations,* kupandishwa cheo au vyeo, ni haki ya kila Askari kwa mujibu wa Kanuni hiyo. Pia inaeleza kwamba katika kila baada ya kipindi cha miaka mitatu, Askari Polisi atapanda cheo kutoka hatua moja kwenda nyingine iwapo katika kipindi hicho hatakuwa amehusishwa na kosa lolote la kinidhamu ambalo litasababisha kutokupanda kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Jeshi hilo kwa kipindi hicho cha miaka mitatu, ni lazima Askari apewe au aende katika mafunzo. Tofauti na hapo ni kumnyima haki yake ya kiutumishi Askari huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limekuwa likilalamikiwa sana na Askari wengi wa Jeshi la Polisi, hasa kwa wale wenye vyeo vya chini au wasiokuwa na vyeo kabisa. Wako wanaodai kuwa upatikanaji wa vyeo hivi unapatikana kwa upendeleo au kwa vigezo visivyokuwa wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inapenda kuiuliza Serikali je, taratibu zinazotokana na Kanuni hii zinafuatwa ipasavyo na kama zinafuatwa, kwa nini malalamiko yamekuwa mengi? Inakuwaje Askari amelitumikia Jeshi hilo kwa miaka 20 lakini anastaafu akiwa hana cheo au anastaafu na cheo cha *CPL* au *SGT*?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kuna waraka uliotolewa wa *WP* kwa wale wote ambao walikwishakuwa na vyeo walivyonavyo kwa muda wa zaidi ya miaka miwili, kwenda katika mafunzo kwa ajili ya kupandishwa vyeo. Jambo la kustaajabisha ni kuwa waraka huo haukuhusisha Askari wa kiume ambao nao walistahili kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaona huu ni ubaguzi wa dhahiri wa kijinsia na unachangia kwa kiasi kikubwa kuligawa Jeshi la Polisi. Tukumbuke katika vyombo vya ulinzi, vyeo vinatokana na muda wa utumishi na juhudi binafsi katika utendaji wa kazi. Kuweka siasa na mipaka ya kijinsia katika vyombo vya ulinzi, ni kuharibu sifa nzuri iliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, cheo katika utumishi maana yake ni maslahi, je, wanaume hawahitaji maslahi hayo? Kwa hili, tunaitaka Serikali kuliangalia upya suala zima la upandishwaji wa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kutokuwahamisha Askari Polisi, kumesababisha matatizo mengi sana kunakopelekea hata Askari hao kusahau wajibu wao na kuanza kujihusisha na vitendo vya uvunjifu wa sheria. Hivyo, tunaitaka Serikali kuliangalia kwa makini suala hili la kuwahamisha vituo Askari kulingana na Kanuni na taratibu zao za utumishi zinavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Polisi wanaotumia pikipiki katika mpango wa kupambana na ujambazi. Huu ni mpango maalum ambao unatumika hasa na Jeshi la Polisi katika jiji la Dar es salaam. Huu sio mpango mbaya katika harakati za kuhakikisha Jeshi la Polisi linatimiza majukumu yake ya kulinda usalama wa raia na mali zao nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya kuasisi mpango huu, Kambi ya Upinzani inapenda kuhoji mambo yafuatayo:-

(1) Je, Serikali imetathmini kiasi gani juu ya ufanisi wa mpango huo na lengo lililokusudiwa?

(2) Je, takwimu za matukio ya ujambazi au uhalifu ambayo yameshawahi kuzuiwa au kuepushwa ni ngapi zilizotokana na juhudi za Askari wa mpango huu? Hili tunaliuliza kwa sababu Askari hawa hutumia gharama kubwa za mafuta ya pikipiki kwa ajili ya zunguka zunguka hiyo.

(3) Je, Serikali inachunguza kwa kiasi gani utendaji wa Kikosi cha Askari hao, kwani kumekuwa na malalimiko ya kuleta usumbufu kwa baadhi ya Askari kudai rushwa hasa kwa madereva na makondakta wa daladala na hata raia wa kawaida? Askari hao wamekua wakipewa majina tofauti kama vile Tigo kutokana na tabia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaomba Serikali ifanye uchunguzi yakinifu kuangalia ufanisi wa mpango huu na ikiwezekana ni vyema kila mara uwe unafuatiliwa kwa karibu isiwe ni kero kwa wananchi bali uwe ni faraja kwa raia wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha *Identification Bureau*, kitengo hiki ni muhimu sana kwa utendaji wa kila siku wa Jeshi la Polisi. Kazi nyeti zinazofanywa na Kitengo hiki ni pamoja na uhakiki wa alama za vidole, kuangalia silaha lakini kwa ujumla wake ni kuhakiki vielelezo mbalimbali vinavyohitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina na kutolewa taarifa inayokidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutoa zabuni kwa kampuni ambayo iliuza vifaa hivyo kwa Jeshi la Polisi (*Technobrain*), ni jambo la kusikitisha na la ajabu kwamba inasemekana kampuni hiyo iliyouza vifaa hivyo, haikuandaa mkakati wa lazima wa kuwaelimisha Askari wa Jeshi la Polisi, kuweza kuwafunza na kuwapa taaluma ya kutumia vifaa hivyo, badala yake Jeshi la Polisi limeajiri watu nje ya Jeshi hilo kufanya kazi hizo nyeti.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, ieleze ni kwa nini Askari waliokula kiapo cha utumishi, wasipewe mafunzo ya kufanya kazi hiyo nyeti? Kwa kuwa bado hatujachelewa, ni lini sasa Askari wetu watapatiwa mafunzo ama ndani au nje ya nchi ili kitengo hiki kwa asilimia mia moja kiendeshwe na Jeshi la Polisi peke yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa silaha, umiliki wa silaha kwa watu binafsi unahitaji kufuata taratibu za kwanza kupitia kwa watendaji katika ngazi ya Kijiji na au mtaa kwa mijini. Lengo na nia ikiwa ni pamoja na kuthibitisha makazi, uadilifu na kuaminika kwa mwomba silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu una udhaifu mkubwa sana, kwani inawezekana rushwa ikatumika kwa wale wasiofuata utaratibu vizuri na kwa uadilifu. Kukosekana kwa uadilifu kwa viongozi katika ngazi hiyo kuna hatari ya kuruhusu wahalifu kupenya na kumiliki silaha kwa kulipa kitu kidogo. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iangalie upya utaratibu huu na kuusimamia kikamilifu ikibidi usimamiwe na au mwombaji athibitishwe na Mkutano Mkuu wa Kijiji kuliko kazi hiyo kuachiwa *WEO* au *VEO* peke yake. Ngazi ya Polisi iwe makini kuthibitisha kuwa taratibu zimefuatwa kwa kutumia utaalamu wao kabla hatua za kuidhinisha utoaji wa silaha kuchukuliwa katika ngazi za juu. Mahali pengine hata wanatumia kinachoitwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Kata chombo ambacho hakiko kisheria. Kwa utaratibu huu, Polisi watashindwa kukataa kutoa vibali kwani tayari Kamati za Ulinzi na usalama ambazo si vyombo vya kisheria wanakuwa wametoa baraka zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuondoa mamlaka ya kuendesha kesi kwa Polisi na kuendeshwa na Idara ya Mkurugenzi wa mashtaka. Huu ni mpango muhimu sana katika kuhakikisha haki za raia katika taasisi ya Mahakama nchini inatendeka kwa wakati na ipasavyo. Jukumu la uendeshaji mashtaka kufanywa chini ya ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka litasaidia ufanisi mkubwa tofauti na hapo awali ambapo lilikuwa chini ya Jeshi la Polisi waliokuwa na kazi ya kukamata wahalifu, kupeleleza makosa, kuwapeleka Magerezani na kuendesha upelelezi katika mashtaka husika, hali ambayo ilileta malalamiko mengi hasa yale ya ucheleweshwaji wa kesi kwa hoja kuwa uchunguzi na ushahidi bado haujakamilika. Ufanisi huu tunaouzungumza utapatikana kwa sababu Jeshi la Polisi sasa litabaki na jukumu moja tu la upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia hii njema, Kambi ya Upinzani, bado ina wasiwasi na upatikanaji wa ufanisi huo. Hii inatokana na kwamba hata *DPP* (Eliaza Faleshi), alikiri kuwa pamoja na kuasisiwa kwa mpango huu, bado kutakuwa na uhusiano wa karibu utakaoendelea kati ya Polisi na Idara hiyo na Mawakili wa Serikali, kwani upelelezi na uendeshaji wa mashtaka ni vitu vinavyohusiana sana. Wasiwasi wetu ambao tungependa Serikali iweke wazi ni kuwa itatumia mikakati gani kuhakisha ucheleweshaji na usumbufu uliokuwepo katika kipindi cha nyuma hautokei tena baada ya kazi hizi mbili kutenganishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano *DPP* katika taarifa yake alieleza kuwa katika kutekeleza mpango huu Mawakili wa Serikali au Wanasheria wa Serikali *(State Attorneys)* 157 wameajiriwa na kupelekwa katika Mikoa 13. Idadi hii ya Mawakili hawa ni ndogo sana ukilinganisha na ukubwa wa Tanzania na haja na malengo ya mpango wenyewe. Lakini pia upelelezi lazima bado unafanywa na Jeshi la Polisi. Kambi ya Upinzani, inadhani bila kuwa na sheria inayoweka viwango vilivyowazi mathalan upelelezi lazima ukamilike ndani ya muda fulani na kama haujakamilika kibali lazima ipatikane kwa ngazi fulani nayo kibali hicho kiwekewe masharti tutakumbana na urasimu mkubwa zaidi kuliko hata awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya mpango huu, Kambi ya Upinzani, inataka pia mambo yafuatayo:-

(a) Serikali iboreshe utendaji wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuajiri watendaji wa kutosha hasa *State Attorneys*.

(b) Serikali iboreshe Taasisi mpya ya Mafunzo ya Uanasheria *(Law School of Tanzania)*, ili kuhakikisha inatoa wahitimu wa kutosha na walio mahiri ambao watafanya kazi katika Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kushikilia nafasi zilizokuwa chini ya Polisi. Ili kuboresha *Law School*, ni lazima itambuliwe kama Taasisi ya Elimu ya Juu na wanafunzi wake wastahili mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ili kuwawezesha watarajali hao kumudu masomo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Interpol Department*, itakumbukwa kwamba kitengo hiki kimeanzishwa ili kurahisisha utendaji wa Jeshi la Polisi hasa kwa mambo yanayohusisha Mataifa tofauti. Kwa mfano, hivi karibuni Kitengo hiki kiliendesha msako wa kuyakamata magari yaliyoibiwa kutoka Japan, UK, Afrika Kusini na Kenya na kuingizwa Tanzania, jumla ya magari 42 yalikamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba iliyopita, nilikitaka Kitengo hiki kifanye kazi ya kumtafuta mtoto Mariam Farid wa Zanzibar, aliyetoroshwa na Mwalimu wake ambaye ni Mganda. Lakini inasikitisha kwamba hadi hii leo Kitengo hiki hakijafanikisha kumtafuta na kumpata mtoto huyu hali ambayo imeleta majonzi yaliyokatisha tamaa kabisa kwa familia ya mtoto huyo mdogo. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya Serikali je, kati ya magari na binadamu, ni kipi kina thamani zaidi? Kwa nini *Interpol* hufanya juhudi kubwa pale magari yanapoibiwa lakini kwa kumtafuta binadamu haionyeshi kama kuna juhudi zozote zinachukuliwa kumtafuta binadamu huyo, wala hakuna taarifa inayotolewa. Huu si uwajibikaji bora wa Kitengo hiki na hakijengi taswira nzuri kwa jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza, Idara ya Magereza, ni mojawapo ya Idara muhimu katika Serikali yetu. Dira ya Idara hii, ni kuwa mfumo wa kurekebisha raia waliopatikana na hatia ya kuvunja sheria za nchi ili watokapo Gerezani wawe raia wema katika jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha usalama wa raia na mali zao, hiki ni chombo muhimu kinachokusudiwa kurekebisha tabia zisizokubalika za wanajamii hasa wale wanaoshikiliwa kwa matendo ya uhalifu na yasiyo ya kimaadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, falsafa ya kuwa na chombo hiki kwa Tanzania, inaonekana haileweki kwani kwa muda mrefu suala la uboreshaji wa mfumo mzima wa Magereza umekuwa ukipigiwa kelele na watu pamoja na taasisi mbalimbali lakini mabadiliko katika maeneo ya msingi yanayolalamikiwa hayaonekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Magereza duniani ni kuwa Vyuo vya Mafunzo ili kuwabadilisha tabia wahusika kutoka katika mwenendo mbaya na wawe raia wema. Lakini kinachosikitisha ni kwamba Tanzania tumeyageuza Magereza na kuwa *Torture Camps*, kwa wafungwa kuwekwa katika mazingira mabaya, kupewa au kufanyishwa kazi ngumu na kutozingatiwa au kunyimwa haki nyingine za msingi zikiwemo za chakula. Hii ni dhahiri kwani hata kiwango cha kilichotengwa na Serikali katika bajeti hii ni nusu tu ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika hotuba ya mwaka jana, Kambi ya Upinzani, iliyataja Magereza ya Kilimo kama vile, Gereza la Kigongoni- Bagamoyo, Gereza la Kiberege –Morogoro, Gereza la Wami Mkuu, Gereza la Kibiti - Pwani na kadhalika. Magereza haya bado yanazalisha ingawaje takwimu zinaonyesha si kwa kiasi kama kile kilichokuwa kikizalishwa miaka ya nyuma. Pamoja na uzalishaji huo, wafungwa katika Magereza hayo wanaishi katika hali ngumu sana ya kupata chakula. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu hali ya maisha na vitendea kazi kwa ajili ya uzalishaji mashambani katika Magereza hayo na kiasi gani halisi kinazalishwa katika Magereza hayo katika miaka mitano iliyopita na chakula hicho kimetumika vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi ya Upinzani, inashauri kuwa mfumo mzima wa Magereza, urekebishwe ili uendane na falsafa ya kuwa na Magereza na sio kuwa na *torture camps* kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa usafiri wa mahabusu na wafungwa. Hivi karibuni Serikali imezindua mkakati wa kuboresha usafiri wa mahabusu na wafungwa wanaotoka na kwenda Mahakamani kwa kutumia mabasi ya kisasa badala ya kutumia makarandinga. Hili ni jambo la kutia moyo na kufurahisha kwani inaonesha kuwa Serikali imetambua na kujali kwamba mahabusu na wafungwa ni binadamu na raia wenye kuhitaji huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho haya yasiishie tu kwa Magereza ya Dar es salaam kama hali ilivyo sasa na yasiishie katika kipengele cha usafiri bali pia yaendelea katika maeneo mengine muhimu kwa mahabusu na wafungwa. Maeneo hayo ni:-

(a) Makazi ya wafungwa na ya Askari yaboreshwe kwa kujenga nyumba ambazo zitafuata viwango vya nyumba za kuishi binadamu kama ilivyo katika Magereza ya nchi nyingine nyingi duniani.

(b) Aina za kazi na adhabu wanazopewa wafungwa na mahabusu, yasiwe ni sehemu ya kumaliza uhai/uwezo wa kimwili wa mhusika kwa mateso makali yasiyo ya lazima bali yawe ni vyuo vya mafunzo kwa ajili kurekebisha tabia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano kati ya Polisi na Magereza *(Symbiotic Relationship),* Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza ni sawa na mtu na nduguye. Magereza wanacho kitengo chao cha ujenzi na vilevile ni watengenezaji wazuri wa samani za nyumbani na ofisini. Kitengo hiki kinaweza kutumika pia kwa manufaa ya Jeshi la Polisi. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri kuliangalia jambo hili kwa makini, kwani kama ukiangalia kiasi cha fedha zinazotengwa kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa samani na eneo zima la ujenzi wa nyumba za Askari badala ya kandarasi hizo kupewa kampuni binafsi kazi hiyo inaweza kufanywa vizuri sana na Jeshi la Magereza. Uhusiano huu ndio utakaokuwa wa tija kwa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ninapenda nitoe mfano kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo inatumia ipasavyo *Symbiotic Relationship* katika miradi yake ya maendeleo. Hali halisi kwa hili, ni ule mradi wa ukamilishaji wa Nyumba za Maendeleo Michenzani Zanzibar ambazo zilijengwa na vikosi vya *SMZ* kama vile *JKU*, Magereza, *KVZ, KZU* tu na si makampuni binafsi ambayo huwa na gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hili likiendelezwa vizuri, magereza yanaweza kutumika kama taasisi za uzalishaji na mafunzo badala ya kutumika kama *torture camps* kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inapendekeza kuwa Serikali itilie maanani suala la matumizi ya '*Symbiotic Relationship'* katika mipango na tasisi zake ili kuongeza kipato na kupunguza gharama kubwa zisizo za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Mambo ya Ndani Wakimbizi na Makambi ya Wakimbizi, Serikali imekuwa ikibeba mzigo mkubwa kwa wakimbizi kutoka nchi mbalimbali za Kiafrika tulizopakana nazo kama vile Burundi, Rwanda, *DRC* na kadhalika. Tatizo hili mara kadhaa limekuwa likisumbua hata bajeti ya Taifa katika kutoa huduma kwa wananchi hao wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa kwamba makambi mengi ya wakimbizi yamefungwa kutokana na baadhi ya wakimbizi kurudi katika nchi zao lakini bado Taifa lina mzigo mkubwa wa wakimbizi wapatao 160,000 waliopo katika makambi manne ya Lugufi 1, Nduta, Mtabila, na Nyarugusu licha ya kambi ya Lukole A kufungwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Serikali inafanya juhudi kubwa katika kuwahudumia wakimbizi ikishirikiana na jumuiya za Kimataifa, lakini kwa sasa na kwa maoni ya Kambi ya Upinzani ni kwamba Serikali ibadilishe sera yake kwa kukemea vikali matendo ya nchi au viongozi wakuu wa nchi jirani yanayoashiria au yatakayopelekea kutokea kwa ghasia zitakazosababisha ongezeko la wakimbizi kuliko kusubiri kuwahifadhi na kuwahudumia wakimbizi, hii ni kwa sababu kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linawezekana na mfano mzuri ni kama ule uliyoonyeshwa kwa Zimbabwe ambapo Waziri Bernard Membe, alitoa tamko kumtaka Raisi huyo ahakikishe uchaguzi unakuwa huru na wa haki ili kupunguza maafa yasiyo ya lazima. Pia njia za usuluhishi baina ya pande zinazogombana, ni hatua muafaka katika kupunguza idadi ya wakimbizi. Mfano usuluhishi wa Kenya, bila usuluhishi wa aina ile leo hii tungekuwa na wakimbizi wengi kutoka Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uraia wa nchi mbili. Suala la kuwa na uraia wa nchi mbili, limekua ni kilio cha muda mrefu katika nchi yetu, hii ni kutokana na kusambaa kwa Watanzania katika nchi mbalimbali duniani. Katika bajeti iliyopita suala hili lilielezwa kuwa lipo ngazi ya Baraza la Mawaziri kwa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ahadi iliyotolewa, inasikitisha kwamba suala hili bado linaonekana halijapewa uzito wa aina yake. Hii ni kwa sababu hivi karibuni Mheshimiwa Khamis Kagasheki, aliliambia Bunge hili wakati akijibu swali la Mheshimiwa Jecha kwamba Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, bado inaliangalia suala hili kwa makini na mchakato utakapokamilika, Muswada utaletwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunaona kuwa kauli ya Waziri katika bajeti ya mwaka jana na kauli ya Naibu Waziri ya juzi, zinapingana. Swali je, kwa usahihi mpango huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kauli ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, ilinishangaza na kukatisha tamaa kwa kusema kuwa suala la uraia wa nchi mbili linahitaji

muda mrefu kwa vile linahusisha Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar kwa sababu suala la uraia ni la Muungano, hivyo sheria ikipitishwa na Bunge inafanya kazi na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri katika jibu lake alibainisha matatizo yatokanayo na kukosekana, kwa uraia wa nchi mbili kama vile Watanzania wengi wanapoteza uraia wao wa kuzaliwa mara wanapopata uraia wa nchi nyingine kwa sababu kwa mujibu wa Katiba yetu kuwa na uraia wa nchi mbili sio halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itekeleze ahadi zake kuhakikisha Katiba inarekebishwa ili kuruhusu Watanzania kuwa na uraia wa nchi mbili na visitumike visingizio visivyo na msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya Utaifa, suala la vitambulisho vya Utaifa/Uraia, ni kilio cha muda mrefu cha Watanzania. Kwa mujibu wa taarifa, ni kuwa mchakato wa kutangaza zabuni kwa ajili ya wakala wa kulishughulikia jambo hili umeshaanza kama ilivyotolewa na Mratibu Mkuu wa mradi huu, bwana Dickson Maimu. Hoja yetu katika hili, ni kuwa Serikali, bado inataka kuchelewesha upatikanaji wa vitambulisho hivyo. Kwa mujibu wa taarifa ya bwana Maimu, ni kuwa mradi huo utakamilika ndani ya miaka mitano kutoka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu hakukuwa na haja ya kuitangaza zabuni kutafuta makampuni au wakala mpya kwa ajili ya mradi huu, kwani RITA, ni wakala tosha na mahiri kabisa ambaye anafaa kupewa kazi hii kwa vile ina takwimu za kutosha za Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ibainishe wazi na kuondoa utata na hofu miongoni mwa Watanzania kuwa itatoa Vitambulisho vya Uraia *(National Identities)*. Hii ni kwa sababu hizi ni dhana mbili tofauti na pia kuna taarifa kuwa vyeti vya kuzaliwa havitakuwa na umuhimu kwani vitambulisho hivi vitatolewa kwa watu ambao sio Watanzania lakini wanaishi Tanzania, je, ni vigezo gani vitatumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaomba Serikali iwe makini katika kuliendea jambo hili hasa hatua nzima ya kumpata mzabuni ili isiingize ufisadi ndani yake na kuliingizia Taifa gharama zisizo za lazima kama zile zilizosababishwa na uzalishaji wa umeme wa dharura kwa Makampuni ya *Richmond* na *Dowans*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kuzingatia yafuatayo katika kuunda mchakato mzima wa mradi wa vitambulisho vya Utaifa.

(1) Vitambulisho viwe vya kudumu na visivyoweza kufojiwa kwa haraka. Hili litawezekana kwa kutafuta makampuni yanayotoka katika nchi zinazotumia vitambulisho hivyo kwa muda mrefu sasa kama vile Uingereza, Marekani na hata Rwanda;

(2) Serikali iwe makini katika Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo kwani hapa ndio sehemu ambayo mtu anaweza kupenyeza taarifa za kunghushi ili baadaye apate Kitambulisho cha Utaifa; na

(3) Kampuni itakayopewa jukumu la kutengeneza vitambulisho hivyo ishirikiane bega kwa bega na Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA), ili kupata takwimu halisi na sahihi za Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa mawasiliano ya simu nchini, ni wazi kuwa nchi yetu katika kipindi hiki, imekuwa na maendeleo makubwa ya matumizi ya simu za mkononi. Hata hivyo, kwa kiwango kikubwa, mawasiliano haya ya simu za mikononi, yanachangia katika ongezeko la vitendo vya uhalifu kutokana udhibiti mbovu wa mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kwamba *line* za simu za kila mtandao zinauzwa hovyo bila udhibiti na kwa bei rahisi kiasi kwamba mtu mmoja anaweza kumiliki hata laini 1000 kwa wakati mmoja. Hii husaidia kwa watu kununua laini akaitumia kwa matumizi yasiyo mazuri na baadaye kuitupa kwa sababu hakuna usajili katika mamlaka maalum nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana ilisemwa ndani ya Bunge hili na Mheshimiwa Waziri kwamba Jeshi la Polisi, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano ya Taifa, itadhibiti mawasiliano ya simu za mikononi kwani imebainika kuwa zinatumika kuwezesha kutendeka makosa ya uhalifu kama utekaji nyara, ujambazi, vitisho na matusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba udhibiti huo haujafanyika, je, Serikali ilishindwa kutekeleza lengo hili kwa nini? Inashangaza kwa vile tunayo Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*), kwa nini isipewe jukumu hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano nchini Canada, South Africa na Australia na hata India, wana utaratibu wa kurejista wamiliki wa laini za simu ili kudhibiti matumizi mabaya ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa mawasiliano ya simu, unahitaji kufanywa pia kwa kuangalia umri wa watu wanaomiliki simu hizo, pia kwa kulingana na mahali walipo kwa mfano iwe ni marufuku wakati wakiendesha vyombo vya usafiri kama magari na pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tulizingatie hili na tusitafute mchawi wa ongezeko la mimba katika umri mdogo, ongezeko la vitendo vya kimapenzi mashuleni na hata vyuo vikuu, ongezeko la maambukizi ya ukimwi, haya yote kwa kiasi fulani huchangiwa na udhibiti mbovu wa mawasiliano ya simu za mikononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inataka *TCRA* ipewe mamlaka ya kutengeneza taratibu za ununuzi na umiliki wa laini za simu ikijumuisha kuwepo usajili wa mmiliki wa laini husika na namba ya utambulisho wa laini hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Zima Moto, hii ni Idara inayolalamikiwa sana katika utendaji wake hasa pale yanapotokea majanga ya moto yenye kuhitaji kushuhulikiwa kwa haraka. Mara nyingi, magari ya uokozi au kuzima moto, hufika eneo la tukio kwa kuchelewa sana kiasi kwamba kama ni nyumba au kitu chochote kinachoungua kinakua kimeshateketea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara chache sana, Idara hii imefanikiwa kuepusha majanga ya moto, hii inatokana na upungufu wa vitendea kazi kama magari na vinginevyo. Inawezekana katika Mkoa mzima huwa hakuna magari ya kutosha ya kuzima moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani, ni kuwa miundombinu ya Idara hii, iboreshwe kwa kununua magari ya kutosha, kuongeza vituo vya kuweka magari hayo ya uokozi na kuongeza watendaji ili ifikiwe ile dhana ya kuwa ni chombo cha uokozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahamiaji haramu, ni tatizo la dunia kwa sasa. Nchi nyingi duniani zinatengeneza Sera na Sheria mahsusi za kupambana na tatizo hili. Kwa upande wa Tanzania, tatizo la wahamiaji haramu, lipo kwani kila leo tunasikia taarifa za kukamatwa watu wanaoingia nchini isivyo halali, sina hakika kwamba tuna Sheria na Sera mahsusi zinazoweka mikakati ya kupambana na wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kwamba mbali ya kutokuwa na Sheria na Sera mahsusi juu ya jambo hili, lakini pia inaonekana Idara zinazohusika hazilifanyii kazi ipasavyo tatizo hili. Nitatoa mfano au ushahidi wa kauli yangu kupitia taarifa ya Peter Kivuyo, *(Deputy Director of Criminal Investigation),* alisema wakati akitoa taarifa juu ya operesheni ya idara ya *Interpol* kuchunguza magari yaliyoibiwa kutoka katika nchi mbalimbali na kuletwa Tanzania kwamba wamekamata wahamiaji haramu 11 kutoka Kenya, Rwanda na Somalia ambao wapo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa kama si operesheni hii, wahamiaji hawa haramu wasingekamatwa. Hivi kweli tunaipenda Tanzania yetu? Maoni ya Kambi ni kuwa, iwekwe Sera na Sheria mahsusi ya kudhibiti wahamiaji haramu nchini ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunaiomba Serikali kuweka mtandao wa kudumu wa *computer* katika *entry point* zote nchini ili kujua na kudhibiti wageni waingiao na watokao nchini. Hii itawarahisishia Idara ya Uhamiaji kufanya kazi zao kwa urahisi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Micheweni, kwa ushirikiano wanaonipa pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, tujitahidi kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nakuja kuwaita wachangiaji. Hali yetu ilivyokaa hapa, walioomba kuchangia pekee yao wapo 43, leo tumetumia muda mwingi sana. Kwa hiyo, mchana huu tunaweza kupata wachangiaji wawili tu na tutaanza na wale ambao hawajachangia hata mara moja ambao wapo saba, waliochangia zaidi ya mara mbili wanakwenda zaidi ya kumi na ngapi huko. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, wengi hamtapata nafasi ya kuchangia.

Sasa nitamwita kwanza Mheshimiwa Bahati Ali Abeid lakini pia nitamwita Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa hata kama amechangia mara moja kwa sababu anapaswa kwenda kuungana na Mheshimiwa Spika, kule Kuala Lumpur**.** Kwa hiyo, anaondoka mchana huu, lakini hata hivyo angepewa nafasi ya kuchangia. Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, wajiandae.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi mchana wa leo kuwa mchangiaji wa kwanza katika hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake kwa hotuba hii nzuri ambayo inawapa moyo Watanzania walio wengi kwa uhakika wa ulinzi na usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu, kwa kuwapongeza Askari wetu wa Jeshi la Polisi, kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa ya kulinda raia na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zetu hao wanafanya kazi kubwa sana ambayo inaleta matumaini kwa wananchi walio wengi hasa pale wanapokabiliana na majambazi na kuwatia mikononi. Lakini pia kwa kufanikiwa kushika silaha nzito ambazo zingeathiri mali na wananchi wetu walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, ametueleze kuwa Serikali ina mikakati ya madhubuti ya kuboresha hali ya kukabiliana na wahalifu wakiwemo na majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niiombe Serikali wanapofanya maboresho hayo basi waliboreshe na Jeshi letu hili kwa posho na mishahara kwa sababu ndugu zetu hawa, wanafanya kazi kubwa. Kwa hiyo, Waswahili tunasema mcheza kwao hutunzwa na wao imefika wakati muafaka sasa Serikali ilione Jeshi letu hili ilitunze, lakini isilitunze kwa mishahara na posho tu, pia iwatunze katika makazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu hawa, wanaishi katika mazingira magumu sana, mazingira ambayo hatukuzoea kuishi Watanzania, mazingira ya chumba kimoja, baba na watoto, ni mazingira magumu kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali mwakani iiongezee bajeti Wizara hii ili waweze kujenga nyumba nyingi zaidi za wafanyakazi na siyo nyumba ya chumba kimoja kwa Askari mwenye mke na watoto wapewe nyumba yenye vyumba viwili ili aweze kuishi kwa mazingira ambayo yamezoeleka kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema tuboreshe mishahara, kila mfanyakazi anapoomba aboreshewe mshahara, anajiwekea hatma yake ya baadaye, hata kama hali ya maisha imepanda zaidi, mishahara ya Askari wetu haiwezi kukabiliana na hali ngumu hasa ukizingatia Askari wetu ni watu wa kuhama hapa na pale kila siku. Mwaka huu, anaweza akawa yuko Pemba lakini mwaka ujao anaweza akawa yuko Mbeya, hawezi kukabiliana na maisha magumu tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapomhamisha Askari kutoka eneo moja kwenda eneo lingine, inakuwa umemvurugia utaratibu wake aliojipangia wa mwaka nzima. Kama tunavyojua, kila mmoja ana bajeti yake ya mwaka nzima na Askari hana mradi mbadala, Askari hawezi kulima, Askari anafanya kazi usiku na mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anapojaribu kulima hapa mwaka ukiisha, anaacha mazao yake anakwenda Mkoa mwingine, amevurugikiwa na pengine kule anakokwenda unamwambia posho yako ya kutolewa hapa kwenda sehemu nyingine Serikali sasa hivi haina,

itabidi ukopeshe. Hivi Askari huyu akopeshe anazipata wapi? Serikali haina fedha mpaka Askari akopeshwe kweli? Naiomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri, tunapomhamisha Askari kwenda sehemu nyingine basi tuhakikishe yale mafao yanaandamana na safari yake kuliko kuambiwa akopeshe, atapewa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke hapo sasa niende moja kwa moja kwenye ajira ya Jeshi hili la Polisi. Hivi karibuni Wizara imefanya ajira kwa vijana wetu. Utaratibu uliotumika kuwapata vijana hawa ambao watajiunga na Jeshi la Polisi, si mbaya hata kidogo kwa sababu umeanzia Wilayani ukaenda Mkoani. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba sisi wanawake, tunasema wanawake mbele kwa maendeleo na sio nyuma, mchakato huu ulipofanywa, wanawake wamepewa nafasi chache katika ajira. Unaposema niletee wanaume 30 au 40 lakini wanawake wawili kwa Mkoa, haipendekezi hata kidogo. Wanawake tupewe nafasi, tunaweza, ushahidi upo wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa wa Upinzani, anasema wanawake wa Jeshi hili wanapewa vyeo zaidi kuliko wanaume, si kweli, lakini wanawake tunafanya kazi kubwa na tuna uwezo mkubwa. Mwanamke unapomweka katika nafasi ya uongozi, anafanya kazi kubwa, ili asijivunjie hadhi yake kama mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani, namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapoajiri tena vijana basi wanawake tupewe nafasi zaidi isiwe nafasi mbili kwa Mkoa, hazitoshi, wanawake wanalalamika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia mishahara kwa sababu viinua mgongo vya Askari wetu hawa wanapostaafu vinakuwa vidogo sana. Viinua mgongo vyenyewe baadhi ya Askari wetu wa chini wanapostaafu, wanapata taabu kubwa sana kupata kiinua mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lililopita la Bajeti, nilichangia hapa Wizara ya Waziri Mkuu, kuwa Askari wetu wanachelewa sana kupatiwa viinua mgongo wakati wanapostaafu. Wapo Askari baadhi wamestaafu, wamefikia miaka minne na kuendelea mpaka leo hii hawajapatiwa kiinua mgongo. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa na kujibu hoja za Wabunge basi atuambie ni Askari wangapi wameishi zaidi ya miaka minne, mitano ambao hawajapata viinua mgongo yao na ni kwa nini, atupe sababu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie katika eneo la michezo, maana kengele ya kwanza imeshalia. Jeshi letu la Polisi, kuna michezo mbalimbali hata kama kumejitokeza muono wa karibu sana kuwa Serikali yetu inapenda sana mpira wa miguu kuliko michezo mingine lakini Jeshi letu la Polisi kule Zanzibar wana timu ya *netball* ya wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wetu hawa wameiletea sifa nchi yetu kwa kupata ushindi wa Afrika ya Mashiriki zaidi ya miaka mitatu na kuendelea. Hii ni sifa kubwa kwa kuitangaza nchi yetu ya Tanzania. Lakini Askari wetu hawa hatuwapongezi au kama tunawapongeza ni kwa mdomo tu lakini kwenye sekta yako naambiwa ndiyo kwenye chakula chako, ndio kwenye kujivunia kwako. Kwa hiyo, tuwape vyeo Askari wetu hawa kwa kuwapongeza. Tuwapatie vyeo kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kutuletea nuru, kuitangaza nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wapo vijana ambao wanashirikiana na Jeshi hili kwa michezo mbalimbali. Kuna kijana ambaye anashirikiana na timu yetu hii, kapata tunzo mara mbili kuwa mfungaji bora. Tunaonaje tukimwajiri katika Jeshi letu ili akaingia katika

sehemu ya michezo ili akaweza kutuletea maendeleo zaidi kwenye michezo hii ya Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizidi kusisitiza katika sehemu ambazo nimechangia. Naomba sana mishahara iboreshwe kwa Jeshi hili hasa Askari wa chini lakini pia nyumba za Askari wetu ziboreshwe. Wanamichezo wetu wapewe kipaumbele, wapewe vyeo kwa kazi kubwa wanayoifanya lakini wastaafu wapatiwe mafao yao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa muda huu ili nichangie hotuba nzuri sana hii ya Mambo ya Ndani.

Mimi nianze kwa kusema kwamba sina tatizo na hotuba kimsingi kwa sababu wala sina sababu ya kuwahukumu kwamba kuna mambo mengi hawakufanya wakati uwezo wa kifedha hawana. Lakini kuna mambo machache ambayo ninapenda niseme na ninaomba wayasikilize vizuri ili wayarekebishe kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze na Kitengo cha Usalama Barabarani. Jeshi la Polisi ni zuri na hicho Kitengo chenyewe cha Usalama Barabarani ni kizuri kwa ujumla wake. Lakini kuna watu miongoni mwao wanakuwa na matatizo na huu ni ubinadamu kwa sababu aliyekuwa Rais wa Marekani Izan Haur, alipokuwa anazungumza na wanafunzi wa Penslania, aliwaambiwa maneno yafuatayo na mimi naomba niyanukuu:-

*"The creation of money and the coming of the women, made the world very dangerous place to leave, because many people, when the question of money comes, are untrustworthy"*. Haya ni maneno ya Izan Haur wala si yangu mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Usalama Barabarani kama tunawaangalia wao sio wanaoanzisha matatizo, wanaoanzisha matatizo mara nyingi ni wenye magari wenyewe. Kwa sababu gari itasimama, Kondakta anazungumza kidogo na Dereva, unamwona anashuka amebana mkono, wanakwenda pembeni na Askari, hujui kinafanyika nini. Mimi ninashauri mazungumzo yote ya Dereva na Utingo wake, yafanywe ndani ya gari na abiria waliomo mle wawe wanasikia kinachozungumzwa kama Askari wa Usalama Barabarani wamebaini kuna tatizo. Hizi tuhuma ndogo ndogo zitaondoka, zitaondoka kabisa lakini haiwezekani wanashuka Askari wanakwenda pembeni watu wasituhumu, watatuhumu kuwa kuna fedha zinatolewa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kuwa hili ni tatizo wala si la wote ni baadhi yao. Hivi karibuni nilikuwa kwenye basi natoka hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam. Basi lilianza kujazwa watu sana hapa hapa na wakawa wanaendelea kupakia mpaka tulipofika Dumila. Kuna kijana mmoja pale anaitwa Will, ni *Inspector*, ndiye anayeongoza Kitengo cha Usalama Barabarani kwenye Kituo kile, alikuja yeye na Askari wake wawili, waliingia ndani ya gari, wakawashusha watu wote waliozidi mle, wakawalazimisha wenye gari kuwalipa watu nauli zao pale pale wapande magari mengine na wakamzuia mmoja wa tajiri wa gari na konda ili wawawepeleke Mahakamani, sasa huu ndiyo utaratibu. Sasa kama wapo wanaofanya wala huna sababu ya kusema kuwa kitengo chote kimeoza lakini kuna tatizo. Sasa mimi nafikiri utaratibu huu unapaswa kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Uhamiaji. Watu wameshasema sana kuhusu uhamiaji na *ID cards* na mambo mengine. Sasa hivi tuna tatizo kubwa. Lazima tuelewe kuwa nchi yetu tunapakana na watu wengi ambao wanaweza wakatumia fursa hiyo ya kuwa ni majirani zetu, kuingia ndani ya nchi na kufanya vitu vya ajabu ajabu. Hatuwezi kuwabagua miongoni mwao na sisi kwa sababu ya vitambulisho. Inasikitisha leo ni zaidi ya miaka 40 ya uhuru wetu jambo hili hatujaweza kulifanya. Majirani wetu wote, tayari wana vitambulisho. Sasa ninaomba hiki kigugumizi hebu kiondoke. Tuweke lengo kwamba ikifika mwaka 2010 kabla ya uchaguzi, kila Mtanzania atakuwa na kitambulisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa kwenye suala la *passport. Passport* katika nchi nyingi duniani ni haki ya msingi ya raia wa nchi hiyo lakini kwetu bado inaonekana ni tatizo. Hapa kutafuta *passport* ni balaa. Mtu itabidi atafute mtu wa kumshika mkono, itabidi atafute mtu wa kumsaidia kana kwamba anaomba kitu kigeni, wakati ni haki yake ambayo amepewa Kikatiba kwa sababu ili utembee unapotaka, kama ilivyosema Katiba, lazima upate *passport.* Sasa kwa nini inakuwa ni usumbufu mpaka upite kwa huyu, uzungumze na huyu, uulizwe maswali, sijui babu yako kazaliwa wapi, sijui baba yako kazaliwa wapi, inahusu nini mambo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama baba yangu na mama yangu wamezaliwa ndani ya nchi hii kuna sababu gani ya kuniuliza mambo mengine, kwa sababu *definitely* mimi ni raia wa hapa! Ndiyo! Hiyo ni kwa mujibu wa Sheria ya Uraia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, napenda kusema kuwa kuna tatizo ndani ya Ofisi zetu za Kibalozi. Watanzania walioko nje wanapotaka kubadilisha *passport* zao katika Ofisi za Kibalozi, wanasumbuka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mifano ya watu wawili hapa. Nina mfano wa kijana mmoja, anaitwa Seif Ali, yeye ameomba kubadilisha *passport* yake ili apewe mpya kwa sababu imekwisha muda katika Ubalozi wetu wa London. Ni zaidi ya miaka 2 sasa hajafanikiwa. Baba yake ana matatizo, anaumwa, anashindwa kuja kumwangilia kwa sababu hana *passport,* mara anaulizwa hivi, mara anaulizwa vile, inasumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko bwana mmoja, anaitwa Sharani Said Ali. Huyu naye ameomba kubadilisha *passport* katika Ubalozi wetu huo huo wa Uingereza. Mtu ambaye yuko Uingereza kwa miaka zaidi ya 25, 30, linaletwa faili lake hapa, anaulizwa wewe ulikwenda kufanya nini huko? Sasa mimi nafikiria haya siyo masuala ya ulikwenda kufanya nini huko, wewe unapokuja hapa London ulikuja kufanya nini, si sote tunatembea? Sasa mtu anapokwenda unamwuliza maswali ya ajabu ajabu ili umkwamishe tu. Kwa kweli hii si haki na huu si ustaarabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kinachoshangaza, unamwuliza Mkurugenzi hakujibu. Unauliza Wizara ya Mambo ya Nje, hawajibu. Hawa jamaa wa Mambo ya Ndani labda nisiwahukumu, sijawauliza sana. Lakini natumia fursa hii kuwauliza leo, hebu watujibu. Kiongozi wa Upinzani anasema yeye amewauliza mpaka kwa maandishi lakini watu wa lugha ya mjini, wanasema wanakula jiwe, hawajibu kitu. Sasa hili ni tatizo. Mnawasumbua watu visivyo halali. Watu wetu, raia wetu msiwafanye wakajiona wanyonge ugenini. Namalizia hilo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye Askari Polisi. Askari Polisi, ni Askari wanaofanya kazi za kujituma kwa kiwango kikubwa sana na mimi nasema ndiyo Askari wanaofanya kazi kubwa kuliko Askari wa aina yoyote waliopo ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukiwa wa kweli, Askari Polisi wana matatizo makubwa. Wana matatizo ya kuishi kwa maana ya nyumba zao na hapa nipongeze tu juhudi ambazo zinachukuliwa na Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla za kuwajengea nyumba Askari Polisi. Ukweli, hili ni jambo ambalo ni lazima tuliheshimu na tuiombe Serikali iendelee kufanya hivyo kwa nia safi kabisa kwa sababu hawa ni watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa ukiangalia chakula, Askari mwenye familia ya watoto watano, sita, saba unamlipa shilingi 1,600 kwa siku kuwa ndiyo posho yake ya chakula, inasikitisha sana. Sasa ile simwambii Waziri wa Mambo ya Ndani kwa sababu ndiyo bajeti keshapewa, bajeti zetu zina *ceiling* lakini ni suala ambalo Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu wewe ndiyo Mkuu wa Serikali, jambo hili ni vizuri mkaliangalia mapema, mkaona ni namna gani tunaweza kuwapandishia Askari posho hii ya chakula. Shilingi 50,000 kwa mwezi jamani na pengine anakaa mbali, anakwenda kufanya kazi mahali pengine, huo usafiri hana, atazitumia kwa nauli tu. Nafikiri ni vizuri, tunaona magari ya watu mbalimbali Askari Polisi wanaomba *lift*, sasa Askari Polisi unaomba *lift* kwenye gari ya abiria, inasumbua kidogo, tujitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapo hapo, pesa tunazitumia kwa mambo mengine. Nimeangalia kuna pesa wanazodai Askari Polisi ni kama bilioni tano hivi ni malimbikizo mbalimbali. Lakini wakati huo huo, kuna pesa kama bilioni 1.6 zimetengwa eti kununulia magari ya maji machafu. Sasa Waziri Mkuu, unatununulia magari sisi ambao hatuna fujo, sisi tunaogopa nguo tu ya Askari achilia mbali gari. Nasema sisi kwa sababu gari liko moja Pemba lakini limetumika siku hii moja tu siku ya tarehe 30 usiku watu wamekaa kwenye Ofisi ya *CUF*, Wilaya wamemwagiwa maji, halaa si nimekaa ghalani! Sasa kwa nini hizi pesa bilioni 1.6 usiwalipe Askari? Kwa nini usiwalipe Askari hizi pesa, haya mambo mnaweza mkafanya katika bajeti ya mwaka 2010/2011, mkanunua magari manne, matano, lakini siyo sasa hivi. Sasa hivi walipeni hawa jamaa, wana dhiki, wana njaa bwana. Matokeo yake, tutawahukumu kwa vitu mbalimbali, wanachukua rushwa, hawataacha mandhali wana njaa, watachukua tu. Waboresheeni mishahara, walipeni haki zao ili msiweze kuwakuhumu kwa mambo madogo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hapo sasa niondoke nije *specifically* kwenye Askari wa Zanzibar. Nimezungumza hivi karibuni kabisa, wamenieleza kisa ambacho kimewapata wa Askari Pemba, kama jambo hili limetokea kweli Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, naomba ulifuatilie kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari walikuwa na madai yao, zimeletwa vocha ambazo tayari ni za malipo kutoka Zanzibar kwenye Kitengo chao wenyewe, wameambiwa watie saini vocha hizo, ikiashiria kuwa wanalipwa halafu vocha zimechukuliwa pesa hawakupewa. Mpaka hivi tunavyoongea, pesa hizo hawajapewa. Sasa kama Askari ambao tunawatuma sisi kuchunguza mambo kama haya wanafanyiwa wao sasa, hili ni jambo la ajabu sana. Ninapenda suala hili kama limetokea, Mheshimiwa Waziri ulifuatilie kwa karibu na uone imekuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, askari wanaokwenda kusoma, Askari waliokwenda kusoma hivi karibuni, upande huu wa Tanzania Bara wamelipwa pesa zao, *alhamdulilah*, wamekwenda kulipwa pale kwenye chuo lakini Askari wa Zanzibar mpaka hivi tunavyozungumza hawajalipwa. Sasa hii inajenga sura ya kuwa Askari wa upande fulani wanakumbukwa haraka wa upande mwingine hawakumbukwi, naamini wala siyo madhumuni

ya msingi ya Jeshi la Polisi, siamini kabisa, ni utendaji mbovu wa baadhi ya watu, naomba hili mlirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika hilo hilo, kuna Askari ambao wanaporudi masomoni wanapewa pesa kidogo ni kama Sh.140,000 hivi. Ni pesa ndogo hiyo, lakini wenzao wa huku Bara wapewa wa kule Zanzibar hawajapewa, wapeni!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kingine ambacho ni cha kusikitisha zaidi na hiki kinaonekana kimsingi ndiyo chenye kuzua matatizo. Askari walikopeshwa *Vesper* na vyombo vingine vya usafiri. Pesa zao zimekatwa kidogo kidogo kama ilivyo utaratibu mpaka wamemaliza mikopo. Lakini kuna habari ya kuwa aliyekopesha *Vesper* hajalipwa hizi pesa na ndiyo maana sasa hizi pesa ndogo ndogo zinazokwenda kwa madhumuni ya kupewa Askari badala ya kupewa Askari wenyewe zinakwenda kulipiwa madeni. Kama hivyo ni kweli, hilo ni jambo la hatari, ni jambo ambalo linajenga uadui na uhasama usiokuwa wa lazima ndani ya chombo hiki ambacho kina nidhamu kubwa. Askari bahati nzuri hawatoi mambo yao mpaka yawe yamewafika kweli kweli, wala hawagomi, hawa siyo wanafunzi kuwa watagoma wakapigwa marungu, watalalamika tu lakini watalalamika mpaka lini? Unamfanya mtu ambaye ana bunduki alalamike kila siku, nafikiri Wizara inapaswa kuchukua hatua ya haraka sana ili Askari wetu wapunguze kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikukusudia kusema sana, lakini nasema, masuala ya madai ya Askari yaangaliwe, mishahara yao iangaliwe na hizi tofauti, Askari hawa wanafanyiwa hawa hawafanyiwi, ni mbaya mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kama ambavyo sisi sote humu ni maiti watarajiwa yaani iko siku tutakufa na vile vile Askari wale wote, wenye vyeo vikubwa kubwa, ni wastaafu watarajiwa. Sisi Wabunge humu, kuna Wabunge walioacha Ubunge labda miaka minne, mitano ukiwaona mitaani unasikitika. Sasa Askari utakuja sikitika zaidi, ndiyo maana yake, unamkuta anakuwa mlinzi pahala tu, anadhalilishwa tena Askari aliyekuwa na cheo kikubwa. Naomba muangalie mafao yao, muangalie hali zao za baadaye zitakuwaje baada ya kustaafu. Tusiwadhalilishe watu ambao wamelitumikia Taifa kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hawezi mtu kuchangia ukatosha dakika zake. Kwa hiyo, tukirudi saa za jioni, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji ajiandae, Mheshimiwa Fatma Othman Ali naye ajiandae. Mheshimiwa Rajab Hamad Juma na Mheshimiwa Ali Juma Haji hawa ni wale ambao hawajachangia hata mara moja, muwe karibu na wengine nitawataja jioni.

Sasa wakati tunaendelea na msiba wetu, Mheshimiwa Kiongozi wa Mapinduzi, ametuma salamu za rambirambi kupitia kwa Waziri Mkuu na kwa Spika kama ifuatavyo, ninanukuu:-

"*Nimepokea kwa masikitiko makubwa, habari za kifo cha Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mbunge wa Chama Cha CHADEMA, aliyefariki Dodoma usiku wa kuamkia jana kwa ajali ya gari wakati alipokuwa akitokea Dodoma kwenda Dar es Salaam.*

*Wakati wa uhai wake, marehemu alikuwa miongoni mwa Wabunge wa Upinzani waliokuwa wakitoa michango mbalimbali katika mijadala ya Bunge. Kwa mantiki hiyo, Chama chake na nchi yetu, imempoteza Kiongozi ambaye alihitajika sana katika shughuli za Bunge.*

*Kwa hiyo, kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Kiongozi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, natoa salamu za rambirambi kwako na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaitakia familia yake, wananchi wa Jimbo la Tarime na Wabunge wote, subra katika kipindi hiki kigumu cha msiba.*

*Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina".*

Imesainiwa na Mheshimiwa Nahodha Shamsi Nahodha, Waziri Kiongozi na Serikali ya Mapinduzi. Kwa niaba yenu, tunashukuru sana kwa ujumbe huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tutarudi tena saa 11 jioni. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 kamili jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana, niliwataja wafuatao wangeanza. Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Othman Ali na Mheshimiwa Rajab Hamad Juma na Ali Juma Haji, watafuatia. Mheshimiwa Dr. Haji!

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa machana huu wa leo na mimi kupata fursa ya kuwa mchangiaji katika hoja iliyokuwepo mbele yetu, hoja ya Mambo ya Ndani.

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nimefikia siku hii ya leo na mimi kuipata nafasi hii katika kuchangia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea zaidi, ninaomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja lakini kuunga mkono kwangu kutakuwa na masharti mwisho wa mazungumzo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, nimpongeze zaidi *Inspector General*, Mheshimiwa Mwema, pamoja na Makamishna wote, kwa mujibu wa taratibu na hasa zaidi Kamishna wa Zanzibar ambako ndiko ninakotoka na ninashuhudia jinsi gani anavyopata taabu na kazi katika kuendesha shughuli za kazi yao huko Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ulinzi na hasa kazi ya Polisi, ni kazi ngumu. Kama tukizingatia kwamba sisi tumelala, sisi tunaangalia ngoma, sisi tunaangalia michezo kama Simba na Yanga lakini matokeo yake ndugu zetu hawa wa Polisi mambo hayo yote wana hamu nayo wanashindwa kwa ajili ya kutekeleza wajibu wao wa kulinda usalama wa raia

pamoja na mali zao. Sasa tufikirie kazi kama hii ambayo inawabidi wao kuitekeleza kila wakati, ina ugumu gain kuwafikiria?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu, kuna msemaji mmoja ambaye kwa mujibu wa toleo lake au maelekezo yake, kutoka Kambi ya Upinzani alisema hivi:-

*"Inaeleweka wazi na vyema kwamba kazi hii inahitaji muda wa mapumziko kwani zile siku ambazo raia au hata wafanyakazi wanapopata mapumziko au kusherehekea sikukuu mbalimbali nchini, Askari yeye huwa ndiye wakati wake mgumu wa kuhakikisha kwamba kila kitu kinakwenda salama. Ukweli wa mambo ni kwamba Askari wote wa Jeshi la Polisi ni wenye nidhamu ya hali ya juu kabisa katika utendaji wao."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikiwa kama hii ndiyo hali halisi ya utendaji wa kazi wa Polisi, nitashangaa kama kutakuwa na malalamiko ya kusema kwamba mtu kupekuliwa mwisho saa 12.00, wakati mtu huyuhuyu vitendo vyake vinakuwa kuanzia saa 12.00! Kweli hapo kuna uhalali wa kusema kwamba asipekuliwe baada ya saa 12.00?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, kwa upande wangu, nafikiri Askari waachwe wafanye kazi yao kwa mujibu wa taratibu zao wanavyoona zinafaa, mradi hawavunji sheria, kanuni na kumdhulumu mtu yeyote. Kwa hivyo, mimi naunga mkono kabisa juhudi kubwa wanayofanya ndugu zetu hawa wa Polisi katika kudumisha hali ya usalama wa nchi yetu na kututendea yale ambayo wanahisi yanafaa kwa ajili ya usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia, ni kuhusu usafiri kwa wenzetu hawa. Ni jambo la kusikitisha sana kwamba leo unamkuta Askari wakati wa asubuhi au wakati wa mchana, pengine keshachoka, anatamani kurudi nyumbani au asubuhi anataka kwenda kazini, tunaburuzana kwenye milango ya daladala, anataka kwenda kazini awahi, kwa sababu hana usafiri. Sasa ikiwa kama leo ni hali hii ya usumbufu kama huu kwa usafiri wa ndugu zetu hawa Askari, tutategemea vipi Askari huyu leo achukue jukumu walau la kuwatetea watoto wadogo wanaodhalilika katika kupanda daladala ya kutaka kuwahi shule wakati na yeye anangojewa kazini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Wizara na kwa maana hiyo Serikali, izingatie suala la usafiri wa Askari. Hili si jambo la kubuni, ni jambo ambalo nalishuhudia. Kwa sababu ninapokuwepo Dar-es-Salaam, mimi huwa ninakaa Gongo la Mboto, asubuhi nitoke Majohe nije Gongo la Mboto, Gongo la Mboto ndio niwahi kazini Ofisi ya Bunge, ninakumbana nao. Kwa hiyo, nafikiri suala hili linahitaji kufanyiwa marekebisho ya haraka na kwa kila hali ili kuhakikisha kwamba ndugu zetu hawa ambao hawaishi katika Makambi ya Askari au hata wale ambao wanaishi kwenye makambi, wapatiwe usafiri. Ikiwa kama ni usafiri wa pamoja au kwa wale ambao watataka waweze kupatiwa walau vyombo vya usafiri kwa mikopo ili kuwasaidia katika safari zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu makazi ya Polisi na ulinzi kwa jumla. Kwa kweli ni aibu kwa jinsi nchi yetu Tanzania inavyosifika na kwa ukweli sio sifa za kubuni, lakini utashangaa leo unamkuta Askari anajibanza katika banda lililojengwa na mabati, choo atoke nje kwenda kujisaidia. Najua kweli hali ya uchumi ni mbaya lakini kuna kila hali ya kuona kwamba suala hili nalo linazingatiwa ipasavyo. Naishukuru sana Wizara kwamba safari hii imetenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za ghorofa, lakini fedha hizi isiwe kutengwa, zitengwe halafu zitolewe na katika kutolewa zitumike vile ambavyo inapaswa ili kuwaondoshea usumbufu ndugu zetu hawa Askari na hili sio kwa sehemu moja takribani sehemu zote. Ninashauri kwamba wajaribu kutafuta vifungu, wachukue sehemu moja, waamue kwamba mwaka huu tunajenga hapa, mwaka huu tunajenga hapa, mwaka huu

tunajenga hapa, kwa kufuata zile *priorities* zilizokuwepo katika sehemu zao hizo za kuishi pamoja na kuendeleza kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninapenda kuliongelea ni kuhusu ajira ya Askari Polisi. Kuna malalamiko kwamba suala la ajira ni suala nyeti lakini juu ya unyeti wake, tunaamini kwamba tunahitaji watu ambao ni waaminifu, waliokuwa na afya njema, wachapa kazi, waliokuwa na taaluma ya kufaa katika Jeshi letu la Polisi. Lakini kinachonisikitisha ni kwamba sheria hizi za uajiri sijui zikoje, leo ukichukulia kama watu wa Zanzibar mrefu wao ni kama mie, futi tano au pengine zaidi ya mimi ufupi wao, leo anakuja kuandikisha Polisi kapungua nchi mbili anaambiwa wewe hufai, eeh, japo ana taaluma ya kutosha lakini anaambiwa wewe hufai kwa sababu urefu wako umepungua inchi mbili. Kwani jamani katika kazi za Askari hakuna kazi zinazofanywa na Askari wafupi? Sisi tuliokuwa wafupi tusile? Mbona nawaona wafupi na wanafanya kazi vizuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninashauri sana kwamba sheria hizi kuna haja ya kupitiwa upya na ikionekana kwamba kuna upungufu kidogo zirekebishwe. Hivi sasa ni wakati wa sayansi na teknolojia sio wakati wa urefu na unene, wako watu warefu na pengine utendaji wao wakashindwa na watu waliokuwa wafupi. Ninaamini katika jeshi la Polisi, wako wafupi na wanafanya kazi vizuri sana. Kwa hiyo, ninaomba sheria hii ipitiwe upya na iweze kuangaliwa ili tuhakikishe kwamba haki inatendeka kwa waliokuwa wafupi na waliokuwa warefu. Kuna kazi ambazo hata Askari akiwa mfupi anaweza akazifanya la kama si hivyo nasema labda porini wangebakia twiga tu waliokuwa warefu wanaona mbali, lakini akina chura wasingeweza kuishi. Kwa hiyo, ninaomba sana sheria hii ipitiwe upya na irekebishwe pale inapowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ninapenda kulizungumzia kabla sijapigiwa kengele, ni kuhusu suala la Askari kupendana. Kuna kila haja ya kuona kwamba katika Jeshi hili la Polisi wote pamoja na Mambo ya Ndani wawe wanapendana. Haitapendeza kumuona Askari mmoja ambaye kwa uwezo wake akachukua hatua za kumdhalilisha Askari mwingine aliyekuwa mdogo na akafikia kiwango cha kumpa uhamisho au kumnyima cheo eti tu kwa sababu ambazo ni za kibinafsi au kwa sababu ya kutokuelewa. Ninawaomba sana ndugu zetu wafanyakazi wa Jeshi la Polisi, Usalama wa Raia kwa jumla, pamoja na vyombo vyote ambavyo vinahusiana na Mambo ya Ndani, kuanza kupendana wao kwanza. Wapendane ili kuweza kuhakikisha Jeshi lao la Polisi linakwenda sambamba na kila Askari akiwa mkubwa au akiwa mdogo, anatekeleza kazi zake bila ya uwoga au bila ya wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikiwa tu kama masuala haya niliyoyazungumza kuhusu Mheshimiwa Waziri kunipa taarifa hapa, kunijibu kwamba inawezekana na kusema kwamba labda Askari watapimwa kwa kiwango hiki, tena hapo itakuwa ile kuunga mkono kwa hoja hii, sitaweza kuiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na usafiri, ninashindwa kuunga mkono Wizara au serikali kwa kero hii, kwa nini haiwapi fedha za kutosha Wzara hii ili waweze kumudu kufanya kazi zao ipasavyo? Naiomba sana Serikali kutokana na ugumu na unyeti wa kazi za ulinzi, tafadhali ifanye kila jitihada ya kuona kwamba inawatengea fedha za kutosha ili kufanikisha kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia zote mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, sinabudi nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia siku hii ya leo kuweza kusimama kwenye ukumbi huu wa Bunge nikiwa mzima wa afya na pia kuweza kuchangia hotuba nzuri aliyoitoa Waziri wa Mambo ya Ndani. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na Sheria za Jeshi la Polisi. Sheria za Jeshi la Polisi, nyingi zimeshapitwa na wakati. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, kuleta Muswada kwenye Bunge hili ili Sheria hizi zirekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba kumshukuru au kumpongeza Mkuu wa Jeshi la Polisi, *Inspector General,* Said Mwema, pamoja na Kamishna, Hamisi Simba, Kamishna wa Zanzibar, pamoja na makamanda wake wote wa Zanzibar, kwa kazi kubwa na juhudi zao kubwa walizozifanya kulipunguza kwa kasi kubwa wimbi la ujambazi ambalo lilikuwa linatusumbua sana wananchi wa Zanzibar. Kwa hilo, nawapa hongera na Mungu awajalie wazidi kuifanya kazi yao hiyo kwa salama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye vitendea kazi vya Jeshi la Polisi. Hii ni mara ya tatu nasimama kwenye ukumbi wako huu kuomba vitendea kazi kwenye Jeshi la Polisi hasa kule Zanzibar. Jeshi la Polisi Zanzibar, lina matatizo makubwa ya vitendea kazi hususan, gari, pikipiki, radio za mikononi, zana za kufanyia kazi maofisini, wangali bado wana zana za kizamani na bado magari mengi waliyokuwanayo Askari au Kikosi cha Polisi Zanzibar, ni mabovu. Kwa hili, namuomba Mheshimiwa Waziri, katika mgao wake wa magari, alifikirie sana Jeshi la Polisi Zanzibar hasa kwenye Kituo cha Polisi cha Mazizini kule Zanzibar. Kituo hiki kiko katikati ya wakubwa wetu, nikisema Wabunge, Mawaziri na Wawakilishi wengi wanaishi kwenye mtaa wa Mazizini. Ajabu ya kituo hiki hakina gari, hakina pikipiki wala ile baiskeli, kwa kweli namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamishna wa Zanzibar, wafanye jitihada za kukipatia kituo hiki usafiri japo wa pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea nije kwenye makazi. Kwa kweli Askari wetu wana makazi duni yasiyoridhisha, japokuwa nimeona katika hotuba ya Waziri, ameeleza pale Ziwani Zanzibar atajenga nyumba tatu ambapo kila moja itakuwa na koo 240, kwa kweli bado haitoshi. Itasaidia tu lakini bado kidogo kwani Askari wengi waliofanya kazi Zanzibar wengi wao wanaishi kwenye boma hili la Ziwani na kutoka kwenda kufanya kazi nje. Kwa kweli ninaomba katika awamu ya pili ya majengo yako haya Mheshimiwa Waziri, uwazidishie Askari wa Zanzibar nyumba za kuishi Askari na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, niwapongeze wachezaji *netball* wa Polisi ambao hawa ni wanaume wa Polisi waliocheza *netball* na kupata ushindi kwa mara ya saba, wanaleta kombe Tanzania. Kila wanapokwenda ikiwa nje ya nchi au ndani ya nchi, vijana hawa wanashinda na kupeperusha bendera ya Tanzania nchi za nje. Sasa ninachomwomba Mheshimiwa Waziri, hebu wafikirie hawa vijana, wameshaleta kombe Tanzania mara ya saba na wameshapeperusha bendera ya Tanzania na wameiletea sifa Tanzania, kwa kuwapa tuzo au kuwatambua kama tunavyowatambua wachezaji wengine wanapokuja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Waziri, naomba vijana hawa nao watambuliwe na waenziwe kama wanavyofanyiwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ajira kwa Zanzibar. Mara nyingi inapoletwa ajira ya Askari kwa Zanzibar utasikia wanatakiwa wanawake 10 wanaume 200 au wanatakiwa wanawake 20 wanaume 400, kwa kweli bado wanawake hamjawatendea haki. Angalau mnapoajiri wanaume 200 mngeweka wanawake 100, lakini ila siku zinapoletwa ajira kwa Zanzibar utaona wanawake tuna manung'uniko makubwa kwani kasma inayoletwa inakuwa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye ajira hiyohiyo, juzi tu kulikuwa na ajira sehemu ya ufundi, cha kusikitisha watu wetu wote waliotoka Unguja, Pemba, walikuja Bara kuja kufanya mitihani ya majaribio, matokeo yake vijana wote ambao wana vyeti wamekosa, wote waliochukuliwa ni vijana kutoka Tanzania Bara. Kwa hali hiyo, tunamwomba sana Mkuu wa Jeshi la Polisi, zinapotokea ajira kama hizi za ufundi, aidha wa kushona cherehani, wa kushona viatu, wa uashi, ikiwa seremala, nafasi hizi ziletwe moja kwa moja kwa Kamishna wa Zanzibar. Yeye mwenyewe ndio atakayeweza kujua achukue mafundi wangapi ili awapeleke kwenye ajira Moshi. Tunaomba sana hili, nalisisitiza kwa ajira ya mafundi kule Zanzibar safari hii mmetupa mtihani mkubwa sana kwa watoto wetu wanavyopita wakilia mitaani na wana vyeti na wanapita wakisikitika kwa nini wote basi wakose, kweli vyeti vyote vile walivyokuwanavyo havifai? Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, hili suala alichukulie kwa umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kasma ya mafuta inayotolewa Zanzibar, ni ndogo sana, haikidhi mahitaji ya miezi mitatu wanayopewa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ya kwanza au ya pili?

**NAIBU SPIKA:** Ya kwanza!

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wewe ndio umepanga bajeti ya 2009/2010, ulifikirie sana Jeshi la Polisi Zanzibar na hii kasma ya mafuta mnayoipa. Kwa kweli kasma ya mafuta inayoletwa Zanzibar ni ndogo, haitoshi kwa sababu inatumika kwa Mikoa yote mitano ya Zanzibar, kwa hali hiyo, naomba hili nalo Mheshimiwa Waziri, ulifikirie kwa makini sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wale Askari waliostaafu, ambao wamekufa, jamani wapatiwe malipo yao kwa haraka. Inasikitisha, kuna Askari wamekufa tangu mwaka 2000 mpaka hii leo mwaka 2008 malipo yao hawajalipwa, sasa sijui tatizo liko wapi, tatizo liko kwenu Jeshi la Polisi au tatizo liko wapi au Hazina? Naomba Mheshimiwa Waziri na hili nalo ulitilie mkazo kwa Wanajeshi waliostaafu Zanzibar pamoja na waliokufa. Naomba sana suala hili Waziri, uliingilie kati ili watu hawa wapate haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni hospitali tuliyokuwanayo Ziwani Zanzibar. Haspitali hii inahudumia Mikoa yote mitano ya Zanzibar, inahudumia na raia waliokuwa karibu na kambi ya pale Ziwani, tunachokiomba kwako Mheshimiwa Waziri, tunaomba Daktari mtaalamu aje pale ili kusaidia, tunao madaktari lakini wengi wao sio wataalamu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, ukishirikiana na Mkuu wa Jeshi la Polisi, katika kitengo hiki cha hospitali ya Ziwani, tunaomba tupatiwe Daktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kutoa mchango wangu katika kuchangia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii na viongozi wengine wote wakiwemo Makamishna wa vikosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yangu itaelekea hasa kwenye Jeshi la Polisi na kidogo nitakwenda kwenye Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninaanza na posho ya Jeshi la Polisi. Vijana wetu wa Polisi wanalalamika hawaelewi posho zao. Inawezekana wanapewa, lakini hawako wazi yaani hawayaelewi. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri awaagize watendaji wa Jeshi la Polisi yaani viongozi wa Jeshi la Polisi wayaweke wazi, mshahara upi, posho ipi, posho hii ipi na posho hii lipi.

Kwa mfano, inasemekana kuna kitu kinachoitwa *Rest Assistance* lakini Askari anakwambia mimi nina umri wa miaka kumi ya kazi sijawahi kuisikia posho hiyo, yaani sijawahi kupata posho hiyo. Itakapokuwa ni kweli basi tunamdhulumu. Lakini inawezekana sio kweli kwa sababu hajaeleweshwa tu kwamba hii ndiyo ipi na hii ndiyo ipi.

Aidha, vilevile katika suala la maposho wanapofanya kazi za *operation* kwa mfano kule kwetu Zanzibar wanapangwa kwenda kwenye mahoteli, *beach* huko wanafuatana na *commission* za utalii, wanastahiki kwa kazi hizo maalum wapate posho ya *operation*, lakini posho hizo wanazikosa. Kuna posho nyingine kama vile posho ya uhamisho kutoka Mkoa kwenda Mkoa, kutoka Wilaya kwenda Wilaya haya pia vijana wetu Polisi wanalalamika kuwa hawazipati hawa Askari wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aagize Makamanda wetu waziweke wazi, siwatetei moja kwa moja kwamba hawapati, lakini wanalalamika kuwa hawapati. Inawezekana inakuwepo katika *package* ya mishahara yao, lakini haina tofauti na wakaeleweshwa kuwa mshahara wako ni huu *scale* yako ni hii na posho yako inayokustahilia ni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni suala la elimu. Kwa hapa naomba sana ninukuu maelekezo ya Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika ukurasa wa 136 Ibara ya 111 (a), ilani inasema hivi, naomba kunukuu: "Katika Kipindi cha mwaka 2005/2010 Serikali za CCM, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitaendelea na utekelezaji wa majukumu yafuatayo kwenye sekta hii:-

1. Kuendeleza Sera ya CCM ya kuwa na Majeshi madogo ya ulinzi wa nchi na usalama wa raia yenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa," Mwisho wa kunukuu.

Sasa hapa nakusudia kuzungumzia taaluma. Taaluma ina maana kubwa na pengine kwa sababu Mheshimwa Waziri ni Mwanasheria, inawezekana akaichambua vizuri zaidi. Lakini ninachokusudia kuzungumza ni kuwa vijana wetu wanalalamika wanamaliza wakati mwingine Askari wetu *form four* wanajiendeleza wanafanya *A-Level* vizuri, wanafaulu kuingia Chuo Kikuu lakini wanazuiliwa. *AGP* ametoa toleo la kuwa wasiendelee kwenda kwenye vyuo vikuu. Sasa ilani inasema tutaboresha vikosi vyetu kwa taaluma, unapomzuia Askari ambaye amefanya vizuri *O-Level* na *A-Level* ana *apply* Chuo Kikuu anakubaliwa, lakini Jeshi linamzuia, hapo inakuwaje?

Tunaposema taaluma inakusudiwa nini? Ni ile shoto kulia ya Moshi na taaluma nyingine tu za kiaskari au na hiyo ni sehemu ya Taaluma? Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri kesho tukijaaliwa utakapokuja ku-*wind up* hili nalo tuwekee wazi ili tuwafahamishe vizuri vijana wetu. *(Makofi)*

Aidha, wengine wanakwenda kwenye *Medical Course* kutoka Upolisi, lakini sasa hawapati *support* yoyote ya masomo yao ndani ya Jeshi, wakati ilani nayo inasema tutaboresha majeshi yetu kitaaluma. Sambamba na hapo, nagusia vyeo vya Askari wetu. Nampongeza sana *Inspector General,* hivi karibuni ametoa mafunzo kwa vijana wetu wengi sana na Mheshimiwa Waziri umetusomea hapa zaidi ya Askari 10,000 wamepata mafunzo, wamepata vyeo, lakini vyeo vyenyewe aliyekuwa mtupu amekwenda kwenye Koplo, aliyekuwa Koplo amekwenda kwenye Usajenti, vimemalizia hapo. Kutoka hapo vyeo vya Polisi vinakuwa vigumu sana tena sana, Askari wetu wanafika hatua ya kustaafu tunawasibu kwenye Mabunge, wanasifiwa na Wizara lakini vyeo hawapati. Sasa hizo sifa gani zinakuwa? Mtu unamsifu lakini kumtunza humtunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kupitia Wizara hii naomba haya na ninadhani siyo Polisi tu, hata Magereza na kwa sasa vikosi vyote vya Uhamiaji, *Fire Brigade*, zote hizo inaonekana upatikanaji wa vyeo unakuwa mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni vyema sana Mheshimiwa Waziri ukatuambia au Jeshi la Polisi likatuambia kuna *ratio* gani hasa tunasika kama raia kadha sina uhakika lakini kwa mfano raia 300 walindwe na Askari mmoja kwa mfano, lakini Jeshi lenyewe linaelewa. Lakini je, katika Askari wangapi walio wazuri, wema, wanahitaji vyetu gani viwepo? Lakini pana Askari 300 katika kituo hapo Bosi wao ni yule *Sir Major*, hapana mwenye jiwe moja, hapana mwenye jiwe la pili wala hapana mwenye jiwe la tatu. Kwa hiyo, nadhani pia hili nalo lingezingatiwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa tatu ni mafao ya ajali kazini. Mheshimiwa Waziri hili hatulitekelezi katika majeshi yetu nasema katika majeshi yetu, lakini nitatoa mfano mzuri katika Jeshi la Polisi. Katika mwaka 1996 nilikuwa nikifanya kazi katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kaskazini Unguja kama ni mmoja katika Maofisa wakubwa pale ofisini kwake. Tulitembeza Mwenge na Mwenge wetu ulipata ajali Askari mmoja akafariki, Askari mwingine akakatika mguu, basi mpaka leo mwaka wa 12 hajapata mafao yoyote.

Askari huyo ana Na. E4807 anaitwa Khamis Makame anafanya kazi katika Kituo cha Mkokotoni, inasikitisha sana. Inasikitisha zaidi kwani kuna Waziri mmoja wa Mambo ya Ndani katika Mawaziri waliopita alikwenda Zanzibar akazungumza na Askari Polisi akadai haki zake akapata jibu la maajabu sana akaambiwa aha! hizo pesa zenyewe chache sana huko kudai unahangaika bure. Sasa hayo sio maneno mazuri hata kama ni Sh. 10,000/= kwa 1996,

basi Mheshimiwa Waziri hivi sasa huyu *Regard* kama ni shilingi milioni 10 na umpe mtu huyu.

Nitaunga mkono hoja kwa sababu sina desturi ya visindo, ni mpole na kuheshimu sana Mheshimiwa Waziri inawezekana ndugu yangu na Naibu Waziri pengine ni Baba yangu na *Inspector General* ni kaka yangu na kwa sababu umelipokea na kwa huruma yako nadhani utalitazama katika mtizamo mzuri ili huyu kijana wetu aone kama anastahiki kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia hizi kazi hasa za *Police Marine*, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Tumbatu, Tumbatu yenyewe hasa ni sehemu ya kisiwa, wanakwenda Viongozi wakubwawakubwa kama Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Zanzibar, Mawaziri Wakuu na wakubwa wote. Lakini *participation* ya *Police Marine* hatuioni nako ni baharini, wanakwenda Polisi wa kawaida tu sasa hii *role ya Police Marine* ni nini ? Au iko bandarini tu ? Kama iko bandarini tu basi, ibadilishwe jina iitwe *Port Police* au iitwe vingine vyovyote. Lakini kama ni *Police Marine* mle mahali mwingine namo tunaihitaji sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wale wanaosema Askari wetu hasa wakubwa wa Askari hawapendani au hawawapendi wadogo. Askari anafanya kazi nzuri sana kwa miaka 20 lakini dakika 10 tu anayofanya kosa anaachishwa kazi hapo maana yake hatupendani. Mimi nadhani hiyo si nzuri na tufike pahali tuseme kuwa kosa la dakika 10 lisimuachishe kazi Askari aliyefanya vizuri kwa miaka 20, aadhibiwe kwa kiasi cha kuadhibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nakwenda sasa kwenye uhamiaji ambapo kwa kule Zanzibar uhamiaji inafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA :** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Ali Juma Haji na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji ajiandae ingawa alichelewa kuomba.

**MHE. ALI JUMA HAJI :** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaaliwa afya njema kuweza kusimama hapa leo na kuweza kuchangia hii hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake hii nzuri tu pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Makamishna wote pamoja na watendaji wote ambao kwa namna moja ama nyingine waliweza kuchangia kukamilisha hotuba hii ambayo leo iko hapa mbele yetu, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza ni kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi yake nzuri inayofanya Bara na Visiwani au Bara na Zanzibar. Lakini niishangae Wizara labda wenyewe baada ya kazi nzuri Askari tunawapongeza kwa kazi wanazofanya vizuri lakini wanapofika wakati wa kustaafu Askari hawa wakati mwingine wanadhalilika sana baada ya kustaafu wanakuwa hawana mbele wala nyuma, hawana mafao yoyote yanayowasaidia na hii ni kutokana na mfumo huu ambao mimi nauita ni wa kibaguzi wa mambo ya *pension* na *gratuity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka juzi nilichangia hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani na nikatoa mifano mingi na mmoja uliokuwa umeathiri zaidi nikatoa kwa Askari ambaye ninamfahamu alifanya kazi kwa miaka 32 na alipostaafu alipata kiinua mgongo cha shilingi milioni 1,200,000/= na hiyo nikatoa ushahidi na mpaka Mheshimiwa Spika akanitaka

nipeleke vielelezo kwa Waziri aliyekuwepo wakati ule na nikampelekea lakini nikajibiwa kwa mdomo tu hivi kwamba kutokana na Sheria hastahili kurekebishiwa kwa sababu aliingia katika mfumo wa Sheria na nilikubali hivyo kwa sababu ni kweli Sheria ilikwishampita lakini tukasisitiza sana kwamba mfumo huu wa kuulizwa Askari baada ya kutimiza miaka 12 ya kazi unahitaji mfumo gani wa kiinua mgongo yaani bakshishi ama pensheni tukasema haufai ni wa kibaguzi kwa sababu nimesema ni wa kibaguzi unadhihirisha wazi ubaguzi wake.

Mfumo huu unawaumiza Askari wa chini tu tumesema sana lakini akishafikia cheo cha *Inspector*, yaani Msaidizi Mwandamizi mfumo huu unamtoa moja kwa moja. Sasa kama yeye toka chini kachagua mfumo huu wa kusema kwamba mimi nataka kiinua mgongo, lakini akifikia cheo cha *Inspector* anatoka moja kwa moja na kuingizwa katika mfumo wa *Pension*. Ni sababu gani hasa hebu tujibuni ni sababu gani hasa kwa nini yeye atolewe moja kwa moja na yule Askari wa chini abakishwe pale pale, unawadhalilisha.

Wenzangu hapa waliotangulia walisema kwamba Mheshimiwa Waziri ajiandae kwamba kupokea watu ambao wanaathirika sana na mfumo huu, lakini nasema asijiandae, wapo sasa hivi hawana mbele wala nyuma, ushahidi tunao. Huu mfumo nina wasiwasi kama unapingana hata na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Labda kwa kusema hivyo ninukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halafu yake tuangalie na huu mfumo kama kweli bado unafaa kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kunukuu, katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sehemu ya tatu ambayo inazungumza haki na wajibu muhimu, Kifungu Namba 13 (i) na (ii) nasoma hivyo tu, kinasema kwamba:

(i) “Watu wote ni sawa mbele ya Sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya Sheria.”

(ii) “Ni marufuku kwa Sheria yoyote iliyotungwa na Mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taswira yake.”

Sasa hapa nasema huu mfumo ni wa ubaguzi kwa sababu kidhahiri hauonyeshi ni wa ubaguzi lakini kitaswira unaonyesha ni wa kibaguzi. Kwa sababu wa dhahiri wanapata kiinua mgongo chao lakini taswira inayowapata hawa hii ni dhahiri ni wa ubaguzi hautufai, tunaomba huu mfumo urekekebishwe na Waziri wakati ule alisema kwamba anakwenda kufanyia marekebisho *PGO*, lakini hadi leo hii hakuna chochote na kilichoshangaza zaidi hivi juzi tu kaka yetu hapa Naibu Waziri alijibu swali Na. 27 nafikiri Mkutano uliopita, alijibu swali la Mbunge wa Fuoni akajibu kama ifuatavyo, naomba pia ninukuu kidogo, sitasoma majibu yote lakini nitasoma sehemu tu inayogusia hicho ninachokitaka: *(Makofi)*

“Jeshi la Polisi lilichukua hatua ya kukusanya maoni ya watu mbalimbali wakiwemo Askari na kugundua kwamba mfumo huu bado unafaa kutumika kwa manufaa ya Jeshi lenyewe na Askari pia”

Hii mimi inanishangaza, hili Jeshi la Polisi litapata manufaa gani? Hebu Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie wazi manufaa linayopata Jeshi la Polisi kwa kutumia mfano huu ambao unaumiza Askari. Hili jeshi lenyewe linapata manufaa gani ? Tunataka tuambiwe hapa ili tujue. *(Makofi)*

Halafu inavyoshangaza ni kwamba katika majibu haya Naibu Waziri alisema kwamba alikusanya maoni ya wananchi mbalimbali. Nili ni jambo la Askari, tunategemea mwananchi

atupe maoni gani ya Askari? Hawezi kutupa! Hata mimi Kaka yangu binafsi aliwahi kuniuliza wakati sijawa Mbunge, akaniambia bwana mimi nakaribia kustaafu, lakini kuna mfumo kule wa *pension* na kiinua mgongo, nichague upi? Mimi kwa majibu ya haraka nikamwambia chagua kiinua mgongo kwa sababu nimeshazoea uraiani ukimaliza kiinua mgongo unapata *lump sum* halafu unaendelea na *pension.* Kumbe sivyo, kaumia sana na ninajuta. Nimemuathiri na mimi sijui. Kwa hiyo, kwanza elimu hakuna ya kutosha kwa maaskari wetu, inaonyesha elimu haitolewi vizuri na wao wanaingia katika mfumo huu unawaangamiza. Kwa hiyo, naomba mfumo huu uondolewe, tena usiwe na mjadala, faida gani na Serikali ina kigugumizi gani? Hebu tuelezwe ina kigugumizi gani? Unafaa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini sijui kama mnakaa na Maaskari wa chini na nina wasiwasi mkubwa kwamba huwa mnakaa na maaskari wa vyeo vya juu ambao wao ndiyo wananufaika, hawatakwambieni wanaoathirika ni Askari wa chini. Sasa mimi naomba kama kweli mmekaa na Maaskari hasa kule Zanzibar, huu ni wa nchi nzima, lakini ninasema kule Zanzibar ndiyo wanaotuagiza. Sasa mmekaa nao lini na wapi? Tuelewe! Kwa sababu watakuwa wanasema uongo kama kule wanatuambia hautufai na huku ninyi wanawaambia kwamba unatufaa hilo ningeomba nipate maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninalopenda kuchangia ni kuhusu makazi ya Askari, mimi nampongeza Waziri kwa juhudi zake anazofanya kuhusu makazi ya Askari. Lakini nimeangalia katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kwamba kuna nyumba ya Kamanda tu ambayo inajengwa mwaka 2007/2008, nikaenda mbele zaidi nikasema labda nyumba za makasi ya Askari zitakwenda 2008/2009, hamna kitu. Sasa tunategemea hawa maaskari wakae wapi? Ukipita kituo kile cha Mkokotoni Waziri anakijua, ukipita barabara unamwona Askari anaingia Chumbani mlango huo huo! Sasa jamani Maaskari wetu tunawapeleka wapi? Tuwasifu tu kwamba wanafanya kazi vizuri! Lakini katika maslahi yanakuwa sio mazuri!

Mimi naomba na nyumba za Maaskari katika Mkoa wa Kaskazini nazo zijengwe ikiwa mwaka huu umepita, basi mwaka 2009/2010 tukijaaliwa atakayekuwa yupo katika Bunge hili, basi tuone makadirio yao katika nyumba za Maaskari kwa sababu tunajua kwa mwaka huu haitawezekana lakini tunawaomba sana mwaka 2009/2010 Mheshimiwa Waziri tuone bajeti yao, nyumba za Maaskari Mkoa wa Kaskazini Unguja.

La tatu, pengine litakuwa la mwisho kabla sijapigiwa kengele ni kuhusu usafiri. Ni kweli usafiri wa Maaskari wetu unakuwa duni sana. Mimi ninavyofahamu kunakuwa na gari ambalo pengine linakuwa la Kamanda, sasa gari la Kamanda kama kutatokea tukio la haraka na Kamanda pengine anatakiwa aende Makao Makuu kuna kikao mimi nadhani Kamanda atakimbilia Kikao. Sasa viwekwe vyombo vya usafiri kwa ajili ya utendaji kazi mbali na gari ya Kamanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda la mwisho zaidi ni kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamishna kuhusu vyeo. Amejitahidi kweli na hata sisi tulikuwa tunaona vijana wanatuagaaga tu tunakwenda huko, lakini vyeo vile vya Koplo na Sajenti. Sasa tunachoomba ni kwamba pawe na mwendelezo isiwe tena anakaa nacho mpaka kinachanika palepale hata kubadilishiwa kile cheo pia ni taabu achilia mbali kupandishwa. Kwa hiyo, tunaomba vikuzwe tena siyo kubakia palepale. Hili tunaliomba sana, wamejitahidi sana, tunawapongeza kwa hili kwa mwaka huu. *((Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa juhudi inayofanya kwa kupambana na wahalifu wengi, lakini ningeomba ifanye juhudi kwa hawa wauaji wa maalbino. Kwa kweli inasikitisha sana, Jeshi la Polisi kama limeweza kupambana na uhalifu

mkubwa wa majambazi hawa wanaovamia mabenki watashindwaji kupambana na hawa wauaji wa Maalbini? Kwa kweli ipo haja sasa hivi kuvalia njuga, kama IGP umeshaanza hii kazi tunaomba uiendeleze kwa juhudi kubwa, kama hujaanza basi uianze kwa nguvu zote tuone hawa watu wanakamatwa na wanafikishwa kwenye vyombo vya Sheria na kama atakamatwa mtu ambaye ana udhibitisho kukutwa kwa mfano tunaona kwenye magazeti kwamba kakamatwa na mkono wa Albino au mguu, leo hawa wanaambiwa leo lete mkono au mguu lakini kesho atakuja kuambiwa ukila nyama ya Albini utapata utajiri zaidi, na Albini watasakwa kuliko Kitimoto. Tunaomba hili jambo lidhibitiwe vikali sana kwani tutafika katika hatari kubwa na inasikitisha. *(Kicheko/Makofi)*

Mimi juzi nimemsikia yule Mama ambaye mtoto wake amekatwa mguu na mimi machozi yalikuwa yananitoka namsikiliza alivyokuwa akihadithia. Jeshi la Polisi tunaomba livalie njuga haya mambo yakomeshwe na tusikie hasa yanavyokomeshwa kama yanavyokomeshwa mambo ya ujambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo kwa sababu sijakuwa mzoefu sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana, lakini umemaliza dakika zako. Mheshimiwa Haji Juma Sereweji.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia. Kwa niaba yangu na niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naisifu hotuba ya Mheshimiwa Waziri, safi, nzuri na inayoeleweka. Halafu hakuna asiyejua hata mmoja kwamba Jeshi la Polisi ni Jeshi ambalo linafanya kazi sana na linafanya kazi nzito kwa sababu kukiwa na msiba, Polisi lazima wawepo, kukiwa na starehe Polisi wawepo, kukiwa na ghasia Polisi wawepo na kukiwa na vita wao ni watu wa kwanza kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, labda kidogo tu niunganishe na msemaji mwenzangu aliyechangia hivi sasa. Mimi nashangazwa sana na Mkataba huu wa kiinua mgongo na pensheni na sisi Wabunge ndiyo tunaosikiliza kero na yale yote ambayo wananchi wetu yanawatatiza. Lakini nashangaa kwamba Viongozi wetu waasisi, baada ya kupata Jamhuri tu wakasema tutayachukua yale yote mazuri waliyoyaacha Wakoloni na tutayaboresha, lakini yale yote ambayo sio mazuri ndani ya wananchi wetu na nchi yetu tutayaondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana kuona mpaka leo tunapiga kelele lakini Jeshi la Polisi wanashindwa kabisa kuyaondoa yanayowakera askari wetu. Lakini yale mabaya waliyoyaacha wakoloni kwa Maofisa yote yameondolewa. Hii inaonyesha wazi kwamba askari wa chini mpaka leo hawafanyiwi haki. Nimemaliza, meseji imefika. Naomba hili liondolewe ili Jeshi letu la Polisi liende kisasa na hasa ilivyokuwa nchi yetu inafuata haki za binadamu na utawala bora. Hivi leo vipi utamtuma Askari Polisi kuanzia mwaka mmoja mpaka miaka thelathini asipate pensheni, utawala bora uko wapi, haki za binadamu ziko wapi na kwa nini tusiondoe haya. Natumaini wanaohusika wamesikia na inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nataka kutoa jawabu dogo kuhusu silaha au vitendea kazi ambavyo wanakabidhiwa askari wetu. Nasikitika Mheshimiwa mmoja wa Kambi ya Upinzani alichangia kwa kusema kwamba, gari la maji machafu lisingenunuliwa

wakati kuna nyuklia zinatengenezwa katika nchi mbalimbali na anayetengenezewa sio nguruwe, tembo wala farasi, wanatengenezewa binadamu watakaofanya mabaya na hii silaha ya maji machafu ni sawa sawa na bomu la machozi. Panapotokea ghasia unamwagiwa maji machafu, unajipangusa, unakwenda kwako unaoga, yamekwisha. Tena ni silaha ndogo tu ambayo unamwagiwa maji machafu ambayo yanakuwasha, basi unaondoka eneo la tukio na maji haya hayadhuru kuliko wangetumia silaha kali. Kwa hiyo, maji machafu ni silaha ya kawaida na nyepesi inayokwenda na wakati na haki za binadamu na utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge yeyote atakayesema kwamba, kusiwe na silaha katika jeshi hata wanajeshi wenyewe wataona hatuwatendei haki na hasa jeshi la sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu uhamisho. Leo natoka hapa na ndiyo nikawa na hamu sana ya kuchangia. Nimepata meseji inayosema kwamba karibu askari mia tatu watahamishwa Zanzibar na wengine wameshahamishwa. Mpaka sasa ni mwezi mmoja na nusu hawajapata mishahara yao, hawajapata posho wanaambiwa mjitazame hivyo hivyo, kutoka Zanzibar kuja Mikoani Tanzania Bara, hivi askari huyo atajikimu vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naheshimu sana ule msemo na sheria za kipolisi zinazosema kwamba, fanya kwanza halafu lalamika, *do and then complain*. Lakini ule umeletwa kwa wakati ambapo hakuna amani, askari wamekwisha unaambiwa umetoka lindo, kakamate lindo, pale hutolalamika kwa sababu unajua kwamba nisipokwenda kuna matatizo, lakini katika nchi yetu hakuna vita. Sasa utamwondoaje askari bila kumpa posho, mshahara wake, hujui nyumbani kaondokaje, anaondoka anakuja Tanzania Bara, huku mgeni, akishawishiwa vyovyote, atashawishiwa na atapokea rushwa ili ajikimu. Kama hilo kweli limetokea waliobakia warekebishiwe mishahara yao, posho zao halafu waje kukamata sehemu walizorekebishiwa.

Mheshimiwa Spika, naelezea kuhusu vitendea kazi hasa magari au gari vipando vituoni. Askari wetu kazi zao haziendi vizuri kutokana na kukosa vitendea kazi ili kufuatilia mahali ambako vitendo vya kihalifu vimetokea. Mara nyingi wananchi huwa wanalalamika na sisi Wabunge unafika wakati tunawapakia askari kwa kuwasaidia, unafika kituoni, mafuta hakuna gari ipo. Lakini juzi imetoka kauli kutoka kwa Waziri akisema kwamba, hakuna ruhusa ya mwananchi yeyote kutoa ruhusa au pesa za mafuta kumpa askari kufuatilia jambo lolote lililotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuuliza: Je, kweli jeshi la Polisi limejidhatiti kuweka mafuta petroli au dizeli ya kutosha vituoni ili askari wetu waende vizuri. Kwa sababu tusikae hapa Bungeni kusema hayo wakati huko chini bado hayajateremshwa. Kwa hiyo, naomba vitendea kazi na magari yawepo katika vituo vyetu kwa sababu kama tukio linatokea lakini askari akikawia kufika ushahidi na waliofanya makosa yale wote wanatoweka, ushahidi unakosekana na kama yupo raia aliyekuwa tayari kutoa ushahidi hawatomkuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna shaka kwamba nimelaumu lakini sitoweza kulaumu moja kwa moja kwa sababu Jeshi la Polisi ni safi, viongozi wao wakiambiwa wanasikia na ujambazi ulikuwa mkubwa sana, sasa haupo. Kwa hiyo, nawapongeza.

**NAIBU SPIKA:** Wewe mwenyewe ulikuwa Polisi! *(Kicheko)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napongeza kwa dhati kabisa utendaji wa Polisi hasa sehemu za malindo, trafiki na sehemu zote

zinazohusika, lakini vilevile naomba *patrol* ya trafiki na askari wa kawaida izidi kuimarika na hasa katika Miji Mikuu kama Zanzibar, Dar es Salaam, Arusha na Mwanza kwa sababu ndiyo sehemu zinazotokea matukio makubwa kila mara, lakini inasikitisha kuona kwamba hivi sasa hata mpanda baiskeli anamdhalilisha Askari wa Polisi kwa sababu hana mbinu yoyote ya kumkamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu sio wakati wa kufukuzana kwa miguu, huu ni wakati wa kufukuzana kwa vyombo vya usafiri. Sasa utakuta trafiki hana hata pikipiki, makosa yanatendeka hana la kufanya, hakuna pikipiki za doria, lakini hata askari ukimkuta usiku katika lindo hata tochi au kurunzi atafute yake wakati zamani askari akiwa katika lindo lazima ahakikishwe anayo tochi inayoingia dawa sita, nne au tano ambayo nayo peke yake ilikuwa ni silaha kwa sababu ukikaa kwenye lindo au *patrol* peke yake, ikionekana askari akipita sehemu moja mara mbili au tatu akaenda sehemu nyingine, basi hapo hata mtu atakuwa na wasiwasi kwamba pengine hapa yupo askari, hafanyi uhalifu wowote. Lakini hata ukiwa na tochi ukimulika tochi kule kama kuna mhalifu, basi atarudi nyuma na hatofanya uhalifu. Kwa hiyo, vyombo vidogo vidogo naomba navyo viwepo ili askari wetu wafanye kazi kiuhakika na kileo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo kwa dhati kabisa naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu wataala, aliyenijaalia uzima na afya njema mpaka nikapata nguvu ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kulipongeza Jeshi la Zimamoto kwa kazi yao nzuri katika kuhakikisha kwamba maisha ya watu pamoja na mali zao yako salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko na kuna jambo ambalo halipendezi na inafaa kidogo liangaliwe. Jeshi la zimamoto wametoa namba zao ili pale ambapo kuna tukio lolote la moto wapigiwe simu, lakini kuna baadhi ya watu wanatumia namba hizo vibaya kwa kuwapigia simu Jeshi la Zimamoto, wakifika mahali au katika eneo fulani, basi kunakuwa hakuna lolote, wanaambiwa njoo mbele tukio lipo, wakifika simu inazimwa. Hiyo ni miito ya moto ya uongo kwa watu wa zimamoto. Kupitia Bunge hili ningewaasa wananchi wote wa Tanzania wanaotusikiliza kwamba, ni vyema tutumie namba hizi vizuri ili pale ambapo tukio likitokea kweli, basi wenzetu wasije kufikiri ni masihara. Tunajua kuna utani na masihara kwa makabila mbalimbali lakini sio vizuri kuingiza utani kazini. Hilo ilikuwa ni dibaji yangu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengine kwamba baadhi ya nyaya zinazoingizwa nchini zipo chini ya kiwango ambazo pia zinachangia katika kusababisha moto. Naomba mamlaka husika iangalie suala hili, vifaa vyote vya umeme zikiwemo hizo nyaya zinazoingizwa nchini kutoka nje zilizolalamikiwa sana juu ya matukio haya ya moto viangaliwe kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko yote, sakata la manunuzi ya magari tisa ya zimamoto kinyume na taratibu ambayo ilipelekea wenzetu wa miundombinu wachelewe kuyasajili magari haya, hili ni tatizo kubwa. Magari haya yalinunuliwa kwa fedha ya Serikali Kuu baina ya mwaka 2003 – 2006, ni magari ya Halmashauri tisa. Kila gari liligharimu Sh.

300m/= mpaka Sh. 350m/=. Magari haya yalinunuliwa kama mapya lakini miundombinu walikataa kuyasajili magari haya kwa sababu waliona hayapo katika ubora au kiwango kinachostahili na wameyasajili kama ambayo yametumika *(used).*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo na hapa kuna utata, kuna haja ya kufanyiwa kazi. Magari ya Manispaa na Hamashauri zaa Songea, Mtwara-Mikindani, Temeke, Ilala, Moshi, Morogoro, Kigoma, Kibaha na Dodoma. Magari haya tisa ni kwamba miundombinu walikataa kuyasajili kwa sababu waliona hayapo katika kiwango kinachostahili zaidi ya Sh. 2.9bn/= zimetumika ambazo ni kodi za walipa kodi, maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina pingamizi kabisa na wazabuni wetu lakini nina hofu na mashaka makubwa na makampuni ambayo yametengeneza magari haya ya zimamoto. Kuna makampuni matatu ambayo magari haya yametoka, Albert Zigla – Ujerumani, hiki ni kiwanda cha kwanza kabisa. Kiwanda cha pili ni *Continental Contract Service* cha Uingereza na cha tatu ni *National Fire Fighting Manufacturing* kutoka Dubai. Ndiko magari haya tisa ya zimamoto yalikonunuliwa na huko ndiko kwenye hofu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina wasi wasi na wazabuni wetu kwani wanajulikana *KERNEL Limited*, *ACHELIS Tanganyika Limited* pamoja na *COZY Traders*, wote wa Dar es Salaam, hawa ni wazabuni wazuri, ni wazalendo na waaminifu sina pingamizi nao, lakini hili ndio tatizo kubwa hivi sasa. Wizara inafahamu na hili ni tatizo la muda mrefu. Kwa nini muda wote Wizara imekaa kimya haituambii tatizo liko wapi. Sasa napendekeza kwamba, Bunge liridhike na liliridhie kuunda Kamati Teule itakayochunguza mwenendo mzima wa manunuzi ya magari haya ya zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nigusie kidogo Jeshi la Polisi. Kwa kweli nawapongeza, wanafanya kazi nzuri. Napenda nimpongeza *IGP*, Ndugu Said Mwema na Makamishna wote na rafiki yangu Kamishna Godwin Mtweve ambaye kwa njia moja au nyingine pale ambapo ukimpigia simu tu kama kuna tatizo la ujambazi basi haichukui muda analishughulikia. Hongera *IGP*, Makamishna wote na kwa namna ya pekee hongera Kamishna Goldwin Mtweve. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunawasifu lakini maslahi yao ni madogo. Posho ya nyumba ni asilimia kumi ya mshahara wake, inategemea na mshahara wake kwa sababu kuna baadhi ya askari ambao wanapata posho ya nyumba Sh. 18,000/=, wengine Sh. 20,000/= na wengine Sh. 30,000/=. Nadhani hii si posho ya nyumba bali ni posho ya chumba na askari kama binadamu wana familia, wana watoto wanne au watano tena wakubwa, hivi ndiyo kweli walale kwenye chumba kimoja, baba, mama na watoto wenye umri wa miaka kumi nne?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo, mtoto mkubwa sio vizuri kulala naye katika chumba kimoja. Nadhani utaratibu uandaliwe wa kuboresha posho hii ya nyumba kutoka asilimia kumi hadi asilimia thelathini ili tuepukane na aibu ya baadhi ya askari wetu ambao hawana uwezo wa kujikimu kulala kwenye chumba kimoja. Ni hatari kulala na watoto. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tuna tatizo hili askari wamekuwa wakilalamika na posho za usafiri pamoja na fedha za kupandishwa vyeo na pia kuna madeni makubwa ya wazabuni. Kwa hiyo, askari wanadai na wazabuni wanadai. Amesema Mheshiimiwa Khalifa asubuhi, jibu la madeni haya ni Sh. 5bn/= lakini Wizara au Serikali imeridhia kununua magari mawili ya kutuliza ghasia kwa Sh. 1.6bn/=, imepigwa kelele hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachogomba ni kwamba, tuna madeni mengi ya Sh. 5bn/=, kwa hiyo ni vema kwanza Sh. 1.6bn/= tungeitumia kuwalipa madeni yao Polisi, hiyo ndiyo hoja ya msingi na bado muda upo wa kununua magari hayo, kwenye Sh. 5bn/= ambayo tunadaiwa tukitoa Sh. 1.6/=, itabaki Sh. 3.4bn/=, hiyo ndiyo hoja ya msingi kwamba ni vyema kuanza kulipa madeni ya Polisi na hata kama tungekuwa hatulipi madeni ya Polisi tungenunua makoti ambayo risasi haipenyi *(bullet proof vest)* ili askari wajikinge wakati wakishambuliana na majambazi. Tusisubiri mpaka askari wakapigwa risasi wakafa, tukaandaa risasi ya kutoa machozi, alikuwa hodari, alikuwa mwenzetu, ameacha pengo, hicho ndio kinachogomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa ufafanuzi huo itaeleweka namna gani tunapinga kununuliwa kwa magari mawili haya ya kutuliza ghasia ambayo yana maji machafu na hakuna ghasia Tanzania, nchi hii ni ya amani kabisa, watu wanatulizana. Sasa ukisema magari ya kutuliza ghasia kidogo napata mashaka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nigusie kidogo kwenye posho ya chakula. Sh. 50,000/= ni kidogo sana, wastani wa Sh. 1,700/= kwa siku, kwa milo mitatu. Askari anatakiwa ajenge mwili amepewa Sh. 1,700/= kwa siku. Jamani askari huyu akanunue nini? Nadhani kuna haja ya kubadilika angalau hii posho ya chakula iongezeke angalau kufikia Sh. 150,000/=, chonde chonde kwani hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie sheria ya ndoa. Askari akiajiriwa anatakiwa asioe wala kuolewa kwa muda wa miaka mitatu, huku tukiwa na tatizo kubwa la maambukizi ya UKIMWI. Sheria hii ilipotungwa nafikiri kwa wakati huo ilikuwa ni muafaka, lakini nafikiri kwa sasa nafikiri imepitwa na wakati, inafaa irekebishwe. Ni vyema askari akiajiriwa awe na uwezo wa kuoa au kuolewa, nafikiri hilo litakuwa ni jambo zuri kabisa. Tusiiache hivyo, tukasema askari asioe wala kuolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nije kwenye msongamano wa wafungwa. Msongamano wa wafungwa unachangiwa na mambo mengi, kuna suala zima la kubambikizwa kesi, unapopita magerezani mara nyingi unapohoji, basi kesi nyingi zinakuwa ni za kubambikizwa na hasa kwenye vijiji na vitongoji *VEOs* na *WEOs* huko wamekuwa ni Miungu watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano mmoja, kuna Kijiji cha Mtanga, Kata ya Kagongo, Tarafa ya Mwandiga, Kigoma Vijijini kila siku kesi haziishi, ukiuliza tatizo ni nini ni kwamba wanakijiji wamekwenda kuhoji mapato na matumizi. Ukienda Kijiji kingine cha Kisingiri, Kata ya Ilola, Jimbo la Solwa, tatizo nini wamehoji mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana kwamba viongozi wakubwa wa Vijiji na Kata hawataki kuhojiwa namna gani mapato na matumizi ya Serikali yanakuwa. Hilo ni tatizo. Naomba Polisi waliangalie suala hili kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna adhabu kwa wezi wa mifugo. Ukienda magerezani unakuta viwango vya adhabu vinafanana, aliiba kuku mmoja miaka mitano, mbuzi kumi miaka mitano, ng'ombe ishirini miaka mitano. Naomba sheria hiyo irekebishwe. Hilo nalo ni tatizo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kutazama Kesi *(Case Flow Management Committee)* hazifanyi kazi, wanasema haziwezeshwi. Kwa hiyo, tunaomba ziwezeshwe, tuzipe fedha kikamilifu ili angalau wafungwa wa magerezani wapungue. Mpango wa *Parole* ambao wafungwa wa muda mfupi pia ufanyiwe kazi kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, penye mazuri na kasoro zipo, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuna matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwenye Fungu 28 – Jeshi la Polisi. Naomba ninukuu: "Masurufu yasiyotolewa maelezo ni Sh. 24,439,650 /=". Hili ni tatizo. "Idara ya Magereza, matumizi yasiyo na nyaraka na yenye nyaraka pungufu ni Sh. 7,987,500". Hili ni tatizo lingine. "Kuna upotevu wa fedha na vifaa kwa Sh. 4,840,756/=", hili pia tatizo lingine. "Kwenye Magereza, malipo bila idhini Sh. 101,616,291/"=. Hili ni tatizo, tunachopewa ni kidogo, kwa hiyo, ningeomba matumizi kwenye Jeshi la Polisi na Magereza yadhibitiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna malalamiko ya ubadhirifu wa fedha katika Zahanati ya Chuo cha Polisi Ziwani, tunataka tuthibitishiwe jambo hili kama lipo, hii haipo kwenye ripoti na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Tunaomba tupate ufafanuzi ya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu vitambulisho vya Taifa. Hili limepigiwa kelele mara nyingi na nadhani pengine lingeanzia katika Mikoa ya mipakani lakini tuanze uhakiki wa kuwajua ni nani raia wa Tanzania na nani sio raia wa Tanzania kwa sababu katika maeneo hayo watu wameoana wapo pamoja na wanasema wao hawajui mipaka ya wakoloni, wanachojua wao ni kwamba wameoana, wamezaliana, mjomba na shangazi. Wasiwasi wangu, tusije kupata viongozi ambao sio Watanzania na hasa tukielekea katika uchaguzi wa mwaka 2009 wa Vijiji na Vitongoji. Naomba tufanye uhakiki mwanzo kabla ya kutoa vitambulisho vya uraia tena tuanze kutoa katika Mikoa ya mipakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia suala la uhamiaji au uhamiaji haramu. Sambamba na hilo nigusie tu kwamba kuna baadhi ya maeneo hasa kule kwenye Mto Songwe baina ya Tanzania na Malawi, hakuna vituo vya uhamiaji. Kwa hiyo, wahamiaji haramu wamekuwa ni wengi sana. Waethiopia wanaingia kwa wingi na Wasomali wanaingia kwa wingi. Kwa hiyo, unakuta matatizo siku zote yanaongezeka. Tatizo ni kwamba, bado hakuna vituo vya uhamiaji, naishauri Serikali kuandaa mazingira mahsusi kabisa ya kujenga vituo vya uhamiaji katika maeneo ya Isingole Ileje na pia Kasimuro kule Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie kwa majengo yanayovuja au jengo la Makao Makuu la Kusini Pemba. Tumepiga makelele mara nyingi kwamba jengo hili ni bovu, linavuja, lifanyiwe ukarabati, lakini kila siku tunaambiwa mambo yako mbioni, nia ni njema, mchakato unaendelea, jengo litakarabatiwa. Lugha hizi zinatosha naomba chonde chonde Mheshimiwa Waziri na Naibu wake watuangalie katika hili. Jengo lile linavuja hatari ikinyesha mvua, ghorofa ya kwanza, ghorofa ya pili na *ground floor* kunavuja hatari. Kwa njia moja au nyingine nafikiri Mawaziri mmewashauri, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chakula kimepikwa kwenye eneo langu, nimeonja lakini mambo madogo madogo niliyokuwa nayo ni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia kusimama hapa na kutoa mawazo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP*, Mkurugenzi, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amewasilisha bajeti yake, ukweli ni nzuri, inatia moyo, ina ukweli mwingi. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake ukurasa wa 11, amezungumzia masuala ya ujenzi. Napenda niishukuru Wizara kwa sababu bajeti iliyopita nilizungumzia sana masuala ya nyumba za Polisi Ziwani na Mawaziri waliokuwa wakati huo waliniahidi watatujengea nyumba kumi lakini naelewa wazi ahadi ya Serikali inaanza miaka mitano. Sasa katika kipindi hiki napenda niwashukuru sana kwa ujenzi wa nyumba tatu ambao unaendelea vizuri. Kwa hiyo, naamini hata tukifika mwaka 2010 angalau zinaweza kuwa sita, kwa jitihada hii iliyoanza vizuri nategemea angalau tunaweza kupata sita ili kupunguza usumbufu wa makazi ya maaskari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Kamishna wa Polisi Zanzibar akishirikiana na *RPC* Mkoa wa Mjini. Ukweli katika Mkoa ambao ulikuwa na matatizo ya mambo mengi ya kihalifu, basi Mkoa wa Mjini kwa Zanzibar ulikuwa unaongoza kwa sababu mjini ndiyo mjini lakini kwa kazi nzuri waliyoifanya wameweza kupunguza kwa kiasi kikubwa sana na naomba jitihada hizi ziendelee ili watu waweze kuishi vizuri, ikiwa kama ni moja ya kazi zao za kulinda usalama wa nchi, wananchi wenyewe na mali zao. Kwa hiyo, kulikuwa na matukio mengi, tunashukuru kwa kiasi kikubwa yamepungua kutokana na jitihada zao, *RPC* na Kamishna wa Zanzibar, narudia tena kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kuongelea usalama wa barabarani. Hili nalirudia kwa mara ya pili, Bunge lililopita nilizungumzia na sasa nalirudia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa Mahakamani umekuwa mkubwa sana kutokana na kutotoa adhabu za papo kwa papo zile ndogo ndogo ambazo hazitaki ushahidi wala jambo lolote lingine. Kule Zanzibar kama daladala inaandikwa abiria kumi na nne maana yake kumi na nne. Sasa dereva akizidisha abiria mmoja unampeleka Mahakamani anakwenda kufanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu amepanda baiskeli haina taa, unampeleka Mahakamani anakwenda kufanya nini? Japokuwa hapa Dodoma kupanda baiskeli bila taa ni jambo la kawaida, lakini kule ni tatizo na hapa Dodoma tumelizungumza sana, lakini mpaka leo, linaonekana ni jambo la kawaida tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri alitafutie ufumbuzi ili itumike kama inavyotumika huku Tanzania Bara, makosa madogo madogo ya madereva wawe wanapigwa faini wanamalizana, hawaendi Mahakamani. Sasa hebu tuwaamini na wale Polisi waliopo kule ili waweze kufanya kazi na kupunguza msongamano ambao sio wa lazima kule Mahakamani. Kwa kweli Mahakama tunazipa kazi kubwa ambazo nyingine ni za kuzitatua kwa dakika kumi, lakini mtu anakamatwa na baiskeli kama nilivyoeleza, anapangiwa siku ya kwenda Mahakamani bila sababu yoyote. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo ili liweze kutusaidia katika kupunguza msongamano Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitendea kazi. Najua kwamba hali yetu ya kifedha sio nzuri na kwamba hatuwezi kila kituo tukakipatia gari moja, mbili, tatu, najua ni tatizo. Lakini tumezungumzia sana suala la vitendea kazi basi vituo angalau vipatiwe pikipiki ili yale mambo ya dharura basi waweze kuyashughulikia, na sasa wakifika huko kama kunahitajika gari basi wao ndiyo watafanya utaratibu wa kutafuta gari ili kile walichokiendea kiweze kupata ufumbuzi. Lakini unaweza kupiga simu kwenye kituo cha Polisi, gari kama

walivyozungumza wenzangu pengine ni ya Mkuu wa Kituo cha Polisi tu wakati huo haipo, hakuna kitu chochote kingine kinachoweza kuwasaidia wakafika katika sehemu ya tukio na wakalitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo tumejaribu sana kuomba angalau *radio call* za mkononi ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Sawa nakubali sungura mdogo hagawiki kama tunavyotaka, lakini jitihada pia ikiwepo basi kwa asilimia japo ndogo tunaweza kupunguza tatizo hilo. Sasa kama hili haliwezekani pia basi wale Askari wanaokwenda kwenye lindo wanazo simu zao za mikononi basi angalau wapewe vocha ili katika matukio waweze kuzitumia simu zao, lakini hizo simu wawekewe fedha siyo simu zao wazitumie moja kwa moja katika matukio, sawa anafanya kazi lakini hebu tuwafikirie wasaidiwe angalau kupewa vocha kama wapo Askari wane, basi Askari wawili wawekewe vocha ili waweze kuisaidia Polisi katika njia hiyo. Mimi nafikiri tukifanya hivyo tutaweza pia kupunguza matatizo na kupata taarifa ambazo zinahitajika kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mlundikano wa wafungwa kwenye Magereza. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengi wamezungumzia suala hili. Nakumbuka katika ukurasa wa nane katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amezungumzia kujenga Magereza. Mimi sitoi kipaumbele sana katika kujenga Magereza. Pamoja na kwamba katika taarifa yake Mheshimiwa Waziri kuna kipindi cha ijue Magereza. Wajaribu kuongeza jitihada zaidi ya kutoa elimu ili watu kupunguze kufanya makosa. Kuna makosa mengine hutegemei kutokea, lakini kuna makosa mengine yanafanywa kwa makusudi, sasa yale hayaepukiki. Kwa sababu mtu kufikia hatua ya kuua hiyo siyo bahati mbaya, huyo amedhamiria. Lakini kuna makosa mengi madogo madogo ambayo watu wakipata elimu basi yanaweza yakapungua na watu wakipunguza kufanya makosa ndivyo watakavyopungua kwenda katika Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kama ni suluhisho litakalotusaidia kuongeza Magereza, maana yake tunawaambia fanyeni zaidi. Kwa hiyo, ningeomba sana wazidishe kutoa elimu ili wafungwa wapungue katika Magereza kwani hizo ni nguvu kazi zitakazoweza kutusaidia kwa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la maalbino. Kwa taarifa yenu siku Wizara ya Nishati na Madini ilipofanya sherehe tulikuwa na kazi kubwa sana ya kumlinda Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir kwa sababu watu wa madini hao ndiyo walioanzisha mambo ya maalbino. Kwa hiyo, tulijitahidi sana na Mheshimiwa Wilson Masilingi hapa angalau wasiweze kumchukua. Sasa hili nataka lishughulikiwe vizuri sana na linatakiwa kushughulikiwa kwa sababu ni suala ambalo linaleta matatizo nchi yetu. Ni mfumo ambao umezuka haujulikani ulipoanzia wala utakapoishia.

Kwa maana hiyo, hatujui utamalizika lini? Kuanza ndiyo umeanza, lakini kumalizika hatujui utamalizika lini? Kwa hiyo, tungeomba sana pamoja na jitihada zote, pamoja na vikosi vyote alivyothibitisha Mheshimiwa Waziri vinaundwa kwa ajili ya kazi hizo tunaomba jitihada iongezwe ili tuweze kuepusha ama kumaliza kabisa vifo vya ndugu zetu maalbino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama makosa hawana lakini wanahukumiwa kwa tamaa. Kwa hiyo, tamaa za baadhi ya watu zinawafanya maalbino wawe hawana raha ya kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii na mimi kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi yao nzuri wanayoifanya ingawa wapo Askari wachache. Aidha, kwa mapenzi yao wenyewe wanafanya mambo ambayo wanataka kulipaka tope Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi wengi tu, wakilalamika pale wanapotuhumiwa na mali zao kukamatwa na kupelekwa katika Vituo vya Polisi mali hizo hupotea, hazijulikani zinapokwenda. Sasa tunataka Mheshimiwa Waziri atueleze. Mimi ninavyojua Polisi kazi yake ni kulinda raia pamoja na mali zake. Lakini inakuwaje pale mali zinapopelekwa katika Kituo cha Polisi na tunaamini pale ulinzi upo, mali hizo zinapotea? Tunataka kupata maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulisema hilo, ningependa pia kuzungumzia matatizo kwa Askari wetu wa Polisi. Kama walivyokwishakusema Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Maaskari wetu wanapewa posho ya chakula ya Sh.1,600/= kwa siku. Sisi wenyewe ni mashahidi kwamba hali ya maisha na gharama za maisha zimepanda, Sh. 1,600/= kwa Askari ambaye ana familia ya watoto wawili tu hiyo hela haitoshi. Labda kama tunataka Askari wetu wale chakula cha kujaza matumbo ilimradi washibe, lakini kama tunataka kweli wale chakula chenye kujenga miwili yao na waweze kupata afya bora, kwa Sh. 1,600/= hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari hao wanafanya kazi katika mazingira magumu, na kama kweli tunataka vijana hao waweze kufanya kazi kwa kujituma na kwa moyo mmoja na wasiweze kujiingiza katika vitendo vya rushwa, basi Wizara iweze kuangalia posho hii kupanda angalau waweze kupata mlo mzuri, wao na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika tatizo lingine la Askari wetu, ni kuhusu sare za Polisi. Maaskari hawa wana sare moja tu na *uniform* yao ni moja tu. Sasa Askari huyu anafanya kazi usiku na mchana, *uniform* aliyonayo ni moja, inafuliwa saa ngapi? Inakauka saa ngapi? Inapasiwa saa ngapi? Mara nyingi unakuta Askari wetu sio nadhifu, *uniform* zao zimechakaa na nyingine vimewekewa hata viraka. Sasa hili ni kuwadhalilisha vijana wetu wa Jeshi la Polisi ambao wanafanya kazi kwa kujituma. Tungeomba hilo nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua bajeti ya Wizara hii ni kidogo, lakini inabidi tuseme ili Serikali isikie ili katika bajeti ijayo iweze kuangalia matatizo hayo ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye makazi ya Polisi. Katika bajeti iliyopita nilisema na hili nimpongeze Mheshimiwa Waziri, amelisema katika hotuba yake kwamba wameanza, lakini bado makazi ya Polisi ni tatizo kubwa sana. Nyumba nyingi zimejengwa enzi zile za mkoloni na hata nyumba tulizozijenga sisi wenyewe nyingi ni za bati na Maaskari hao wanapata shida sana na nyumba hizo nyingi zina *room* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukibahatika kuingia katika nyumba hizo utaona vituko. Wanatumia shuka kugawa, ili kupata vyumba ndani ya chumba kimoja. Maaskari hao wana watoto, wana wake na wanahitaji faragha pia. Wanapotoka kazini wamechoka baba na mama

wanahitaji kuzungumza na kupanga maisha yao, lakini na watoto nao wapo, wana watoto wa kike na wa kiume katika chumba kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti iliyopita nilisema hayo siyo maadili mazuri kwa sisi Watanzania. Tunaomba sana hili liangaliwe, waongezewe bajeti kwa ajili ya kujenga makazi ya Maaskari wetu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la nyumba kuna makundi mawili. Wale Maaskari ambao wamebahatika kupata nyumba za Polisi hizo huwa hawalipi kodi. Lakini wale Maaskari ambao wanakwenda kupanga uraiani hutoa fedha zao wenyewe kulipa kodi ya pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba hili nalo liweze kuangaliwa ili tuweze kuondoa makundi katika Jeshi la Polisi na wote kama wanalipiwa, basi hao wanaokwenda kupanga uraiani tunaomba na wao waweze kulipiwa kodi hiyo ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni mishahara ya Polisi pamoja na upandishwaji vyeo. Wenzangu wamelisema hili na hili la mishahara naomba liweze kuzingatiwa ili tuweze kuondoa tatizo hili la rushwa ingawa inawezekana hata ukipandisha wale wenye tamaa bado wataendelea kupokea rushwa, lakini ninaamini kama tukiweza kuweka mazingira yao mazuri na mishahara ikipanda inaweza kuwatia moyo na kuachana kabisa na matendo ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa Askari wa Barabarani. Kwanza, nimpongeze Kamanda Kombe hasa kwa Jiji la Dar es Salaam kwa kuweza kuweka utaratibu ule wa asubuhi, kuweka askari wake barabarani kuweza kuongoza magari. Lakini ninapenda kumwambia Kamanda Kombe kwamba baada ya ule muda wa saa tatu kupita maaskari hawa huwa wanaondoka na hii inasababisha msongamano mkubwa sana barabarani na hasa pale taa za barabarani zinapokuwa zimezimika. Kwa sisi tunaotoka Mikoani inakuwa ni taabu sana; kwa kuwa kule tunakotokea maeneo ambayo magari sio mengi kama Dar es Salaam.

Kwa hiyo, tunamwomba Kamanda Kombe pamoja na ule muda wa saa tatu kupita, maaskari waendelee kukaa barabarani na hasa taa zinapozimika nao waweze kuwepo barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la daladala, hakuna madereva ambao wanakiuka taratibu za barabarani kama watu hawa. Nimesikia kuna mpango wa kuviondoa, napongeza mpango huo kwa sababu hawa ndiyo wanaosababisha sana ajali hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Huwa wanakuja mbele yako wanachomeka gari mbele yako na wanasababisha ajali nyingi sana. Kwa hiyo, napongeza utaratibu uliofikiwa na ninaomba wale Askari ambao wana pikipiki waweze kusaidia katika zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nije kwenye suala la uchaguzi Kiteto. Mimi nilikuwa ni mmoja kati ya watu waliopangwa katika uchaguzi ule na nilibahatika kupangwa katika Kata ya Kijungu. Katika kipindi hicho cha uchaguzi katika Kata ya Kijungu kulitokea vurugu.

Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, *RPC* wa Mkoa wa Manyara Pamoja na *IGP*, tuliripoti kwao na walitupa ushirikiano. Lakini pamoja na ushirikiano huo, kuna mambo ambayo ningependa kuyajua. Katika vurugu hizo nilibahatika kuwahi katika Kituo cha Polisi na nilijitambulisha na kutaka kujua ni nini kinachoendelea, maana tulipokuwa njiani kurudi Mjini Kiteto tulisimamishwa na wananchi na wakatuambia Mheshimiwa Mbunge, viongozi wenu wamekamatwa na wamepelekwa Kituo cha Polisi Kijungu.

Nilikwenda na kujitambulisha na kumwuliza Askari niliyemkuta pale, viongozi hawa wana tatizo gani? Alijibu Askari yule na kuniambia kwamba Mheshimiwa Mbunge, naomba umsubiri Mkuu wa Kituo aje yeye atakueleza. Lakini kwa masikitiko makubwa Mkuu yule wa Kituo alipoingia katika Kituo kile alianza kuwapiga viongozi wale na tayari walishawekwa chini ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokijua mimi, mtu anapokuwa chini ya ulinzi humpigi kwa sababu ameshakubali na kukaa chini. Lakini Mkuu yule wa Kituo kwa macho yangu aliwapiga viongozi wale na hata wale niliokuwa nimeongozana nao walipohoji nao waliambiwa wakae chini na kupata kipigo. Mimi nilinusurika, sijui kwa kuwa nilikuwa mwanamke peke yangu au ni Ubunge sijui sababu. Lakini wale niliokuwa nao walipigwa na kusababishiwa maumivu na majeraha makubwa na kijana wetu mmoja, dereva wetu hata kushonwa nyuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujua iliundwa Tume na Tume ile tulisoma kwenye vyombo vya habari kwamba imeshakamilisha uchunguzi wake. Sasa ningependa Mheshimiwa Waziri atuambie Tume ile imegundua nini na katika maelezo tuliyoandika, Kiteto kuna vijana wawili waliojitambulisha wao kuwa ni Usalama wa Taifa na mmoja alikuwa amekamata silaha ya askari, baadaye tulipokuja kukutana naye kituoni Kiteto Kibaya alijitambulisha kwamba ni mwanachama wa chama ambacho tulishiriki nao katika uchaguzi ule. Mwanzo walituambia kwamba wao ni Usalama wa Taifa. Tunataka kupata maelezo kama kweli, wale walikuwa ni Usalama wa Taifa au walikuwa ni wakereketwa wa chama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasikitisha na hawa ndiyo wale niliosema wanatusababisha tukose imani na Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho atupe taarifa ya Tume ile na nini kinaendelea kwa sababu ninajua Tume ile ilitumia fedha za walipa kodi wa nchi hii na tunataka kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba upokee shukrani zangu kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia machache katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri na kuiwasilisha hapa Bungeni na wote tumeifurahia, tumeielewa na imetupa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi za pekee kabisa kwa Waziri na Naibu Waziri kwa namna ambavyo wameonyesha kuimudu sana hii Wizara. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Balozi Kagesheki kwamba mimi na wapiga kura wenzangu wa Bukoba Mjini tuna imani naye, tunampenda na tunamhakikishia kwamba tuko pamoja naye, tunamwombea kila la kheri aweze kumudu shughuli za Kitaifa, lakini pia Jimbo lake la Uchaguzi la Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limepongezwa sana na mimi niko katika utaratibu huo huo wa kuwapongeza Jeshi la Polisi, na hasa kwa kweli Polisi wa Mkoa wa

Kagera. Mkoa wa Kagera kama inavyojulikana uko mpakani. Kuna matukio mengi sana ya ujambazi katika mapori kati ya Karagwe na Ngara, Ngara Biharamulo, Biharamulo na Bukoba na huwa inalazimika magari yote kusindikizwa na Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ujambazi wa kutekwa magari katika Mkoa wa Kagera ni wa muda mrefu sana. Umeanza siku nyingi. Lakini inakuwa wakati mwingine umetulia zinapofanyika *operation*, basi unatulia kidogo. Lakini bado unabaki pale pale. Sasa mimi najiuliza, nafikiri kwamba pengine haujafanyika uchunguzi wa kujua hao majambazi wanatoka wapi? Kama ni nchi jirani ikajulikana na tatizo hilo likashughulikiwa katika utaratibu mwingine labda wa ujirani mwema au kwa ushirikiano wa nchi jirani. Kama majambazi hao tunaishi nao vijijini na mijini, pia ieleweke wananchi wapige kura wawaseme wale watu bila shaka watakuwa wanawafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ujambazi huu umeanza siku nyingi, mimi binafsi nimekwishaatharika katika kutekwa huko. Nilitekwa mwaka 1989. Kwa hiyo, mwaka 1989 ni zamani lakini ilikuwa ni hata kabla ya hapo mpaka nimeshindwa hata wa kumdai maana nilianza kupata ugonjwa wa moyo kuanzia hapo. Kwa hiyo, nina *pressure* mpaka sasa na sijui kama nitapona. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kwa kweli waliangalie hili tatizo kwa sababu limekuwa ni tatizo la kudumu. Katika ujambazi huo huo tulifikiri baada ya wakimbizi kuanza kurudi kwao tutapata amani. Katika Wilaya ya Ngara nadhani wiki mbili zilizopita kulitokea uvamizi katika Kata zilizo mpakani mwa Ngara na Burundi katika maeneo ya Mgoma, Kirusha, Kasange, Mabawe, Chululigwa na maeneo mengine katika Kata zilizo jirani na Burundi walivamiwa wananchi kwa silaha kali kiasi kwamba wakaogopa mpaka wakakimbia nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni hatua gani iliyochukuliwa? Nilimwona *DC* akisema kwamba wananchi wakae watulie, lakini watatuliaje? Ni hatua zipi hasa zilizochukuliwa ili kuhakikisha kwamba kweli tatizo hilo litakwisha kwa sababu mara nyingi sana wavamizi kutoka Burundi wanaivamia sana Ngara katika Kata hizo za mipakani. Sasa imekuwa ni kama tunachezewa tu watu wanauawa, watu wanaibiwa mali zao na sasa katika utaratibu huu wa Burundi na wenyewe kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hivi huu ndiyo ushirikiano tutakaokuwa nao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko ili wananchi wa Ngara waishi kwa amani. Wananchi wa Ngara wanahitaji kuwa na amani. Kwa hiyo, hilo naliomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunalipongeza sana Jeshi la Polisi, lakini ni kwa kiasi gani jeshi hili tunalitunza au askari tunawatunza ili wafanye kazi katika mazingira mazuri, mazingira ya kufurahisha mazingira ambayo hata yanawapa afya nzuri? Hawa askari wanaosindikiza magari katika mapori, ukiwakuta pale porini hata wewe utawaonea huruma sana. Hata inakufanya mtu usiamini kama kweli wanapewa huduma yoyote nzuri. Wewe uniambie amekwenda kulinda majambazi, majambazi yanakuja na silaha kali, wako porini kwenye mahema hawana hata usafiri, hawana hata nyenzo yoyote ambayo inaweza ikawasaidia. Siwezi kujua wanalipwa nini, lakini dalili ninazoziona naona kwa kweli huduma wanayopata sio nzuri. Kwa hiyo, katika kazi hizi ambazo kweli watu wanajitolea kukabiliana na adui ana kwa ana, basi waangaliwe walipwe vizuri ili waweze kufanya hiyo kazi, basi angalau wakijua kwamba na Taifa nalo linatambua kazi hiyo wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, wenzangu wamezungumzia juu ya nyumba za askari na mimi pia napenda kuzungumzia nyumba za askari katika Mkoa wa Kagera. Wilaya

zote kwa kweli nyumba za askari haziridhishi. Nyumba za askari pale Bukoba Mjini Makao Makuu ya Mkoa Buyekela, nyumba zinatisha, ni utaratibu wa kuweka pazia/shuka kama alivyosema mzungumzaji aliyemaliza kuchangia. Nyumba za *FFU* Nshambia kwa kweli zinatisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani Serikali ilione hili nyumba bora ni kigezo kimojawapo cha kwamba uchumi unakua au pengine mtu siyo maskini maana umaskini unaweza ukapimwa hata kigezo cha nyumba kikawemo. Sasa kama wanalala katika nyumba zisizofaa ni dhahiri kwamba hata afya zao zitaathirika. Lakini pia hawataweza kufanya kazi vizuri kama tunavyowatarajia. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana pale Magereza wana ghorofa moja ndipo wanapoishi Askari Magereza na lenyewe linatisha hata kwa kuliangalia. Hakuna matengenezo wanayofanya, mifumo ya maji taka ni mibovu kwa sababu mara nyingi tunaona hata maji yanatiririka. Kwa hiyo, hili jengo pia na lenyewe lingefanyiwa ukarabati ili waweze kuishi vizuri, waweze kuishi angalau isionekana kwamba basi Askari Magereza na mfungwa tofauti yake ni ndogo. Kuwe na tofauti kubwa ingawa pia na wafungwa wanahitaji kuhudumiwa kama binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mmoja siku zimepita aliposikia watu wakilalamika kwamba wafungwa hawapati huduma nzuri, hawapati chakula kizuri, hawapati nini, yeye kwa kweli akajibu kwamba jamani Gerezani siyo Sheraton. Sisi wote tunajua Gereza haliwezi likafanana na Sheraton, hata wakati mwingine, hata nyumbani kwako hapawezi kufanana na Sheraton hiyo ya zamani aliyokuwa anaisema huyo mzungumzaji. Lakini tunachokisema, ni huduma nzuri ya kawaida, wale ni binadamu. Hicho chakula wanachopata kiwe chakula ambacho kinaweza kumfanya mtu apate afya nzuri. Hayo mavazi wanayovaa hata na yeye jamani yanaweza yakafanyiwa *modification* yakawa mazuri zaidi wakaonekana kwamba ni binadamu. Hata malazi, kwani akilala kwenye kitanda kuna nini? Hakuna tatizo! Bado ni mfungwa, maana kumfunga mtu siyo kwamba unakwenda kumtesa, lakini labda ni kumnyima ule uhuru wa kutembea na kufanya anavyotaka wakati wowote. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ayaangalie hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nilikuwa napenda kuchangia sasa hivi tunaona kwamba Taifa letu linakabiliwa na upungufu wa chakula, lakini yapo Magereza ambayo ni ya kilimo yanalima, wafungwa wanalima. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba katika Magereza haya, basi wapewe uwezo, kwa mfano Gereza la Kitengule lipewe uwezo ili liweze kulima hata Magereza mengine kwa sababu ardhi Mkoa wa Kagera sio tatizo. Hata Ngara wanaweza kulima, Biharamulo, Karagwe wakalima hata chakula cha kujitosheleza kwa mahitaji ya wafungwa lakini pia hata kwa kuwauzia watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba wakati huo huo ili kuwezesha Majeshi yetu yafanye kazi vizuri, basi yaweze kupewa nyenzo za kuwasaidia, wawe na magari kama wale maaskari wanaosindikiza wasafiri wanao-*escort* magari wawe na usafiri wao ambapo wanaweza wakapata hata tatizo usiku. Hivi kwa mfano mle porini kukitokea lolote wanafanyaje, wala hawawezi hata kujihami. Kwa hiyo, tuweze kuwa na magari ya kutosha, pikipiki na vyombo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo. Kwa kweli na kwa dhati nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu kwa hotuba yao nzuri sana ya bajeti. Nampongeza sana Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo, nampongeza sana *IGP*, Kamishna wa Magereza, Mkurugenzi wa Uhamiaji na *DCI* na Zimamoto nilimsahau tena mtu wa Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa niende kwenye eneo la vitambulisho vya Serikali. Kwa kweli Watanzania wamesubiri kwa muda mrefu na sasa wote wamepata faraja pamoja na mchakato huu umekuwa na mambo mengi kwa muda mrefu, lakini nilikuwa na mtazamo mwingine kwa sababu Kamati yetu tulibahatika kwenda Zanzibar tukaona wenzetu wa Uhamiaji wa Zanzibar wanavyofanya. Wenzetu wa Uhamiaji wa Zanzibar tenda ile ya vitambulisho hawakutoa kwa Makampuni binafsi waliifanya wao wenyewe Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli kazi hii Idara yetu ya Uhamiaji ina uwezo wa kufanya, kama inaweza kutengeneza *passport* itashindwa nini kutengeneza vitambulisho vya Serikali? Kwa kweli kazi hii ingefanywa na Idara ya Uhamiaji tungeweza kuokoa pesa nyingi zikaingia kwenye matatizo ya Jeshi letu kwa ujumla la Polisi, Magereza na Uhamiaji na tungepata nyumba maeneo mengine. Kwa sababu mradi huu ni mradi mkubwa sana wa pesa nyingi na zimeanza kutoka shilingi bilioni nne tu, lakini kuna mapesa chungu nzima, utagharimu sio chini ya shilingi bilioni 40. Sasa lazima mara nyingine sisi viongozi tuwe wabunifu na ndiyo maana ya uongozi. Leo huu ni mradi wa kudumu, sio mradi wa mara moja. Tunatoa tenda, watu wanazaliwa kila siku, watu wanakua kila siku, sasa tutaendelea kutoa tenda hii mpaka lini? Kama inawezekana, kazi hii ipewe Uhamiaji na tulishazungumza, Kamati zilizungumza, lakini sijui ni wapi watu wasiposikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la matatizo la Jeshi la Polisi la wafanyakazi wa chini, Magereza na Uhamiaji ni suala ambalo Wabunge wote wameliongelea. Mimi nalijua vizuri sana lakini sitaki kuongea nitarudia yale yale. Ni vyema basi tukafanya makubaliano mwakani wakati wa bajeti tunasema sungura mdogo, basi sungura huyo japo paja tuamue liende Wizara ya Mambo ya Ndani likatatue tatizo hilo. Lakini bila ya hivyo, tutasema kila siku matatizo ya Jeshi la Polisi hatuwezi kuondoa na matokeo yake katika hali hii kwa kweli kuondoa rushwa itakuwa shida. Lazima tuambiane ukweli. Ndiyo maana unaambiwa kwenda kituo cha Polisi unakwenda bure lakini kutoka shauri lake ni kubwa sana.

Kwa hiyo, ni vyema sasa tukaangalia, tunaambiwa tunaweza kukopa, hatuwezi kila siku tukakaa tunategemea mapato yetu ya ndani na ya nje wakati Mabenki yapo, vyombo vya pesa vipo tukope tumalize haya matatizo yetu. Leo tunategemea Jeshi la Polisi tunalilaumu litafanya kazi bila ya nyenzo, uwezo na bila ya pesa. Unaambiwa askari wa chini akienda likizo analipwa shilingi 150/= kilomita moja mizigo yake ya usafiri, sasa anakwenda wapi ataweza kufika kwao kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia jambo moja Mheshimiwa Masha mwenzangu, ndugu yangu, Naibu Waziri kaka yangu lakini leo sitaunga mkono hoja hii mpaka kesho. Dar es Salaam kilitokea kifo cha kijana mmoja anaitwa Hijja na mwenzake Minde. Mheshimiwa Waziri anajua. Kilikuwa nikifo cha kutatanisha sana! Hijja aliuawa pale Kimara Temboni, Minde aliuawa Sinza. Mheshimiwa Waziri Mwapachu akaunda Tume. Toka Tume ile iundwe tarehe 28 Februari, 2007 ilipewa wiki tatu tu na ilikuwa na wataalamu wa kila eneo Haki za Binadamu, Idara ya Sheria, Wanasheria waliobobea, wachunguze. Wiki tatu na maamuzi yote tunajua yako tayari, sisi watoto wa mjini bwana. Lakini leo ni mwaka mzima sijui mnapata kigugumizi gani! Sio lako hili Mheshimiwa Masha, wala kaka yangu hapo Mheshimiwa Kagasheki, lakini mmerithi na yule mliyomrithi kazi yote alimaliza. Lakini cha kusikitisha, wale vijana walichukuliwa magari yao matatu, *RAV 4*, mbili na Vitara moja na kuna Kamanda mmoja alikuwa anasifiwa sana alichukua ile gari akawa anaitumia, yanafanana kabisa na yale ya watu wa Madini wale. Sasa naomba kesho wala sitaki maelezo marefu, Taarifa ile ya Tume mtaitangaza lini? Majibu mnayo na yale magari matatu ambayo

Mahakama ilishawafutia wale vijana hawana hatia na ilishaamuliwa magari yao walirejeshewa, sasa kesho naomba mniambie ile gari alichukuaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti ya Waziri Mkuu niliipongeza sana mradi wa nyumba za Polisi wa *Kilwa Road* na niliipongeza Wizara na nikapongeza na *NSSF* kwa kazi nzuri na nikaomba ikiwezekana ili papendeze pale basi tumalizie zote lakini inafurahisha nasikia mpango unaendelea na nyumba zinaendelea kujengwa. Lakini nimetembelea Gereza la Keko la Mahabusu nyumba zile toka zijengwe hazijafanyiwa *repair* ya aina yoyote si ya chooni, sio veranda sio ya nje. Toka wakati wa Mkoloni na hali yake ni mbaya sana. Lakini haitoshi pale Keko kuna hospitali lakini cha ajabu kazi ya hospitali ile ni kupima na kuandika dawa askari wakatafute dawa. Wanapata wapi dawa katika hali kama ile? Lakini haitoshi, kuna migogoro ya mipaka, wamefikisha siku nyingi Wizarani, utekelezaji hakuna.

Sasa namwomba pia Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu na kaka yangu, Mahabusu wa Keko niliwatembelea, wana shida na Waziri au Naibu Waziri mtakapojibu, kesho mtaniambia wakati wowote mkiwa na nafasi tuwatembelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya msongamano wa magari makubwa barabarani, ukifika Chalinze; nilipita pale Jumamosi saa kama tano kasorobo na mimi nina tabia, nimeshazoea kusafiri usiku. Pale Chalinze kulia au kushoto malori yame-*park* mpaka katikati kwenye kingo za barabara. Ndugu zetu wa *traffic* wanakuwa katikati ya malori, wao wako katikati na wanasimamisha malori, bado dakika 20 kuchukua mpaka kuvuka.

Kwa hiyo, huku malori huku malori mnapita katikati, malori ya mafuta na malori ya kila namna. Sasa nafikiri tunangoja siku moja yatokee matatizo pale halafu Waziri Mkuu aunde Tume. Maana yake lori moja pale la mafuta na pale wanatumia vibatari wanaopitisha biashara za korosho na mambo mengine. Kwa hiyo, lori moja la mafuta likiwaka, majumba yote yatateketea na matokeo yake sasa tutaanza kuunda Tume na jambo tulikuwa tunaliona, tunalisikia na tunalielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa Dar es Salaam, watu wamezungumza hali ni mbaya. Kwa sababu sasa hivi mkipanga, mmepanga foleni hivi, daladala zitapita kulia na kushoto, wanasema wanatanua na humwambii kitu. Kulia na kushoto, nyinyi mmekaa kwenye *line* na inaweza kuwachukua hata masaa mawili nyinyi mnaofuata sheria. Lakini baadhi ya ma-*traffic* wanaona. Ifikie mahali hebu tutangaziwe, wenye daladala ngapi wameadhibiwa wakanyang'wanya leseni au wakapelekwa Mahakamani, ndio tatizo hili litakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam kumejaa *breakdown* mbovu na iko minong'ono nyingine zinawahusu wenyewe. Lakini cha kusikitisha, hiyo *breakdown* mbovu inakwenda kuvuta gari ya shilingi milioni 80, milioni 60, sasa tuombe basi *breakdown* ni muhimu na kuvuta magari ni muhimu lakini *breakdown* mbovu tuhakikishe zinaondoshwa Dar es Salaam, wenye uwezo walete *breakdown* nzuri za kuvuta magari yanayolingana na yale yaliyokuweko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona sina la zaidi, mengi tumezungumza, lakini nirudie kumwomba ndugu yangu Mheshimiwa Masha, anajua tumetoka mbali na kaka yangu Mheshimiwa Kagasheki kesho wananchi wa Dar es Salaam wangependa kusikia ile taarifa ambayo ya mauaji ya Hijja na Minde na magari hasa ile *RAV 4* aliyochukua yule bwana mkubwa aliichukuaje?

Mwisho kabisa, nampongeza *IGP*, ndugu yetu, kwa kweli kazi anayoifanya ni nzuri inaleta raha, lakini bado ana watu humo ndani inatakiwa asiwaonee aibu, asafishe ili aende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Kampuni za Ulinzi Binafsi kwa kweli zinanyanyasa wafanyakazi, lakini magari yao wenyewe ya kuchukulia pesa ni mabov, wao jinsi wanavyo-*charge* wana-*charge* kiwango cha juu, lakini wafanyakazi wanawapa malipo ya chini sana kiasi inamshawishi yule mlinzi kwenda nyumba anayolinda kuchungulia chungulia ndani kuna nini ili aweze kuchukua.

Mwisho, tukubaliane Wabunge bajeti ijayo tuwape paja ndugu zetu hawa shida zao ni nyingi. Nawashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Lile suala la Chalinze kuwa na magari makubwa yameziba njia, imenipata mimi dakika 30 hupiti, ni hali mbaya sana saa za usiku.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Tarime watani zangu kwa kuondokewa na kipenzi chao Marehemu Chacha Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Lawrance Masha na Naibu wake Mheshimiwa Kagasheki kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ingawa ni wapya katika Wizara hii. Mheshimiwa Masha namfahamu uwezo wake na Mheshimiwa Kagasheki, nina imani Wizara hii itakwenda vizuri na kwa kasi na kwa viwango.

Niwapongeze pia Watendaji wa Wizara, Katibu Mkuu na wafanyakazi kwa ujumla. Nimpongeze *IGP* Saidi Mwema. Napanda kumpongeza pia aliyekuwa *RPC* wa Kagera Ndugu Msika, alifanya kazi nzuri sana. Naambiwa amehamishiwa Makao Makuu, namkaribisha na kumpongeza *SP* Henry Salewi ambaye amechukua nafasi yake. Lakini pia nitakuwa mchache wa fadhila nisipompongeza Kamanda Tossi kwa kazi nzuri sana anayoifanya Mkoani Kagera. Huyo mzee namwombea Mwenyezi Mungu ampe nguvu na amsaidie kwa sababu anafanya kazi nzuri na ya ajabu sana. Lakini pia nampongeza *OCD* wangu wa Wilaya ya Karagwe Ndugu Chimwaga ananisaidia sana ingawa katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamesemwa hapa kuhusiana na Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi linafanya kazi ambayo kwa kweli naweza nikasema kwamba ni ya kujitoa mhanga, wanafanya kazi nzuri katika mazingira ya kutatanisha. Nasema hivyo na nitakuwa nagusia hivi kwa Wilaya yangu ya Karagwe, ukizungumzia masuala ya ujambazi katika nchi ya Tanzania naweza nikasema kitovu cha ujambazi kiko Wilayani Karagwe. Wilaya ya Karagwe inapakana na nchi ya Rwanda, Burundi pamoja na Uganda na nyie mnafahamu kabisa matatizo ambayo yanatokana na wenzetu ya vita. Tangu vita ianze kwa jirani zetu mwananchi wa Wilaya ya Karagwe hajawahi kupata usingizi, wanalala kwa mashaka masaa yote 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa unatoka Bukoba Mjini unaelekea Karagwe Mjini utapita pori moja linaitwa Uzuri wa Kondoo, pale ndio kitovu cha majambazi. Ukitaka kwenda Ngara unapita pori linaitwa Kimisi, Hifadhi ya Wanyamapori hapo ndio majambazi wamejikita. Nimekuwa nikizungumza hapa kwamba kumaliza ujambazi katika Wilaya ya Karagwe sio jambo la lelemama, ni jambo ambalo linahitaji kuwekeza kwa nguvu sana, Serikali inabidi iwekeze hapa, sio suala la kuja hapa kusema kwamba kasungura kadogo, tunamaliza bajeti tunaondoka, wananchi wanaendelea kufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Wilaya ya Karagwe inayo majimbo mawili. Jimbo la Karagwe na Jimbo la Kyerwa. Kutoka Karagwe Mjini kwenda Jjimbo la Kyerwa mpakani Murongo ni kama kilomita 150 au zaidi. Kutoka Karagwe mjini kwenda Ngara ni zaidi ya kilomita 140. Lakini la ajabu na la kushangaza Waheshimiwa Wabunge hii sehemu ambayo ndiyo nimeizungumzia kwamba ndio kitovu cha ujambazi inayo gari moja la Polisi na kigari chenyewe kimezeeka. Kwa hiyo, unapotokea ujambazi, Jimbo jirani la Kyerwa na wakati huo huo ukatokea ujambazi sehemu nyingine yule *OCD* wangu hata angejitahidi namna gani, hawezi kufika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii na yenyewe inahitaji fedha za kigeni? Kununua vi-*landcruiser* vine au vitano ukaweka pale Karagwe, sidhani kama tunahitaji kukaa na kuzungumza kwa sauti ya juu sana. Mimi nimshauri Mheshimiwa Lawrence Masha na Naibu wake. Jjamani, kelele za Karagwe za wananchi wangu kuuawa na majambazi, ninaomba zifikie mahali sasa zitoshe. Tupeni magari, Maaskari wangu wana moyo, waweze kufanya kazi. Nimezungumza tangu niingie hapa Bungeni nikiomba magari Wilaya ya Karagwe, la kushangaza na kusikitisha, sijawahi kupatiwa gari hata moja. *OCD* wangu sasa hivi akisikia tukio limetokea mahali inabidi aende kukodi teksi. Inabidi akaombe msaada kwa jirani yake ndio aende porini kupambana na majambazi ambao wanatumia silaha za kivita. Mheshimiwa Masha hii naweza nikasema ni aibu kubwa sana na ni fedheha kuacha majambazi wakatamba katika Wilaya ya Karagwe wakati Serikali ipo.

Nawaombeni jamani tupeni magari japo manne kwa kuanzia, moja likae Murongo, moja likae Kimisi, lingine likae Uzuri wa Kondoo na lingine liwe *standby* pale Karagwe Mjini na kuhakikishia maaskari wangu watafanya kazi nzuri. Hata pikipiki za Askari Polisi kufanya kazi, inapotokea ujambazi sehemu za karibu sehemu za kuelekea Bushangaro kupita pori la Bigoro askari wanashindwa kwenda, wananchi wanabaki wanapiga simu mwisho wanasema kwamba askari wa Karagwe wanashirikiana na majambazi, sio kweli, hawana vitendea kazi. Mheshimiwa Masha hawataweza kusaidia hawa watu kama hutawawezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo mengi yamezungumzwa kuhusiana na pori la Kimisi. Ukipita pori la Kimisi ukitokea Ngara kwenda Karagwe utakutana na kijumba kimoja kimechakaa sana, kimejengwa kwa udongo. Hicho ndio kijumba ambacho wanakaa askari wa Karagwe wanaolinda wanasubiri kuwahami wananchi na majambazi kutoka nchi jirani. Kile kijumba hata mtu ukiegemea kidogo kinaanguka. Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ya Bunge ilipita pale ikakiangalia ikatoa mapendekezo, jamani tunaomba basi kijengwe basi hata kwa matofali kiwe imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kagasheki alifika pale Wilayani Karagwe naamini aliziona nyumba za askari Polisi wa Wilaya ya Karagwe, ni kichekesho kitupu! Mimi nimetembelea pale mwanzoni mwa mwaka huu nilizikagua nyumba zao, chumba kimoja cha askari zinakaa familia mbili. Mtu mwenye mke na watoto anakaa kwenye chumba kimoja wametenganisha na shuka na mwingine ana mke na watoto tena wakubwa, sasa hata ile amri ya Mungu itatimizwa vipi jamani katika mazingira kama hayo? Nyumba za askari hakuna, matokeo yake zaidi ya asilimia 70 ya askari wanaishi mtaani kwa kupanga. Ile wanayolipa chumba Sh. 10,000/= mpaka Sh. 15,000/= hata Serikali haiwarudishii. Hakuna *compensation!* Sasa matokeo yake tunabaki kuwalaumu kwamba askari hawana moyo. Kumbe Serikali mnawavunja moyo maaskari wetu. Wapeni nyenzo wafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Karagwe kama Karagwe haina hata askari wa kutosha achana na vifaa. Mahitaji ya Wilaya ya Karagwe ya askari ni zaidi ya mara nne ya wale

ambao wapo sasa hivi. Tupeni askari walinde watu wetu sisi tunateseka sana wananchi wangu wanakufa mno zaidi ya miaka 15 Wilaya ya Karagwe mtu hawezi kutembea kwa amani. Sasa na sisi tunataka uhuru wetu ambao tulipigania kwa pamoja na sisi watu wa Karagwe tufaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa kuhusiana na maslahi ya askari Polisi, akasema, inawezekana askari Polisi hawajui haki zao. Mimi nasema sio kweli.

Nasema hivyo kwa sababu Jeshi la Polisi limeweka vizuri maslahi ya askari wao katika kanuni zao ambayo inaitwa *Police Force Service Regulation* ya mwaka 1995 na imefanyiwa mabadiliko mwaka 1977. Kama hii ingefuatwa vizuri, nakuhakikishia Polisi wetu wasingekuwa na malalamiko hata kidogo. Kuna maslahi mbalimbali, kuna posho ya nyumba kwenye hizi kanuni, kila Polisi ambaye anaishi mtaani inabidi apate posho ya nyumba, lakini hawapewi; posho ya usafiri wanaokaa nje ya nyumba za *Police Barracks,* hawapewi; posho ya matibabu, hawapewi; likizo wanakopwa, hawapewi; fedha za likizo za kwenda nyumbani kwao; lakini kanuni inasema lazima wapewe. Uhamisho, *night duty allowance* askari ambaye analinda usiku lazima apewe *allowance,* sio anakaa pale Benki kama ombaomba. Pia nguo za kiraia askari wetu ambao ni wapelelezi hawapewi posho zao za kununua nguo zao za kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vitu vyote viko kwenye *regulations*. Maaskari Polisi ambao wanalinda pori la Kimisi na mitaa mingine huko maporini wanastahili kupata *dry ration,* chakula kikavu, badala yake Askari anashinda porini hana hata maji hata *biscuit,* Serikali haimpatii, mwisho abiria wanaopita pale anaanza kuwaomba anakuwa kama ombaomba. Kwa kweli wanadhalilishwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitambulisho. Askari wangu wa Karagwe, nilifika pale wakatoa kilio kwamba hawana vitambulisho. Anapomkamata mtu anamwambia mimi ni askari, anaambiwa lete kitambulisho chako, anashindwa kukitoa kwa sababu hana, naomba wapewe vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine *bullet proof.* Sasa hivi majambazi wame-*advance,* majambazi wamejipanga vizuri sana. Tununue zile fulana, tuwape maaskari waweze kujilinda na majambazi. Simu za mkononi, teknolojia imekua, wapeni askari simu za mkononi hata za bei nafuu wakienda porini au sehemu nyingine waweze kuwasiliana na wenzao na kuripoti matukio.

Msongamano Magerezani umeelezwa kwa kirefu, lakini pia Magereza yetu tumeyasahau, wana vigari vya kizamani, hawana maji. Mimi nimefika pale Gereza la Kayanga hawana hata matenki ya kuhifadhia maji. Wamenituma wanaomba wapewe fedha ya kuvuna maji ya mvua, hiyo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitambulisho, imezungumzwa sana hapa na wenzangu lakini nilitaka kusema kwamba fedha ambayo imetengwa ambayo tumeambiwa leo hii ndogo. Ingawa tunahitaji kama shilingi bilioni 58. Sasa Serikali iangalie uwezekano kama tuko *serious* na jambo hili, basi Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nilitaka niseme kwamba Wilaya ya Karagwe naomba iangaliwe kwa makini. Ule ulinzi tunaoupata, sasa hivi maaskari wanajitahidi lakini hautoshi tutaendelea kukaa katika hali kama hiyo mpaka lini? Mimi namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani safari hii ajipigepige ajitahidi mimi niondoke na magari manne

nipeleke Wilayani kwangu. Ninasema hivyo kwa sababu Waheshimiwa Wabunge nyinyi hamjafika Karagwe, mkifika mtajionea, hakuna Mbunge anayeingia Karagwe bila ya kuomba *escort* na kwa bahati mbaya tunapopata *escort* ile anachukua kagari kako labda ni cha *Corolla* maaskari wawili watatu wanaingia humo anakwambia mpakate mtoto wako au mke wako. Maaskari wanaingia humo na bunduki zao.

Sasa inakuwa ni nini hiyo? sisi tunataka *patrol*. Gari moja iwe mbele na gari nyingine iwe nyuma, hapo ndiyo unaweza ukasema kwamba unalindwa. Lakini askari aingie kwenye kagari kako kadogo anasema twende, majambazi wanam-*spot* na wakianza kumshambulia mwenyewe anafurukuta humo ndani hawezi kutoka. Waheshimiwa Wabunge, mimi nawakaribisheni mje Karagwe mtajionea hali halisi na naomba msiombe *escort* ili mwone hali yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba niseme hivi; Serikali kama kweli inataka kuwa *serious*, ninaomba iwekeze katika Wizara hii. *Nothing comes out of nothing*. Haya mambo ya kudanganyana, tunaleta Bajeti ndogo ndogo hivi, hii ni Wizara nyeti. Wabunge hatuwezi kukaa humu ndani kama hatuna usalama. Mabenki hayatafunguliwa kama hatuna usalama. Maaskari wetu wanajitahidi, lakini kwa Bajeti hii tunawaangusha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nilitaka niyaseme hayo na nina imani Mheshimiwa Masha atanipa magari. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwa siku hii ya leo. Kwanza kabisa naomba nianze kwa kusema naiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze MheshimiwamWaziri, Mheshimiwa Naibu Waziri kaka yangu Balozi Kagasheki, Katibu Mkuu Ndg. Mohamed Muya, *IGP* Said Mwema, *Principal Commissioner* wa Magereza Ndugu Nanyalo na Mkurugenzi Mkuu wa Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali, Wizara ya Mambo ya Ndani kwanza kabisa kabla sijasahau kwa kututengea fedha katika Bajeti hii kutujengea Kituo cha Polisi kwenye Wilaya yetu ya Namtumbo, tunaishukuru sana Serikali. Nalipongeza pia Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kutekeleza mipango mikakati yao na tunaamini kabisa tukiwasaidia na kuwapa nguvu basi amani ya nchi yetu itaendelea kuwepo bila kuteteleka. Lakini naomba pia niipongeze Serikali kwa kazi nzuri na hatua kubwa waliyoifanya ya kudhamini mradi wa ujenzi wa nyumba za askari unaojengwa kwa mkopo wa *NSSF*. Hili ni jambo jema kwa askari wetu na tunaamini litaendela nchi nzima kidogo kidogo na mpaka Idara nyingine za Wizara hii ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie ajali za barabarani. Kumekuwa na ajali nyingi zinazosababisha vifo vingi na upotevu wa mali za watu za thamani kubwa sana. Kwa kuwa suala hili la usalama barabarani kwa mujibu wa Sheria linasimamiwa na Jeshi la Polisi pekee, hivyo hufanya suala la *Vehicle Inspection* kuwa ni la Polisi tu. Wakati Sheria hii inatungwa ya usalama barabarani, magari yalikuwa ni kidogo. Lakini wakati ule kama utakumbuka, huduma ya mabasi ilikuwa ni huduma hodhi na ilikuwa inahudumiwa na makampuni makubwa yaliyokuwa chini ya Serikali.

Kwa Mfano, *KAMATA* au *Railway Bus*, utakumbuka watu wa kusini kule *TT Co.* Haya yote yalikuwa ni Mashirika ambayo yalikuwa yanasimamiwa na Serikali na Dar es Salaam

pale kulikuwa kuna *UDA*. Leo ukitizama kwa mjomba wangu kule Lindi Mchinga pale kwa Mheshimiwa Mudhihir wakati ule enzi ya mabasi ya *TT Co*. Yanatembea, ajali zilikuwa aghalabu kuzisikia. Lakini leo hii mabasi ya binafsi yanapita, kuna lami pale, kwa hiyo, ajari zinaongezeka. Sasa baada ya kuja mfumo huu wa uchumi wa soko huria na kuongezeka kwa mabasi ya makampuni mengi ya binafsi mimi naamin kabisa Jeshi letu la Polisi limezidiwa katika Idara hii ya *Vehicle Inspection*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nieleze kwamba ajali hizi pia zinatokana na sababu mbalimbali. Lakini ajali kubwa zinasababishwa na ubovu wa magari au yaliyo chini ya viwango vinavyotakiwa kubeba abiria au mizigo na hivyo husababisha ajali nyingi sana kutokana na ubovu wao. Kwa mfano, takwimu zinaonyesha kwamba mwaka 2006 ajali zilikuwa 109,868, kuanzia Januari mpaka Desemba, 2007 Januari hadi Desemba ajali 230,751. Kuna ongezeko la ajali 120,883 sawa na ongezeko la asilimia 110 za ajali na kati ya hizi ajali za vifo zilikuwa 3,028 kwa mwaka 2006 na ziliua watu 2,657, mwaka 2007 ajali ziliongezeka zikawa 3,065 na watu waliokufa ni 3,071 ambapo ni zaidi ya watu 414 sawa na asilimia 15.6 ya waliokufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea sisi wenyewe Sheria hubadilika au hubadilishwa au hutungwa kulingana na mahitaji. Ushauri wangu ni kwamba wakati umefika tunahitaji sasa tuangalie upya Sheria hii ya usalama barabarani. Jinsi ya kurekebisha kipengele cha Sheria ya usalama barabarani kinachohusu ukaguzi wa magari na Jeshi la Polisi. Kuwe na utaratibu wa *compasory vehicle inspection,* utaratibu ambao utasaidiwa na *reputable private garages.* Ni utaratibu wa kawaida ambao unafanyika na nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Uingereza utaratibu huu upo, unaitwa *MOT* unafanywa na *Ministry of Transport,* lakini unapata *Certificate* ya *MOT* ambayo kila baada ya miezi kadhaa inategemea na gari lako kwamba umetumia kama ni usafiri wa basi, kama ni gari lako binafsi kwa muda gani ndiyo unafanyiwa *inspection* na kupewa *inspection report* ile kwamba wewe unapaswa sasa hivi kutembea barabarani na kupakia abiria. Sasa napenda kutoa ushauri kwamba tuangalie utaratibu huu kwamba Serikali ione kama inawezekana kutoa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii pia kwa Gereji binafsi wawe ma-*agents* wa Serikali watakaochaguliwa na Serikali chini ya Jeshi letu la Polisi kuweza kusaidia kuangalia kila baada ya muda fulani wenye mabasi, vipuri vyao: Je, viko salama? Matairi yao kweli yapo salama? Kwa sababu hawa wamiliki wa mabasi wanaweza kuwa wanayaleta tu mabasi barabarani, matairi yamekwisha, vipuri vile vimekwisha wakati wake, lakini wanaleta tu barabarani na wenye malori hivyo hivyo.

Kwa hiyo, wanasababisha matatizo makubwa ya ajali nyingi barabarani. Hata sisi wenyewe pia wenye magari binafsi inatuwia vigumu wakati mwingine unakuta tairi limekwisha, lakini unasubiri ukipata visenti ununue tairi mbili, matokeo yake ukitembea barabarani tairi zinapasuka zinatupotezea maisha. Kwa hiyo, lazima kuwe na *compulsory vehichle inspection* ambayo itatusaidia sana kupunguza ajali barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika haya masuala ya mabasi tuangalie sana masuala ya *Insurance* za mabasi. Hawa wenye mabasi wengi wao kwa kuokoa tu fedha zao hawaweki *comprehensive insurance.* Wao wanaweka *third part* magari mengi sana. Nina mfano hai wa ndugu yangu aligongwa na basi na basi lile lilikuwa lina *third part insurance*. Kwa hiyo,

tuangalie sana pia utaratibu wa kuona kwamba mabasi haya yanaweka *comprehensive insurance* kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi tena Namtumbo. Leo hii Jeshi letu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imetutengea fedha za kujenga kituo cha Polisi, lakini hatuna Magereza. Nimeanza kushawishi *In charge* wa *Prison* pale Mkoa wa Songea ili kuona kwamba tunaweka katika mchakato ujenzi wa Magereza. Tutakuwa na kituo pale cha Polisi, lakini hatutakuwa na Magereza na gharama ile ya kusafirisha Magereza kutoka Wilaya yetu ya Namtumbo kwenda mpaka Songea Mjini ambapo kwenye Magereza ambapo ni gharama kubwa sana. Kwa hiyo, ningeshukuru sana Magereza nao kwa mwakani nao wakatuwekea kwenye bajeti ili tuwe na Magereza pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naomba nizungumzie kuna malalamiko katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo za Kata kwamba wananchi wetu wanapomkamata mhalifu na kumpeleka katika chombo cha sheria yule aliyemkamata anaambiwa amgharamie mwananchi wake kumpeleka Mahakamani na kama hana fedha za kumgharamia na kumlipa askari yule na kumsafirisha basi yule mtuhumiwa atabaki pale pale au anaweza akaachiwa. Kwa hiyo, haya ni malalamiko makubwa ambayo yapo katika ngazi ya Kata, katika Mahakama zetu za Mwanzo katika Wilaya yetu ya Namtumbo wananchi wanalalamika sana na hili, ningeomba sana Serikali iliangalie na ilitolee wito kuona tunafanyaje ili kuepuka malalamiko ya wananchi wahalifu wanapokamatwa kugharamiwa na yule mshitaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie hapo, ni hayo tu ya Namtumbo na ya Dar es Salaam, yalishasemwa lakini kabla sijamalizia pia kuna jambo moja kwa kuwa muda wangu bado upo kuna jambo la usalama huu wa barabarani. Barabara zinapojengwa sijui wanahusisha vipi watu wa miundombinu na watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusiana na usalama wa watembea kwa miguu.

Sasa hivi kunatokea ajali nyingi sana kwenye hizi njia tatu. Barabara ile kutoka Mwenge mpaka kwenye makutano ya Barabara ya Ali Hassan Mwinyi imetengenezwa njia tatu na kunatokea ajali nyingi sana watu wanakufa sana. Kwa hiyo, naomba nitoe ushauri kama inawezekana maeneo yale yenye *traffic* ya watu kuvuka kila mara ziwekwe *pedestrians bridge* za kawaida tu hata za chuma na mbao kwa sababu watu wanakufa sana. Kuna taarifa za vifo vya watu kugongwa pale na hata kaka yangu aligongwa pale na nilisikitika sana kwa sababu ya urefu wa ile barabara. Kwa hiyo, ninaomba kwamba wakati ujenzi wa barabara hizi unajengwa wangeshirikisha pia Wizara ya Mambo ya Ndani kuona tunafanyaje kuepuka kugongwa kwa hawa watembea kwa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, kwa jioni hii, huyu ndiye Msemaji wetu wa mwisho. Kesho tukijitahidi sana wakati wa asubuhi tutakuwa na wasemajI 11 kwa maana ya kwamba matangazo yawe machache tunaweza kupata 11. Jioni tutataka mtoa hoja ajibu halafu tuingie kwenye Kamati ya Matumizi. Sasa tunalo tangazo la wenzetu ambao watakwenda kushiriki mazishi kule Tarime kesho. Kutakuwa na ndege mbili.

Ndege ya kwanza itaondoka saa 2.00 na watakaohusika na ndege hiyo ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Stephen Wassira, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Susan Lyimo. Waandishi wa Habari wa *TBC* atakuwa Abeid Buntu, Shaban Kisu na Noel Mtega na ndugu wa Marehemu wengine ambao ndugu Abeid Bukuru na Maria Adolf.

Ndege ya pili itaondoka saa 2.30, watakaohusika ndani ya ndege hiyo ni Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Eliata Switi, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Dr. James Wanyacha, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na tutakuwa na ndugu wa Marehemu tena ambao ni Furaha Bukuru na Frola Lyacho.

Kwa hiyo, *bus* litakuwepo hapa ofisini kama huna uwezo wa kufika mwenyewe pale Kiwanja cha Ndege. Naomba muhawi kwa sababu hii ni ndege, haitawasubiri kama mtakuwa mmechelewa na hivyo hivyo mtaelezwa kule ni ndege gani itatangulia kuondoka.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi ya siku ya leo, naomba tukapumzike na nakiahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge Liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 31 Julai, 2008 Saa 3.00 Asubuhi)*